

## **Kikao cha Nane – Tarehe 20 Machi, 2015**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

### **Dua**

*Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Mohammed Mussa) alisoma Dua*

### **MASWALI NA MAJIBU**

#### **Nam. 24**

#### **Chuo cha Mafunzo ya Sayansi ya Bahari**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (Kny. Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza:**

Kwa kuwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (TPDF) mbali na kufanya kazi ya ulinzi wa nchi yetu pamoja na mipaka yake yote kwa umakini mkubwa, vile vile limeanzisha taasisi mbali mbali za kuhudumia jamii kama vile Mahospitali, Vitengo vya Uhandisi katika fani mbali mbali, mashule na kadhalika. Na kwa kuwa Zanzibar ni Visiwa na tunacho kikosi chetu mahiri sana cha KMKM ambacho mbali na kudhibiti magendo nchini kupitia wataalamu wake, husaidia sana katika masuala ya uokozi pale yanapojitokeza majanga hususan ajali za baharini.

Je, ni lini Serikali itapanua bajeti pamoja na kukiwezesha kikosi hiki kuanzisha chuo cha kisasa kitakachotoa mafunzo ya sayansi ya Baharini pamoja na usafiri baharini (*School of Marine Science and Navigation*).

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 lakini kabla ya kulijibu swali hilo kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo KMKM kama ilivyo Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kinafanya kazi za ulinzi, kinatoa huduma za jamii ikiwemo Afya katika Kambi zake takriban zote na Hospitali yake ya Kibweni ni Hospitali kubwa na ya kisasa na inatoa huduma za rufaa kusaidiana na Hospitali yetu Kuu ya Mnazi Mmoja. Aidha, kinatoa mafunzo mbali mbali kwa wapiganaji wake ndani na nje ya Zanzibar na kina wataalamu wa kutosha katika fani zote zinazohitajika kwa kazi walizokabidhiwa kulingana na uwezo wa uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kulinganisha kiuwezo na Jeshi la Wananchi Tanzania kwa ukubwa wake na uwezo wa kirasilimali, lakini naomba niwapongeze sana wapiganaji wa KMKM kwa kazi nzuri na nzito ya ulinzi wanayoifanya, mafunzo wanayoyatoa kwa watendaji wake, huduma za kijamii na hata michezo wako juu sana. Ofisi yangu itawapa kila msaada unaohitajika ambao uko ndani ya uwezo wa Serikali tutashirikiana nao ili wapige hatua zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

KMKM wanacho Chuo cha kuwafunzia wataalamu wake wakiwemo mabaharia ambacho kipo Kama, Serikali inaendelea kukiimarisha Chuo hicho ili kiwe cha kisasa zaidi kadri hali ya uchumi inavyoruhusu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Kwanza nisije nikawa mchoyo nichukuwe fursa hii kumpongeza Waziri kwa umakini alivyojibu swali la msingi kwa nguvu ya hoja na vile vile fursa hii kuwapongeza KMKM kwa juhudi wanazozifanya kwa kusaidia jamii ikiwemo kuanzisha miradi ya huduma za tiba mbali na shughuli za ulinzi na usalama. Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri maswali mawili madogo sana ya nyongeza.

Ni lini Serikali itawapatia madaktari bingwa wa huduma zisizopatika zikiwemo za vipimo, lini Serikali itawasaidia vipimo ambavyo havipatikani hospitali ili sasa vipatikane kama ilivyo hospitali ya Jeshi la Wananchi ya Bububu, hilo moja.

Ulipokuwa ukijibu swali la msingi ulikiri na ulisema Serikali inasaidia, inasaidia kiasi gani kila mwaka kwenye vikosi vya KMKM, Mafunzo na Jeshi la Wananchi ili kupunguza msongamano katika hospitali ambayo inaitwa hospitali ya rufaa ya Mnazi mmoja ambayo haijafika kuwa hospitali ya rufaa hadi hivi sasa ninavyozungumza.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninazipokea pongezi ambazo amezitoa Mhe. Mwakilishi, kwa niaba ya wapiganaji wa kikosi cha KMKM.

Swali lake (a) nataka nimuhakikishie kwamba katika uajiri wetu wa vijana wa safari hii wamo madaktari bingwa ambao tumeshaelewana nao kuwaajiri zaidi ya madaktari watatu katika kikosi chetu, ili kukidhi haja ya matatizo ambayo yanafikia katika kituo chetu kile. Lakini ni kwa kiasi gani tutaliondosha tatizo hili ambalo linaikabili hospitali ya Mnazimmoja, kama nilivyojibu swali mama kwamba au kulingana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania lakini kama tutakuwa na uwezo gani wa kuweza kufanya kulingana na hospitali ya Bububu na hospitali nyengine za kijeshi.

Tuna mpango kabambe, tuna programu maalum kwa kushirikiana na wenzetu wa Marekani. Nataka nilihakikishie Baraza lako Tukufu kupitia Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, tumepata programu na msaada kutoka kwa wenzetu wa Serikali ya Marekani na programu hiyo tayari ipo katika hospitali yetu ya Kibweni na tunao mabingwa wawili kutoka Marekani, ili kuhakikisha kwamba hospitali yetu ya Kibweni inapata viwango ili kuweza kuwasaidia wananchi wa Zanzibar na wapiganaji wengine.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi niwapongeze sana kikosi hiki cha KMKM kutokana na jitihada zao ya kuleta jengo lile ambalo sasa hivi linakubalika katika sehemu za nchi za Afrika. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri nilikuwa nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, pale KMKM kuna mashine ambayo ilikuwa mtu akizama kwa *stage* ya mwanzo anatiwa mule kwa kusaidiwa ili viungo vyake pamoja na mengine yaweze kukamilika. Je, Mhe. Waziri mashine hiyo imeshatengenezwa na kama haijatengenezwa, una mpango gani Mheshimiwa kwa kutafuta mashine nyengine mpya, kwa sababu ile mashine ni muhimu sana kwa watu wanaozama baharini na hasa wanaotumia machupa ya *gas*.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, nataka nikubali au nipokee pongezi kwa niaba ya wapiganaji wa KMKM kama alivyoziwasilisha Mhe. Makame Mshimba. Katika swali lake ni kweli kwamba mashine iliyoko Kibweni ambayo ilikuwa na madhumuni ya kuweza kuwaokoa wananchi au jamii watakaopatwa na maafa baharini hivi sasa ni mbovu na haifanyi kazi. Nataka nimuhakikishie kwamba hata juzi nilipokuwa nikitoa maelezo ya utekelezaji wa maagizo ya kamati nilitaja kwamba Serikali inao mpango kupitia programu yake ya mafunzo ya kuwafundisha ma-*diver* wetu wa Kikosi cha KMKM.

Tunao mpango wa kuinunua mashine ile mpya ili ije isaidie katika uokozi wa majanga pale ambapo yanatokea. Kwa hivi sasa tuna mpango wa kununua mashine moja, lakini inavyotakiwa kutokana na huu ujenzi wa vituo vya maafa vinavyojengwa katika maeneo yetu yote, tunataka tuhakikishie kwamba kila kituo ipo mashine kama ile, ili linapotokezea tatizo kama lile tuweze kufanya kazi ya kuwasaidia au kuwaokoa wananchi.

## Nam. 25

### Kutotekelezwa Malengo ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

**Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny.Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza:**

Kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha robo ya tatu (Januari – Marchi) kwa mwaka wa fedha 2013/2014 malengo ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni pamoja na na kufanya juhudi za makusudi katika kuandaa mazingira kwa ajili ya kufanikisha uchaguzi Mkuu wa 2015 pamoja na kufanikisha kura ya maoni ya Katiba Mpya kabla ya 2015.

Je, ni sababu gani za msingi zinazopelekea hadi leo hii watu wenye sifa kuendelea kuhangaishwa katika kupata kitambulisho cha Mzanzibari kwa ajili ya kuingizwa kwenye Daftari la wapiga kura.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Wawi swali lake Nam. 25 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, uandikishwaji wa Wazanzibari Wakaazi unafanywa kwa kufuata Sheria ya Usajili wa Wazanzibari Wakaazi Namba 7 ya mwaka 2005 na hakuna watu waliotimiza masharti ya usajili ambao wamekataliwa usajili wala kuhangaishwa. Watu wote waliotimiza masharti ya Sheria na utaratibu husajiliwa na kupatiwa vitambulisho bila usumbufu wa aina yoyote.

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Ahsante Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Naomba nimuulize Mhe. Waziri hadi hivi sasa ni vitambulisho vingapi vipo ambavyo havijapatikana wenyewe na kama Wizara, itachukua hatua gani ili kuhakikisha vitambulisho hivyo vinawafika wahusika.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, naomba arejee swali kwa sababu nilipokuwa niki-*concentrate* nilikuwa nasikia mazungumzo mengine.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe naomba urejee swali ili Mhe. Waziri akusikie vizuri zaidi.

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Naomba nimuulize Mhe. Waziri hadi hivi sasa ni vitambulisho vingapi vipo Ofisini kwa Mrajis ambavyo havijapata wenyewe na kama havitachukuliwa na wenyewe wizara ina mpango gani kuhakikisha vitambulisho hivyo vinawafika wahusika.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, sina takwimu sahihi hapa za vitambulisho ambavyo wahusika hawajenda kuvichukua. Lakini kwa ufupi vipo vitambulisho vingi sana ambavyo havijenda kuchukuliwa na wahusika, na hii idadi gani basi naomba niilete kwa Mhe. Mwakilishi kwa maandishi.

Swali la (b) tutafanya nini baada ya kuona vitambulisho hivyo vimekaa kwa muda mrefu havijachukuliwa. Tutachukua hatua ya kuweza kuvifuta katika *register* yetu, katika *database* yetu kwa sababu vitakuwa hawajatokea wenyewe, hiyo ndio hatua ambayo tutaichukua baadae.

### **Utaratibu**

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, swali la msingi nililiuliza mimi lakini kwa bahati mbaya kidogo nilichelewa kutokana na kwamba nilikwenda hospitali kupata matibabu. Leo mwenyewe nimerudi nasimama kwa ajili ya kuuliza swali la nyongeza unaninyima, hunitendei haki. Kwa hivyo naomba uniruhusu niulize swali la nyongeza kutokana na swali langu la msingi Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe naomba tukubaliane kitu kimoja anapotokezea mtu akauliza swali katika eneo hili utaratibu wangu nampa mwenye swali lake, akimaliza nampa mtu upande huu ili aweze kuuliza swali la nyongeza. Na nikimaliza upande huu naelekea upande mwengine ili niweze kupeleka swali jengine la nyongeza. Utaratibu niliojiwekea mimi, ili kuondoa mtafaruku kwamba usiangalie upande mmoja. Na hayo waheshimiwa wajumbe mnayasababisha wenyewe. Kwa utaratibu huo kwa vile wewe ilikuwa ndio mwenye swali lako la msingi, na kwa kuwa mimi nilikuwa nimeshampa Salma ambaye alikuwa amesimama kwa upande mwengine labda nimuombe radhi Mhe. Salma na nikurejeshee wewe, kwa sababu swali lako lilikuwa la msingi kama ambavyo tunakubaliana katika utaratibu huo. Lakini utaratibu wangu ndio huo, likimalizika swali upande mmoja naelekea upande mwengine, sio maswali yote yaelekee upande mmoja.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwanza kwa kunipatia hii nafasi lakini kabla sijauliza swali la nyongeza, ni kwamba sisi hapa Baraza linatumia *standing orders* yaani Kanuni za Baraza, linaendeshwa kwa mujibu wa Kanuni kwa hivyo ningepomba sana tufuate zaidi Kanuni kulikoni utaratibu wa kujipangia wenyewe. Baada ya maelezo hayo naomba nimuulize Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa vitambulisho vya uzanzibari ndio kila kitu katika nchi hii, hiyo ndio ajira, hiyo ndio usafiri na ndio kila kitu. Na kwa kuwa kuna watu ambao takriban wana sifa zote za kupewa hiki kitambulisho na kwa kuwa masheha

kwa kushirikiana inaonekana na taasisi za vitambulisho kwa makusudi mazima wanawanyima watu wenye sifa za kupewa vitambulisho kwa sababu za kisiasa.

Je, Mhe. Waziri ikiwa mtu mwenye dhamana ya vitambulisho pale nchi itakaporipuka kutokana na watu kunyimwa haki zao za vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, Ofisi yako itabeba lawama kwa hili.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimuhakikishie kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itajitahidi sana kwa kushirikiana na wananchi wapenda amani kwamba nchi hii isiripuke, hilo nataka nimuhakikishie.

Pili suala la vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, ninakubaliana nae kwamba ndio kielelezo cha msingi cha mambo mengi yanayowapa fursa wananchi wakaazi wa Zanzibar. Katiba ya mwaka 1984 imetambua kuwepo kwa Sheria ya Mzanzibari, lakini katika kupata hicho kitambulisho cha Mzanzibari kuna taratibu lazima zifuatwe. Sasa ningewaomba Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi kwa jumla kwamba katika kufatilia haki zao, basi ni vyema wakafata taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria badala kutaka kupita njia za mkato.

Mimi kama Waziri tokea nimeingia ofisini kwangu sijapokea barua ya mwananchi yeyote yule aliyenimwa haki hiyo katika ngazi zinazohusika na akamalizia kwangu, kama waziri ambaye ndiye niliyetajwa kama nitabeba lawama. Sasa nawaomba wananchi wafate utaratibu uliopo kwa mujibu wa sheria kama wananyimwa haki wafate hizo taratibu, ili tuone tatizo lipo kwa kiasi gani.

#### UTARATIBU

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, Kanuni zetu zinatutaka kwamba waziri au mtu yeyote anapokuwa na anasema katika Baraza hili awe na uhakika na maneno anayoyasema, na Mhe. Waziri kama atakumbuka wawakilishi wa wananchi wasiopungua sita nikiwemo mimi tulimwendea kumwambia tatizo la vitambulisho vya Uzanibari ukaazi na akaahidi atafuatilia katika majimbo yetu, lakini hadi leo hii hakufanya chochote. Je, katika hili Mhe. Waziri atakubali kwamba ametupotosha wawakilishi wa wananchi katika suala la vitambulisho.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum:** Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikijibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi nilisisitiza na watu wa mwanzo niliowataja ni Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa kufahamu kwamba kupitia Mnadhimu wao wa Chama cha CUF waliniomba kukutana nao, na nilikutana nao na nikawaahidi kwamba ningeweza kufuatilia na ndio maana nilisema kwenye ofisi yangu hakuna lalamiko lolote la mwananchi ambaye ameleta kuona kwamba amenyimwa haki hiyo. Na nikawataka Waheshimiwa Wawakilishi wafate sheria na wananchi wafate sheria.

Utaratibu uliopo ni kwamba pale mwananchi mwenyewe sio kwa kumtumia mtu wala mwakilishi wake, mwakilishi wake anayo nafasi ya kuja kuzungumza hapa kama Mhe. Mwakilishi alipouliza swali, hiyo ndio haki ya mwakilishi kuwawakilisha wananchi wake kwa kuuliza swali au kuhoji ndani ya chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi.

Lakini kwa yule mwananchi ambaye anahisi amenyimwa haki hiyo anatakiwa yeye mwenyewe kama amekwenda kwenye Ofisi ya Wilaya amenyimwa haki hiyo aende kwa Mkurugenzi wa Usajili wa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi alalamike. Na kama kwa Mkurugenzi hakupata fursa ya haki hiyo basi aje kwa waziri, jambo hilo ninavyotaka kusema halijafanyika. Sasa nawaomba wananchi wafate huo utaratibu halafu tuweze kushughulikia matatizo hayo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, maswali matatu yamekwisha naona mmesimama tena, watu watatu wamemalizika, haya Mhe. Salma malizia kwa sababu nilikuwa nishamtaja, Mhe. Salma Bilal malizia.

**Mhe. Salma Mussa Bilali:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumuliza swali la nyongeza la mwisho Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri kwa kuwa sheria ya upatikanaji wa vitambulisho ya Mzanzibari ilipitishwa na Baraza lako...

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, naomba utulivu, Waheshimiwa Wajumbe tunaomba utulivu.

**Mhe. Salma Mussa Bilal:** Na kwa kuwa inaonekana baadhi ya viongozi bado hawajaelewa sheria hii vizuri. Je, Mhe. Waziri huoni kwamba iko haja ya kutupatia mafunzo au semina zaidi sisi viongozi ili tukawaelimishe wananchi wetu ili wapate kuielewa sheria hii na kufuata utaratibu unaotakiwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum:** Mhe. Mwenyekiti, ofisi yangu inaendelea kutoa taaluma kwa wananchi wa Zanzibar kupitia vyombo vya habari kama radio na televisheni. Ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, tunaomba utulivu, tunaomba utulivu Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Nassor kaeni kitako, tunaomba utulivu, tunaomba utulivu.

## UTARATIBU

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, naomba utulivu, Mhe. Nassor naomba utulie, Mhe. Nassor kaa kitako, Mhe. Hija.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nataka unipe nafasi ili wajumbe wanisikilize. Mhe. Mwenyekiti, natumia Kanuni ya 37.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hakika tangu niwe mwakilishi wa Baraza hili...

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, wanaoendelea na zogo nitawatoa nje, nasema nitawatoa nje na si jambo zuri kwa Mhe. Mwakilishi kutolewa nje. Mhe. Hija tunaendelea.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nakuomba udhibiti Baraza hili na haya ni matokeo ya kuvuka utaratibu, unapovuka utaratibu Mwenyekiti unasababisha matatizo kama haya.

Mhe. Mwenyekiti, natumia Kanuni ya 37 nimekuwa mwakilishi kwa kipindi cha miaka karibu kumi hivi sasa, nimeshuhudia baadhi ya mawaziri wakisema uongo sana katika Baraza hili. Kanuni ya 37 Mhe. Mwenyekiti naomba ninukuu.

“Waziri au Mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi isipokuwa kwamba suala aliloulizwa waziri mmoja linaweza kujibiwa na waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu”.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hakika mawaziri wengi baadhi yao wamekuwa wakisema uongo humu ndani. Sasa mimi natumia Kanuni hii kusema kwamba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ anaendelea kusema uongo katika Baraza hili. Sasa utaratibu wa uongo ni moja tu Mwenyekiti, ni kwamba ili tupate ukweli maana yake wawakilishi wanasema uongo kwa tafsiri ya serikali na mawaziri wanasema uongo kwa kuwapotosha wawakilishi. Kwa hivyo, uongo kwa tafsiri ya wananchi, mwananchi maana yake ni mwakilishi maana yake serikali imekuwa ikisema uongo.

Kwa tafsiri ya serikali wawakilishi wamekuwa wakisema uongo maana yake hiki ni chombo cha kusema uongo. Kwa hivyo, mimi natumia kanuni hii kutaka utaratibu upitishwe tuchunguze juu ya nani mkweli kati ya serikali na wawakilishi. Mimi Hija Hassan Hija ikiwa sina sina wananchi ambao wametimiza masharti kamili niko tayari kujiuzulu. Je, Mhe. Waziri kama amedanganya yuko tayari kujiuzulu.

## UTARATIBU

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nimemsikiliza mjumbe mwenzangu sina tatizo naye katika kauli yake na watu nataka wanifahamu vya kutosha, na namshukuru kwa kusoma kifungu cha Kanuni alichokieleza juu ya Mhe. Waziri kusema uongo. Mimi nataka Mhe. Mjumbe aliyekaa atuthibitishie huo uongo kwa kifungu alichokitumia ili Mhe. Waziri apate kujibu hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, hiki chombo chetu ni chombo kikubwa sana tunapofika pahala tukafanya mambo ambayo kinyume na taratibu za kikanuni na sheria zetu itakuwa ni jambo moja ambalo

halipendezi huko nje kwa watu ambao wanatushuhudia hapa. Sasa ningeliomba yale mambo na taratibu ambazo tumeziweka humu ndani tuwe tayari kuzifuata wenyewe. Mimi sijaona tatizo bado liko wapi mpaka dakika hii, isipokuwa kuna hoja ya Mhe. Hija ndio hoja ambayo inatakiwa ijibiwe ya msingi kama ambavyo ame-raise yeye mwenyewe katika Baraza hili. Lakini mambo mengine yote yaliyopita nyuma tatizo lake mimi silioni liko wapi, naomba sana tuendeshe Baraza letu kwa mujibu wa taratibu, si vizuri watu wazima kuadhibiana humu ndani wakati sisi ni wawakilishi wa wananchi katika maeneo mbali mbali. Naomba sana taratibu na sheria na kanuni zifuatwe humu ndani. Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum:** Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hija ameelezea utaratibu juu ya kanuni ambayo ameitaja na kunitaka mimi kusema kwamba mimi nimesema uongo. Lakini kifungu hicho kinasemaje naomba kunukuu.

Wajibu na mipaka ya kujibu swali, kifungu cha 37 (1)

“Waziri au Mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi isipokuwa kwamba swali aliloulizwa waziri moja linaweza kujibiwa na waziri mwingine au na Mwanasheria Mkuu”.

Kifungu kidogo cha (2) kinasema:

“Endapo Spika ataona kwamba waziri au mjumbe aliyeulizwa swali hakujibu swali aliloulizwa anaweza kumtaka waziri au mjumbe huyo ajibu swali aliloulizwa”.

Maswali yote matatu niliyoulizwa nimejibu, utaratibu uliolezwa nimejibu, sasa sioni kama nimesema uongo. Mwaka 2005 Baraza la Wawakilishi lilipitisha sheria Nam. 7 ya mwaka 2007 iliyoipa serikali mamlaka ya kuanzisha rasmi Afisi ya Usajili na kadi za utambulisho ambayo inayo wajibu wa kuhakikisha kuwa Wazanzibari wakaazi wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea wanasajiliwa na kupatiwa kadi za utambulisho. Aidha, kwa sheria hiyo, Wazanzibari wote wenye sifa ya ukaazi na waliotimia umri wa miaka 18 na kuendelea wanalazimika kwenda katika ofisi za Usajili za Wilaya kwa ajili ya kusajiliwa na kupatiwa vitambulisho.

Mamlaka ya kuanzisha Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho yametokana na Katiba ya Zanzibar mwaka 1984, ibara ya 6, kifungu kidogo cha (1) ambayo inatambua kuwepo kwa Mzanzibari ambaye taratibu zake zitategemea na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

Pia kuna sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi Nam. 5 ya mwaka 1985 ambayo imemueleza nani Mzanzibari pamoja na sifa zake. Kutokana na misingi hiyo ndio Baraza la Wawakilishi limetunga sheria ya kumsajili, kumtambua na kumpatia kitambulisho Mzanzibari aliyetimiza masharti ya kisheria .

Sheria Nam. 7 ya mwaka 2005, sheria hiyo kifungu cha (6) imetoa mamlaka kwa Mkurugenzi kuwasajili Wazanzibari waliotimiza masharti ya kisheria na kuwapatia kadi za utambulisho na kuweka kumbukumbu zao.

Kwa mujibu wa sheria Nam. 7 kifungu cha 7 (1) kimemlazimisha kila Mzanzibari mkaazi ambaye ametimiza masharti ya kisheria kusajiliwa. Kanuni ya 3 na ya 4 ya mwaka 2005 ya hiyo sheria wajumbe tuvumiliane anaposema mwingine anasikilizwa.

Kanuni ya 3 na ya 4 ya mwaka 2005 pia inaelezea ulazima wa Mzanzibari mwenye sifa za kisheria kusajiliwa katika Ofisi za Usajili za Wilaya anayoishi. Kwa masharti ya kwamba yeye mwenyewe atafika mbele ya Ofisa wa Usajili wa Wilaya baada ya kupata barua ya uthibitisho kutoka kwa sheha wa shehia anayoishi. Muhusika baada ya kupatiwa barua hutakiwa kufika katika Ofisi ya Usajili ya Wilaya na kujaza fomu maalum ya maombi, baadae fomu hiyo hutakiwa kuthibitishwa tena na sheha aliyetoa barua hiyo ndipo anapoiwasilisha ofisi kuu kwa lengo la kutengenezewa kitambulisho.

Sasa mimi siuoni uongo ambao nimeusema. Ahsante sana Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, naomba busara zitumike, naomba sana busara zitumike, Mhe. Hija ulisimama kwa ajili ya utaratibu na mimi niliridhia hilo au kiti kiliridhia hilo na baada ya maelekezo yako tukamtaka Mhe. Waziri atoe ufafanuzi juu ya jambo ambalo ulikuwa una mashaka nalo. Sasa kama hukuridhika Mhe. Hija

utaratibu unaujua; utaratibu uko wazi kwa hoja ambayo unaihisi kwamba bado ina utata kwa hiyo fuata taratibu zake ambapo wewe unaelewa. Wewe ni kiongozi ambaye mwenyewe umeelekeza. Hiki ni kipindi cha maswali na majibu na waziri ametakiwa kujibu hoja, hoja waziri amejibu tena nini cha ziada Mhe. Hija.

Kama hilo halitoshi hoja hii ya kitambulisho ina siku zake maalum ambazo zimewekwa itakuja kujadiliwa kwa kina, tunapata matatizo gani ndugu zangu. Tunazo siku mbili nzima au siku moja na nusu ya kujadili jambo hili kwa nini tunatoa vitu ambavyo havieleweki.

Naomba sana Waheshimiwa Wajumbe tukubaliane, tuheshimu maamuzi ya Baraza, taratibu ziendelee, siku itakapofika kila mmoja atazungumzia, kuna siku moja na nusu nzima kwa ajili ya suala hili tutazungumza sote kwa umoja wetu. Naomba tuheshimiane na naomba tuendelee na taratibu nyengine.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, mimi sina hoja ya vitambulisho, hoja ya Mhe. Hamad Masoud, nina hoja ya kulinda nidhamu ndani ya Baraza ya uongo. Nimesema hivi mara nyingi wawakilishi wanadai kwamba kuna hoja hii na mawaziri wanakataa maana yake mmoja kati ya hawa ni muongo ndio hoja yangu. Sasa kama Mhe. Waziri anasema kwamba sifa ni miaka 18, sifa ya miaka mitatu ya ukaazi, sifa ya Mzanzibari mimi ushahidi ninao muunde utaratibu wa kumuona nani muongo kati ya mimi na serikali.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Hija Hassan naona hujanifahamu, maana yeke umesema waziri hakutoa maneno ambayo ni yake mwenyewe. Mhe. Waziri amesoma sheria kwa utaratibu ambao tuliupitisha sisi wenyewe hapa.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Na mimi nazungumzia sheria, sizungumzii nyimbo hapa.

**Mhe. Mwenyekiti:** Sheria inatungwa katika Baraza hili la Wawakilishi la Zanzibar ndicho ambacho Mhe. Waziri amekuja kukikariri na amesema kwamba, kwa mujibu wa maelekezo ambayo sote tumeyashuhudia je, uongo wake uko wapi? Ndio hoja ya Mhe. Waziri, sasa kama kuna la ziada katika hili Mhe. Hija Hassan naomba tuheshimiane, naomba taratibu za kibunge zichukue nafasi yake ili uweze kuwasilisha hilo suala lako, sasa katika utaratibu kwamba ikiwa wewe hukuridhika kama vile ilivyo kawaida yetu. Naomba kwa hapa tufikie mwisho tuendelee na mambo mengine. Ahsante katibu. (*Makofi*)

### Nam. 73

#### Usumbufu wa Wanafunzi Katika Skuli ya Mtule

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-**

Hivi majuzi katika Jimbo la Muyuni kumefunguliwa skuli katika eneo la Mtule na kusababisha usumbufu kwa wanafunzi wanaokwenda katika skuli hiyo, pia pamoja na wazee wao.

- Kutoka Pete hadi skuli hiyo ilipo ni kilomita ngapi na kutoka Jambiani hadi Mtule ni kilomita ngapi.
- Ni sababu gani zilizofanya kuachwa kwa mabanda matatu matupu katika Skuli ya Kitogani na kuwapeleka hapo Mtule.
- Je, wizara haioni suala hili kuwa litaleta usumbufu kwa wanafunzi na kusababisha wengine kukosa elimu ya *Qur-an* wakati wakirudi nyumbani huwa ni usiku. Je, huku ni kujenga au kubomoa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 73 lenye vifungu (a), (b) na (c).

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba wizara imefunguwa skuli mpya za kisasa za Sekondari Mtule katika Jimbo la Muyuni ambayo imejengwa kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Dunia. Kufunguliwa kwa skuli hiyo kumekamilisha ufunguzi wa skuli 19 za sekondari zilizojengwa kupitia mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima. Kufunguliwa kwa skuli hizo ambazo zina vifaa vya kutosha na walimu wazuri, zimechangia kwa kiasi kikubwa katika ufaulu wa wanafunzi wetu katika mitihani yao ya Kidato cha Pili na Kidato cha Nne.

Kwa upande wa skuli ya Sekondari ya Mtule, jumla ya wanafunzi 110 wa Kidato cha Kwanza hadi cha Nne kutoka Skuli ya Kitogani wamehamishiwa katika skuli hiyo. Napenda ieleweke kuwa wanafunzi wote waliohamia katika skuli hiyo mpya wanatoka katika vijiji vya Pete, Muungoni na Kitogani tu, na hakuna wanafunzi wanaotoka katika kijiji cha Jambiani. Aidha, kufunguliwa kwa skuli hiyo kunakwenda sambamba na ahadi ya serikali yetu ya kujenga skuli za kisasa katika maeneo yote ya nchi yetu, iwe mijini au vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim kama ifuatavyo:-

- a. Kutoka Pete hadi ilipo skuli ya Sekondari ya Mtule ni kilomita nne na nusu (4.5km) na kutoka Jambiani hadi Mtule ni kilomita sita (6 km).
- b. Madarasa matatu yaliopo katika Skuli ya Kitogani yaliyobakia baada ya kuhamishwa kwa wanafunzi hao, kutatoa nafasi nzuri kwa skuli ya msingi ya Kitogani kuwa na nafasi ya kutosha ya kufundishia shughuli nyengine za kielimu kama vile vyumba vya kufanyia mitihani na nafasi tupu za madarasa itakuwa ni akiba kwa ajili ya uandikishaji wa wanafunzi wapya hapo mwakani. Sera yetu ya Elimu ya mwaka 2006 imeelekeza kutenganisha madarasa ya skuli za Msingi na ya Sekondari (ambazo kwa sasa zinaitwa Msingi na Kati) kwa awamu.

Hivyo madarasa ya Sekondari kupitia Skuli ya Kitogani yaliyohamishwa katika skuli mpya ya Mtule yenye kukidhi haja ya skuli ya Sekondari kwa kuweco huduma zote muhimu zinazohitajika kwa wanafunzi wa ngazi hiyo, ikiwemo maabara za kisasa, Baiolojia, Kemia na Fizikia, chumba cha Kompyuta na Maktaba. Uamuzi kama huu wa kuzitenganisha madarasa skuli za Msingi na Sekondari, umefanywa kwa wanafunzi wa Sekondari nyengine ikiwemo Jumbi Msingi kuhamia Jumbi Sekondari, Kombeni kuhamia Dimani kwa Unguja na kwa na kwa upande wa Pemba Sizinzi kuhamia skuli mpya ya Sekondari ya Chwaka Tumbe na Finya kuhamia skuli mpya ya Wete Sekondari.

Napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kuanza kufanya kazi kwa skuli hiyo kutachangia maendeleo makubwa ya elimu katika skuli hiyo na Jimbo la Muyuni kwa jumla. Ni vizuri tukafanya subira kuona maendeleo yatayoletwa kwa kuweco skuli hiyo.

- c. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haina nia ya kuwasumbua wanafunzi kwa kusoma *Qur-an* kama muhusika alivyoeleza. Pia napenda ieleweke kuwa katika hiyo skuli ya Mtule wanafunzi wanaingia mkondo mmoja tu na wanatoka saa 7.15 na hivyo wanafunzi watapata muda wa kutosha wa kurejea majumbani kwao na kuhudhuria Madrasa kwa wakati muwafaka.

Pia mwananchi mmoja mzalendo mkaazi wa Jozani amejitolea kutoa huduma ya usafiri wa kwenda na kurudi kwa wanafunzi wote 110 kwa gharama ya Shilingi 100 na Shilingi 100 kurudi. Kwa huduma hiyo inawasababisha wanafunzi kufika skuli kwa wakati na kurejea majumbani kwao kwa wakati.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti ahsante sana. Kwanza nichukue fursa hii kuipongeza serikali kwa kutekeleza vizuri sera yake ya elimu na niweze kumpongeza Mhe. Naibu Waziri binafsi yangu nisiwe mchoyo kwake kwa umakini wake anapokuwa akijibu maswali. Baada ya maelezo hayo naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa skuli hiyo iko umbali mkubwa na huduma za usafiri bado hazijawa na uhakika hata kidogo, ukizingatia kipindi hiki sasa ni cha mvua na gari yenyewe ni *carry* nyepesi kuyumba na kuanguka badala ya kutengeneza tukaja tukabomoa. Ni lini kama wizara mtapeleka usafiri wa uhakika na kama mtapeleka mimi nitakuwa sina pingamizi wa suala hilo, ile gari inaweza kuharibika na hana gari mbili wala tatu yule mtu. Bado hali ni tete katika skuli ile kwa wanafunzi. Sasa lini mtapeleka usafiri wa uhakika ili kupunguza tatizo hilo.

Pili, pamoja na kuwa mfadhili kajitokeza bado wanafunzi wana wakati mgumu sana na mabanda bado kama matatu, hata wakipelekwa wanafunzi kuandikishwa bado yatabaki kuwa ni matupu. Hili suala nawaambia kwa busara zao wakaliangalie tena upya. Wakati wa mvua gari ni moja...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Jaku Hashim Ayoub unauliza swali la nyongeza au unatoa maelezo sasa, tunaomba uulize swali la nyongeza.



**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** *Hewallah* Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Naibu Waziri amenielewa swali langu la msingi likoje, bado hali ni tete lini watapeleka usafiri wa uhakika kama wizara.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza ikumbukwe kama skuli hizi ni skuli ambazo tulikusudia ziwe za mfano katika mawilaya na *package* yake ya mwanzo ya skuli hizi tulikuwa tumekusudia ziwe na *boarding* ili wanafunzi wa wilaya nzima zile *cream* tuweze kuzichukua na kuzipeleka pale. Lakini kutokana na kuwa ujenzi huu ulianza kuchelewa mpaka tulipofikia kujenga ikawa gharama za majenzi zimepanda.

Hata hivyo, nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba nia yetu ile ya kwanza skuli hizi kuzijengea dakhalia ili wanafunzi wawe na utulivu wa kukaa na kusoma masomo yao bado upo, na tunatizama ni njia gani ambapo tutafikia lile lengo la Wizara ya Elimu na serikali kwa jumla.

Jengine kwanza nataka nimpongeze pia huyu ndugu yetu Suleiman Issa maafuru Manyota ambaye yeye binafsi amejitolea kutoa hii gari na kuwapeleka wanafunzi wetu kwa gharama ndogo. Nimuombe Mhe. Mwakilishi awe mstahamilivu wizara hivi sasa tuna mpango wa kujaribu kutafuta uwezekano wa kuweza kuwasaidia wanafunzi wetu hawa ambao wanatoka mbali, lakini bado haujafikia pahala pazuri *Inshaallah* sidhani kama kutaharibika jambo lolote. Nitoe wito kama nyinyi Wawakilishi na Wabunge ambao mpo katika haya majimbo pia msaidie hii jitihada ambayo wananchi wengine wameonesha kujali hizi jitihada za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa skuli ile iko mbali sana na wanafunzi kama alivyotoa maelezo kwamba kuna kilomita nne na nusu na kuna wanafunzi wengine wanakaa umbali wa kilomita sita. Na kwa kuwa azma ya serikali ni kujenga dakhalia katika skuli ile lakini mpaka leo azma hiyo bado serikali iko mbioni.

- (a) Ni lini hasa inatarajiwa kujengwa dakhalia skuli ile ili wanafunzi hawa waepukane na usumbufu wa kwenda na kurudi.
- (b) Nimpongeze na mimi huyu bwana mkubwa Suleiman Issa kwa kutoa msaada wa kujitolea kutoa gari yake kwa nauli ya shilingi 100. Je, wizara mbali ya kumpongeza itamsaidia nini kijana huyu aliyejitolea kiuzalendo ili kuungana naye katika kuwasafirisha wanafunzi hawa. Ahsante Mheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuongeza majibu ya Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali aliyoyajibu kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Napenda pia kuliongezea hili suala alilolizungumzia Mhe. Mohammed Mbwana Hamad kwamba lini tutajenga hiyo dakhalia. Alivyozungumza Mhe. Naibu Waziri ni sahihi kwamba nia hiyo ipo na hivi karibuni tumezungumza na Benki ya Dunia inayotukopesha kuzijenga skuli hizi 19 ikiwemo Skuli ya Paje Mtule. Suala la kupunguza baadhi ya vitu alivyoviahidi lilikuja baada ya bei kupanda kutokana na yale matokeo ya mwanzo yalivyowekwa.

Wajumbe hawa wamekuja mara ya pili kuzungumza na sisi tumewapa *priority* zetu katika zile walizozikata wao na moja ni hiyo ya ujenzi wa dakhalia. Napenda kulihakikishia Baraza hili tukufu kwamba dhamira hiyo ipo suala hilo limeshakubaliwa mazungumzo yaliyobakia ni madogo sana ili tuanze kuzijenga dakhalia kwa haraka. Dakhalia tutakayojenga ya mwanzo ni ya Paje, Mtule kutokana na tatizo la masafa ya wanafunzi ambao wanasoma katika skuli hiyo. Ahsante sana.

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Swali (b) nilitaka kujua kuwa huyu Bwana Suleiman Issa kwa kujitolea kwake kwa gharama ya kuwasaidia wanafunzi wizara itaungana naye vipi katika suala hili la kuwasafirisha wanafunzi ili kuondoa usumbufu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Elimu:** Mhe. Mwenyekiti, wizara tunashirikiana naye huyu ndugu ambaye anasaidia, Suleiman Issa na ndio maana nikawa ninajibu kwa sababu ninajua na kwa

sababu tumefuatilia na kukaa naye tukajua kwamba kazi hii ataifanya ndio mashirikiano yetu makubwa ambayo tunampa.

**Mhe. Asha Abdu Haji:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wamefungua skuli katika Wilaya ya Kusini Jimbo la Muyuni, na kwa kuwa skuli hii wamesema kwamba kuna vifaa vyote vimekamilika. Je, wamepeleka walimu wangapi wa sayansi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, idadi kamili ya walimu tuliopoleka wa sayansi nitampa kwa maandishi, lakini ninalolijua kama katika skuli hizi 19 ambazo tumezifungua zote zimepata walimu wa ndani ya nchi na nje ya nchi wakiwemo nchi ya Nigeria ambao tuliwapata hivi karibuni.

#### Nam. 74

#### Tatizo la Kukosekana Umeme Skuli ya Pete

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-**

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuuliza swali Nam. 74 naomba niishukuru wizara kwanza kwa mtego walioutumia wa kujaribu na wamefanikiwa kwa kiasi fulani lakini naona huko mbele kutakuwa na athari. Baada ya maelezo hayo naomba kujibiwa swali langu Nam. 74 ambalo ni mtumishi tu mimi hapa wa wananchi wa Jimbo la Muyuni na huu uwakilishi umetokana na wananchi wa jimbo hilo.

Skuli ya Pete kwa muda mrefu sasa wamekuwa na kilio cha ukosefu wa umeme waliopewa na Mhe. Dkt. Amani Abeid Karume ambaye anastahiki pongezi kwa jitihada alizozichukua kwa wananchi wa Pete pamoja na skuli yenyewe. Kwa muda mrefu sasa hili halijakamilika Kamati ya Skuli ilikuwa ikienda kununua umeme imekatwa Shilingi 5000/= ili kupunguza deni hilo wakati hiyo ilikuwa kauli ya Kiongozi wa juu. Kamati ya Skuli ya Pete imekaa na Meneja wa Shirika la Umeme pamoja na Mwakilishi wao wa jimbo hilo na kufikia muwafaka kuwa waandike barua kwa bodi ili lipatiwe ufumbuzi na barua hiyo imeandikwa karibu nusu mwaka mpaka leo hii hakuna majibu.

Serikali inatoa kauli juu ya usumbufu huo kwa Skuli ya Pete

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 74.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa Mhe. Amani Abeid Karume, Rais Mstaafu wa Awamu ya Sita wa Zanzibar alitoa ahadi ya kuingiziwa umeme katika Skuli ya Pete wakati wa sherehe za kuifungua skuli hiyo mwaka 2005. Ahadi hiyo imetekelezwa na Shirika la Umeme na imeingizwa huduma ya umeme skuli hiyo iliyotekeleza agizo hilo. Ofisi ya Rais ilitoa Shilingi 7,691,146/= kwa kuilipa ZECCO na kufikisha huduma hiyo hapo skuli. Hata hivyo, katika mwezi Oktoba 2009, Shirika la Umeme lilimuandikia Mwalimu Mkuu Skuli ya Pete na kumuarifu kuwa skuli yake inadaiwa Shilingi 2,495,322.29 kutokana na kazi ya kuingiza umeme katika skuli hiyo. Deni hilo limefanya gharama ya kuunganisha umeme katika skuli hiyo kuwa ni Shilingi 10,186,468.29. Mazungumzo yalifanyika katika vipindi mbali mbali baina ya Afisi ya Rais Ikulu, ZECCO na wizara yangu na suala hilo lilipatiwa ufumbuzi kwa deni hilo la umeme.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba, hivi sasa Skuli ya Pete haina deni lolote la umeme la Shirika la ZECCO. Deni la shilingi 2,495,322.29 la siku za nyuma limeingizwa katika madeni ya nyuma ya wizara kwa Shirika la ZECCO. Napenda kuwahakikishia walimu, wanafunzi na wazazi wa Skuli ya Pete kuwa hakutokuwa na usumbufu wowote kwa ZECCO kwa suala hilo. Hata hivyo, tunawashauri kuwa waangalifu kwa matumizi ya umeme kutokana na gharama kubwa za nishati hiyo.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza niendeleo tena kuchukua fursa hii kumpongeza Rais Mstaafu kwa nia njea kwa wananchi wake Dkt Amani Abeid Karume kwa kuisaidia skuli hii. Vile vile Mhe. Naibu Waziri hili swali hata lilikuwa si upande wake lakini sijui lilikuaje kutoka kwake. Hili suala ni la mambo ya Shirika

la Umeme Mhe. Ramadhan Abdallah Shabaan suala hili mara 3 kulileta ndani ya chombo hiki imekuwa kama kinyonga. Jawabu unayoipata inakubaliwa baada ya muda inarudiwa tena pale pale bei ya pilipili hoho mara ya tatu kuuliza suala hili.

Mara ya mwisho wananchi wangu au Kamati ya Skuli tulikwenda kwa Meneja wa Shirika la Umeme akasema deni havezi kulifuta mpaka paandikwe barua, barua hiyo imeandikwa na jawabu yale haijapatikana mpaka hivi sijui kama karatasi hakuna au peni ya kuandikia hakuna.

Hili swali linajirudia kwa mara ya tatu na linanipa shida kuuliza suala hili.

- (a) Mnahakikisha vipi likijirudia na Naibu Waziri keshajibu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeshajibu *reference* hapa ninazo.
- (b) Jukumu la kuunganisha umeme kuendesha gharama za Skuli ni la wizara au skili yenyewe, ukilinganisha wananchi wenyewe hazitoshi huko kuna walimu wengine inabidi kulipia mimi walimu wa skuli kutokana na kuwa kidogo malipa mimi mshahara.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo wa Amali:** Kwanza Mhe. Jaku Hashim Ayoub serikali inafanyakazi pamoja. Hili ni suala la *ZECO* kweli lakini kama Wizara ya Elimu kwa sababu suala hili linatokana na skuli ni juu yetu kulisimamia na tukaona linakwenda vipi.

Mhe. Mwakilishi ni juu tu tarehe 13/3/2015 tulikutana na wenzetu wa Ikulu na *ZECO* tukazungumza nao na wao wakatuhakikishia kama deni hili halipo na Katibu wetu Wizara ya Elimu akataka kwenda kuhakikishia Mhe. Mwenyekiti, nina risiti hii hapa ya Umeme ambayo tulikwenda tukalipia na tukaona *Unit* zetu ni zile zile ambazo tumelipia. Kwa hivyo, naomba tu Mhe. Jaku Hashim Ayoub aamini kama suala hili limemalizika.

#### UTARATIBU

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Jukumu la kuunganisha umeme niliuliza ni gharama za skuli au gharama za wizara. Hasa ukizingatia wananchi wa Jimbo la Muyuni kutokana na hali ilivyo. Nataka kujua hapa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo wa Amali:** Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa bado naendelea kujibu sasa Mhe. Jaku sijui alikuwa na haraka ya nini kutoa utaratibu wakati sijamaliza wala sijaondoka mimi hapa.

Nilikuwa bado naendelea kujibu na nilikuwa nataka niwasilishe hii risiti ya malipo, ili iwe ni ushahidi kwa Baraza hili kama hakuna tatizo hilo tena. Naomba watendaji waje waichukuwe wakupatie Mhe. Mwenyekiti.

Lakini jukumu la kuunganisha umeme katika maskuli, hili ni la wizara na skuli yenyewe husika.

#### Nam. 58

#### Utafiti wa Mimea inayoshambulia Mimea Mingine

**Mhe. Mohammed Haji Khalid – Aliuliza :-**

Mtunda kanga (mla ngamia) ni mmea unaoshambulia sana mimea mingine ikiwemo ya mazao ya chakula kama migomba na mihogo na ya biashara kama mikarafuu.

Je, wizara imefanya utafiti gani juu ya mmea huo kuhusu madhara yake juu ya mimea mingine hasa mikarafuu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 58 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, mmea wa mtunda Kanga au Mlangamia ni mmoja kati ya aina ya mmea ya magugu yaliyoenea hapa visiwani Zanzibar. Mmea huu unauwezo kuishi peke yake au kujizonga kwenye mimea mingine au miti iliyo karibu nao.

Mlangamia si mmea ambao kuishi kwake kunategemea mmea mwengine (*parasite*) ambao ina tabia ya kufyonza chakula kwenye mmea unaozonga, bali huufunga kwa kamba zake mmea mwengine au mti na kuukamua usiweze kunenepa na hata kuufunika kabisa kama mwamvuli na kuukosesha jua ambalo ni muhimu kwa mti au mmea kwa kujitegemea chakula. Kwa kufanya hivyo mti unaozongwa na mlangamia hudhoofika na kufa taratibu na baadae hukauka.

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya taarifa hiyo hakuna utafiti wowote uliofanyika, ila madhara ya mmea huu huwa yanaonekana wazi wazi pale ambapo mashamba yetu yasipo shughulikiwa kwa kupaliliwa na kusafishwa.

Na kama magugu hayo yanaachwa katika mashamba ya mikarafuu hilo linakuwa ni pigo kwa uchumi, kwani tunafahamu kwa jinsi gani nchi yetu inavyolitegemea zao hilo.

Mhe. Mwenyekiti, njia za kukabiliana na tatizo la mmea huu ni kuhakikisha kwamba mashamba yetu yanapata usimamizi mzuri na kanuni za kilimo bora kufuatwa ipasavyo.

Wizara ya Kilimo kupitia kwa mabwana na mabibishamba wake huwa inatoa elimu kwa wakulima juu ya utunzaji bora wa mashamba, kwa kuyafanyia usafi, kuyapalilia magugu au kufyekea miti isiyohitajika ili kuondosha kabisa tatizo hili na kuhakikisha kwamba miti iliyopandwa mashambani inazaa vizuri.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo yake ya awali Mhe. Naibu Waziri alikiri kuwa wizara haijafanya utafiti wowote juu ya madhara yanayosababishwa na mmea huu hatari ambao unanyonya miti mbali mbali na kunyonya kwake kunasababishia hiyo miti mingine kufa.

- (a) Je, haoni kuwa na kwa kuwa anajua kuwa ni hatari na kwa kuwa hawajafanya utafiti haoni kuwa anachangia kupotea kwa miti ya mazao yetu ikiwemo mkafaruu na mazao mingine ya chakula.
- (b) Je mti huu si aghalabu kuota chini kama maelezo ya Mhe. Naibu Waziri yalivyo, mara nyingi huwa unazonga kule juu. Kwa hivyo, hata shamba uliweke safi bado mti ule unabakia kule juu. Kwa hivyo, hamuoni pia kwamba kuna haja ya kufanya utafiti juu ya kuutokomeza mmea huu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:**

- (a) Mhe. Mwenyekiti, mti huu haunyonyi mti ambao unazonga. Mti huu unakuwa unazonga tu lakini haunyonyi ule mti ambao uliozonga, kwa sababu kuna miti inayonya ile inayoota. Huu mti wake zizi lake linakuweco chini ambalo linalotegemea chakula. haidhuru inakuwa mzizi wake ni mgumu kuonekana lakini unakuwa mzizi wake uko juu. Kwa hiyo kama nilivyosema kuondosha mti huu ni kupalilia mashamba yetu, ukesha palilia limemalizika tatizo.
- (b) La kuona ipo haja ya kufanya utafiti, mimi nakubaliana nae kwamba ipo haja ya kufanya utafiti na katika suala hili Idara ya Utafiti basi watalifanyia utafiti kwa sababu tayari wako katika *process* za kufanya utafiti hivi karibuni tu tuliwasiliana na Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti na yeye amewasiliana na wenzetu katika sehemu ya Kilimo Bara ili kuhusu suala hili hili la kufanyia utafiti mti huu wa Mlangamia.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe maongezi yenu sasa yanasababisha watu wa *hansard* washindwe kufanya kazi zao vizuri naomba sana nidhamu iendelee kutumika katika jengo hili ili taratibu zetu ziweze kwenda vizuri.

**Mhe. Salim Abdallah Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu suala hili alisema kuwa huu Mtandakanga ni *parasite* na *parasite* ni kiumbe ambacho kinategemea maisha yake na mambo mengine kutokana na kiumbe chengine kuna *endoparasite* kuna *ectoparasite* na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, swali langu ni kuwa kwa sababu Mtandakanga ni kiumbe katika jamii ya miti na kutokana na utafiti ni kuwa asilimia zaidi ya 95 ya dawa zetu tunazotumia zinatengenezwa Mahospitali zinatokana na miti, na

kwa sababu mti huu unaleta umasikini kwa wakulima na kwa taifa kwa sababu ya kudhoofisha maisha ya miti mengine ambayo ni muhimu kwetu.

Mhe. Waziri haoni kuwa uko umuhimu wa kweli kabisa wa kuufanyia hasa utafiti wa mti huu, kuna mambo gani ambayo ni muhimu au ni yenye dhara kwetu. Na kama ni muhimu utatafutiwa mahala pa kuimarishwa kwa makusudi usiondoke na kuondolewa kule kwenye kilimo tu kuliko kuundoa moja kwa moja halafu baadae ikaja kuwa ni hasara upande wetu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nilichosema katika jibu nisema Mlangamia si mmea ambao kuishi kwake unategema mmea mwingine, sio mmea unaoishi kutegea mmea mwingine, ina maana sio *parasite* nadhani ndivyo nilivyosema.

Swali lake la kuona umuhimu wa kuufanyia utafiti wa kina jinsi ya kwamba mjiti huu una matibabu mimi nakubaliana nae ili kuufanyia utafiti wa kina mjiti huu.

**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman:** Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa ina uhaba wa mabibi mashamba na mara nyingi huelemea kwenye kilimo cha mpunga.

Je, mabibishamba wa kutoa taaluma ya kilimo cha juu kuelimisha usafi wa mashamba wanatokea wapi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tuna uhaba wa mabibimashamba lakini hata hivyo mabibishamba ambao wanatoa taaluma katika sehemu ya mpunga ndio hao hao wanaotoka taaluma katika sehemu ya mihogo.

Vile vile tunazoa *Field Farmers School*, hizi zimo katika mashehia na hawa wanaofunzwa wanatoka katika Shehia zetu na hao hao ndio wanaotoa taaluma katika sehemu ya kilimo cha juu na ukichukulia, mfano Makunduchi kunazalishwa migomba na migomba ile wanatoa taaluma hawa wananchi ambao wako katika skuli hizi. Kwa hivyo, hakuna tatizo la mabibishamba ya kutola taaluma kiasi hicho.

## Nam. 50

### Uwekaji Vioo Katika Majengo ya Mji Mkongwe

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-**

Kwa muda mrefu Mamlaka ya Uhifadhi Mji Mkongwe imekuwa ikizuia wananchi kuweka madirisha ya vioo ambayo hayana asili ya Mji Mkongwe huku wawekezaji na wafanyabiashara kama vile maduka na Ofisi ya Shirika la Magari wakishuhudiwa kuweka madirisha ya vioo kama yale wanayozuwiwa wananchi wengine na sehemu nyengine za Hoteli kuweka vioo.

- (a) Kwa vile Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 imeeleza wazi binaadamu wote wana haki sawa mbele ya sheria, kwanini sheria tunazotunga ndani ya chombo hiki wengine wanaruhusiwa kuzivunja na wengine wakitakiwa kuziheshimu.
- (b) Ni lini wizara dhamana itahakikisha inasimamia majukumu yake kwa mujibu wa sheria badala ya upendeleo jambo ambalo halileti picha nzuri kwa wananchi wake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 50 kama ifuatavyo:-

- (a) Mamlaka ya Mji Mkongwe inafanya kazi zake kwa mujibu wa Sheria za nchi hii ikiwa na dhima kubwa ya kuhifadhi na kuulinda Mji Mkongwe wa Zanzibar ili ubaki katika hadhi yake ya urithi wa asili kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo. Hivyo Mamlaka haifanyi kazi katika misingi ya ubaguzi bali inatekeleza kazi

zake katika misingi ya usawa kwa kumruhusu muomba kibali kufanya matengenezo kwa mujibu wa sheria, kanuni pamoja na taratibu za uhifadhi Mji Mkongwe.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe naomba ieleweke kwamba Jengo la *auto sale* lina madirisha ya vioo ambavyo pembeni mwake yana frame za mbaao yanakubalika, lakini vioo kama jengo la Muzzamil Mlandege havikubaliki.

- (b) Wizara siku zote ipo kwa kusimamia sheria na kulinda haki za wananchi wake.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kutokuwa na afya na hayana viwango na siwezi kuthubutu kumwambia lugha nyengine yoyote.

Mhe. Naibu Waziri uko tayari kufuatana na kufanya ziara mimi na wewe isijekuwa kama zaira ya Wizara ya Afya iliyotolewa jana akaahidi kwenye chombo hapa halafu wakaingia miti.

Uko tayari kufatana mimi na wewe kwenda kushuhudia watu wengine kuruhusiwa kufanya wengine kutokuruhusiwa kufanya shughuli hizo.

Naomba ninukuu Katiba ya Zanzibar inavyosema:-

"Kinga, Haki za lazima wajibu wa mtu binafsi, binaadamu wote huzaliwa huru na wote ni sawa kila mtu anastahili heshima na kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake watu wote ni sawa kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake, watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki ya bila ya ubaguzi wowote kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria. Hakuna sheria itakayokuwa na kifungu chochote ambacho ni cha ubaguzi"

- (a) Mhe. Mwenyekiti, haya ninayozungumza sibahatishi niambie lini uko tayari tufanye ziara ya mimi na wewe kwenda kuonesha kwa vitendo vinavyofanywa katika mamlaka hii ni ubaguzi. Ziara yako isijekuwa kama Wizara ya Afya, "kutaka kufa kuzimia waogopa" hutoa kauli hapa nikajitayarisha mimi hakuna tena kwenda Wizara ya Afya.
- (b) Serikali inazungumzia nini juu ya wafanyabiashara wanaoruhusiwa kujenga ghorofa tatu na wengine kutokuruhusiwa. Sheria za nchi hii ziko ngapi tatu, iko moja tunataka kujua.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:**

- (a) Mhe. Mwenyekiti, sikatai kabisa kufanya ziara na yeye. Kwa hivyo, mimi niko tayari tufanye ziara na twende tukaangalie hata kama tutaenda baada ya kuakhirisha Baraza hili.
- (b) Kama nilivyoeleza hapo awali wizara yangu kupitia mamlaka ya Mji Mkongwe inafanya shughuli zake kisheria. Kwa hivyo hatufanyi kazi kiubaguzi kwa kumbagua mtu, silka, sura au jinsia. Tunafanya kisheria na tutaendelea kuisimamia sheria kama Serikali ambavyo inavyoagiza kwa taasisi zote.

**Mhe. Mwenyekiti:** Naam! kuhusu utaratibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

## UTARATIBU

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri yeyote anayeulizwa swali ambalo analo madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi, kwa ufupi isipokuwa kwamba swali alililoulizwa Mhe. Waziri mmoja linaweza kujibiwa na Waziri mwingine ama Mwanasheria Mkuu.

Yupo tayari Naibu Waziri kujiuzulu pindipo nikenda kumuonesha masuala haya yanayofanyika kinyume na sheria za nchi hii. Upo tayari Mhe. Naibu Waziri au kuna sheria ngapi zinazosimamia nchi hii.

**Mhe. Mwenyekiti:**Mhe. Jaku hoja haikuwepo hapo toka mwanzo uliposema. Ulipokuwa umemtaka Mhe. Waziri endapo kama itathibitika, hilo suala kwamba kuna *double standard* katika hilo, kuna watu wanaruhusiwa, kuna watu hawaruhusiwi ulitaka ukathibitishiane wewe na Mhe. Waziri.

Sasa unasimama kuhusu utaratibu kumtaka Waziri ajiuzulu. Siyo utaratibu wa Kibunge unavyokuwa. Naomba tuheshimu utaratibu. (*Makofi*)

Kuna taratibu za kisheria zifuata. Tusiende kama tunakwenda katika maeneo ambayo siyo ya kutunga sheria. Kanuni ya 37 uliyotumia sote tunaitambua, haielekezi ambavyo wewe unafanya. Naomba tuheshimu taratibu.

Tuendeleo Mhe. Hija Hassan Hija.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, mimi ninaendelea kutoa masikitiko yangu kwamba kila mtu aliyekuwa na macho mawili yaliyokuwa mazima amekuwa akishuhudia ghorofa tatu na ghorofa nne pale maeneo ya Mji Mkongwe.

Swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub ambalo ninataka nijibiwe tena.

- 1) Hivyo Mji Mkongwe chini ya sheria hii wana sheria ngapi wanazisimamia. Ni kwa nini Mhe. Waziri utie ndani changa la macho wakati suala lipo wazi. Kuna sheria ngapi zinazosimamia Mamlaka ya Mji Mkongwe, zipo ghorofa nne na nyengine ya ghorofa ya tatu. Je, ipo sheria (a) na (b).
- 2) Tumeambiwa sisi kwenye Uislamu kwamba mtu ambaye hana la kusema bora anyamaze. Si bora ungenyamaza Mhe. Naibu Waziri.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kwanza naomba nimkumbushe Mhe. Mwakilishi swali halikuja ambalo linahusiana na masuala ya ghorofa, linakuja swali linalohusiana kuweka madirisha ya vioo na nikathibitisha suala hilo kwamba tunafanya kazi zetu kiutaratibu wa kisheria.

Sasa suala vile vile linalohusiana na ujenzi wa nyumba za ghorofa, aidha kuweka ghorofa ngapi basi vile vile nalo tunakwenda katika hali ya utaratibu wa kisheria, hatumbagui mtu kwamba huyu kwa sababu yupo pengine katika hali fulani na tukamruhusu pengine kujenga ghorofa anazozitaka yeye *no!* Isipokuwa tunachokifanya ni kwamba tunakwenda katika utaratibu wetu wa kisheria, mtu yeyote, tunaisimamia sheria yetu kwa kumruhusu mtu kujenga ghorofa kwa mujibu wa sheria na uhifadhi wa Mji Mkongwe.

## UTARATIBU

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, mimi ninafahamu swali la msingi lilivyoulizwa na maswali mengine ya nyongeza, Mhe. Jaku Hashim Ayoub amezungumza pia amegusia ujenzi wa ghorofa.

Mhe. Naibu Waziri aniambie tu, hii sheria ya Mji Mkongwe ina sehemu inaruhusu ghorofa tatu na kuna sehemu inaruhusu ghorofa mbili au kuna sehemu inaruhusu kujenga ghorofa nne.

Kama unasimamia sheria, sheria hiyo kutoka wapi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Hija Hassan Hija kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ninarudia pale pale kwamba tunachoangalia ni sheria. Aidha, mtu yeyote anayetaka kujenga jengo ndani ya Mji Mkongwe, basi tunamuelekeza utaratibu wetu wa kisheria.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kuweza kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu yake ya kuzungukazunguka Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali la kwanza.

- 1) Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa Mji wetu unaitwa *Stone Town* na hivi sasa watu wanajenga matofali badala ya ile dhana ya *Stone Town*.
- 2) Ninataka niombe ni mipaka gani kuanzia wapi hadi kufikia wapi ambayo inaonesha *area* ya Mji Mkongwe.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kwanza nitajibu swali la mwisho kuhusiana na mipaka, hili la mipaka naomba aniachie na nitamjibu kwa vizuri kabisa kwa kutumia njia ya maandishi.

- 1) Kuhusu ujenzi wa majengo ya Mji Mkongwe kwa kutumia matofali, bado suala hili haturuhusu na tunafuatilia yule yeyote ambaye anakwenda kinyume na utaratibu basi tunamchukulia hatua zinazofaa. Tunajitahidi kufuatilia na tunawaongoza wale wote ambao wanaofanya marekebisho ya majengo hayo. La kama kuna mtu kafanya kitu kama hicho kujenga au kufanya ukarabati kwa kutumia matofali, basi ninaomba Mhe. Mwakilishi tushirikiane tufuatilie pamoja tukishatatalipatia ufumbuji suala hilo.

#### UTARATIBU

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, saa nyengine tunamuona kama Mhe. Jaku Hashim Ayoub anakuwa matata, kumbe si matata kutokana na yale majibu.

Mhe. Mwenyekiti, ni katika bajeti iliyopita nilitoa mfano na niliona mtu anajenga matofali badala ya *stone* na nikaeleza sana. Leo Mhe. Naibu Waziri ananiambia na mpaka leo kwa taarifa mheshimiwa hilo tofali lenyewe limeshatiwa bati.

Sasa ananiambia tena kuwa mtu anachukuliwa sheria. Ninamuomba sana Mhe. Naibu Waziri kama Mhe. Jaku alivyosema mimi nipo tayari twende mguu kwa mguu mimi na yeye na tuchukue televisheni, ili aone halafu nione yule atoe amri avunjiwe siku tunayofika, siku ile ile.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Naibu Waziri alikwishakuli hilo. Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri.

#### TAARIFA ZA SERIKLI

##### **Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Baraza Yaliyotokana na Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya 2013/2014**

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora naomba kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji ya Maagizo ya Baraza la Wawakilisho iliyotokana na Kamati ya kudumu ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena hapa na kuja kufanya majukumu ya kuwatumia wananchi wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangalizi huo, sasa naomba Baraza lako tukufu likifuatilia waraka ambao umesambazwa kwao pamoja na mambo ambayo nitayasema lakini maelezo yaliomo katika ukurasa wa kwanza mpaka ukurasa wa tatu yaingie kwenye *hansard* ya Baraza la Wawakilishi kama ni muunganisho wa taarifa ya bango kitita ambalo litalisoma.



Mhe. Mwenyekiti, baada ya kwisha kusema hayo, sasa naomba nisome maagizo moja kwa moja ya utekelezaji wa Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora kama yalivyoagizwa na Baraza la Wawakilishi kupitia Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa 2013/2014.

Maagizo na utekelezaji wake:

### **Agizo la kwanza**

Ilikuwa kumalizwa haraka kwa utata juu ya suala la Ikulu ya Micheweni.

### **Utekelezaji**

Ofisi ya Rais na Utawala Bora, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ na Wizara ya Fedha kwa pamoja zilika na mkandarasi kwa lengo la kutatua utata uliodumu kwa muda mrefu na kuweza kuupatia ufumbuzi. Hatua inayofuata ni kufanya upya mapitio ya ramani. Kwa sasa ramani hizo zimeshachorwa upya na zinafanyiwa utaratibu wa kufanyiwa thamani (*DOQ*) kabla ya kuitisha zabuni ya kumtafuta mkandarasi atakayemaliza ujenzi wa jengo hilo.

### **Agizo la pili**

Ilikuwa ni kuharakisha upatikanaji wa hati miliki za majengo ya Ikulu kwa upande wa Pemba.

### **Utekelezaji**

Hati miliki ya majengo ya Ikulu ya Chake-Chake na Mkoani tayari zimeshapatikana.

### **Agizo la tatu**

Ilikuwa kushughulikia mmomonyoko wa ardhi uliopo upande wa nyuma ya jengo la Ikulu ya Mkoani.

### **Utekelezaji**

Andiko la mradi wa kushughulikia mmomonyoko katika nyumba ya Ikulu ndogo ya Mkoani liliandaliwa. Ushauri ulitolewa ni kwamba mradi huo ujumuishwe katika mradi wa uimarishaji wa nyumba za viongozi na nyumba za Serikali, mradi ambao unasimamiwa na Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora.

### **Agizo la nne**

Ilikuwa ni kusimamia ujenzi wa fensi katika Ikulu ndogo ya Mkokotoni.

### **Utekelezaji**

Ofisi yangu imeanza kushughulikia ujenzi wa ukuta wa nyumba ya Mkokotoni ambapo iliundwa kamati ya pamoja iliyojumuisha uongozi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, kuangalia eneo hilo kama linafaa kutumika kama Ikulu. Kamati hiyo imeshawasilisha ripoti yake na kwa sasa inafanyiwa kazi kabla ya hatua nyengine kuchukuliwa.

### **Agizo la tano**

Ilikuwa ni kuandaa mradi utakaoweza kushughulikia ukarabati pamoja na mmomonyoko wa ardhi uliopo eneo la Ikulu ndogo Bwefum ambao unasababishwa na maji ya chumvi.

### **Utekelezaji**

Andiko la mradi wa kushughulikia mmomonyoko katika nyumba ya Ikulu ndogo ya Bwefum iliandaliwa. Ushauri ulitolewa ni kwamba mradi huo ujumuishwe katika mradi wa uimarishaji wa nyumba za viongozi na nyumba za Serikali, mradi ambao unasimamiwa na Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora.

### **Agizo la sita**

Ilikuwa ni kukamilisha *scheme of service* ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

### **Utekelezaji**

*Scheme of service* ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekamili kwa mujibu wa miundo ya utumishi. *Scheme* hiyo tayari inatumika na wafanyakazi wa Ofisi hii walianza kufaidika nayo tokeo mwezi wa Novemba, 2014.

### **Agizo la saba**

Ilikuwa ni kuangaliwa upya sheria inayompa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili taarifa zake ziwekuwa ni sehemu ya ushahidi.

### **Utekelezaji**

Serikali inalifanyia kwa kupata ushauri zaidi wa kisheria ili kuondoa utata wakati wa matumizi ya sheria hiyo. Na sheria nyengine zinazohusiana na kutoa ushahidi Mahakamani. Sasa maoni yanayotolewa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*Audit opinion*) kwa mujibu wa sheria hayachukuliwi kama ushahidi kamili bali husaidia katika kupatikana ushahidi.

### **Agizo la nane**

Ilikuwa ni Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwashauri Bodi ya Mapato ya Zanzibar kuachana na tabia kukusanya mapato ya Serikali kwa njia ya kawaida (kwa maana ya mkononi).

### **Utekelezaji**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameziarifu taasisi zinazokushanya kodi ikiwemo Bodi ya Mapato ya Zanzibar kuacha utaratibu huo. Ushauri huo tayari umeanza kufanyiwa kazi na taasisi husika.

### **Agizo la tisa**

Ilikuwa kupatiwa usafiri Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuiwa Rushwa na Uhujumu Uchumi ili aweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi.

### **Utekelezaji**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa msaada kutoka Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) imeipatia mamlaka gari moja ambayo kwa sasa inatumiwa na Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hii ili aweze kutekeleze majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Sambamba na hilo, Serikali pia imeipatia mamlaka gari ya pili kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za mamlaka za kila siku. Vile vile Serikali karibuni itaipatia mamlaka gari nyengine kwa ajili ya ofisi yake mpya iliopo Chake-Chake Pemba.

### **Agizo la kumi**

Ilikuwa ni kusimamia na kutekeleza suala la ulinzi katika eneo la Ofisi ya Mamlaka ya Kuzuiwa Rushwa na Uhujumu wa Uchumi.

### **Utekelezaji**

Ofisi za Mamlaka ya Kuzuiwa Rushwa na Uhujumu wa Uchumi zimepatiwali ulinzi na zinalindwa masaa ishirini nne, wakati wa mchana watumishi wa mamlaka walioajiriwa kwa kazi hiyo ya ulinzi ndiyo wanaolinda na kwa wakati usiku walinzi kutoka Kikosi cha Valantia hufanya kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo niliyosema lakini yapo mambo ambayo yameshauriwa na Baraza yatajumuishwa kwenye mpango wa bajeti ya Serikali.

### **Hitimisho**

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii kutoa maelezo ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Na kwa mara nyengine ninapenda kuishukuru kamati hii kwa ushauri na miongozo inayoipa ofisi yangu mara kwa mara.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri. Sasa tunamkaribisha Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Mheshimiwa Kaimu karibu kwa mara nyengine tena. (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais):** Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kuja kuwasilisha utekelezaji wa maagizo ya Baraza la Wawakilishi kupitia Kamati hii ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo kwamba katika kabrasha ambalo tumeligawa kuanzia ukurasa wa kwanza linaloanzia na suala la utangulizi mpaka ukurasa wa kumi na moja, maelezo hayo yaingizwe kwenye *hansard* za Baraza la Wawakilishi ikiwa ni sehemu ya ripoti hii ya utekelezaji wa maagizo ya ofisi hii.

Sasa baada ya kwisha kusema hayo, kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yake.

### **Agizo la kwanza**

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ilitakiwa ichukuwe hatua za kufunga *CCTV camera* katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ajili ya kuimarisha usalama.

### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, ofisi imeanza maandalizi ya utekelezaji wa mpango huu, maandalizi hayo ni pamoja na kuwasiliana na baadhi ya kampuni ili kuweza kupata gharama za kufunga mtambo huo. Mtambo huo unatarajiwa kufungwa katika mwaka wa fedha 2015/2016. Aidha, ofisi imeimarisha masuala ya usalama kwa jumla, kwa kuweka utaratibu unaoeleweka wa wageni kuingia kwa shughuli mbali mbali pamoja na kuongeza ulinzi katika maeneo yote ya ofisi.

### **Agizo la pili**

Agizo la pili lilikuwa serikali kuu iangalie suala la ujenzi wa nyumba za viongozi wa kuu wa kitaifa hasa kisiwani Pemba, kwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais. Aidha, suala la usafiri nalo lipatiwe ufumbuzi kwani gari nyingi za wizara huazimwa kwa ajili ya kuwahudumia viongozi hao pamoja misafara yao.

### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, agizo hili nililitolea ufafanuzi katika taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2012/2013 na maelezo yalikuwa kama yafuatavyo.

"Serikali kupitia Wizara ya Fedha, imeandaa mpango maalum wa ujenzi wa makazi ya viongozi wakuu wa kitaifa kwa Unguja na Pemba. Mpango huo unatekelezwa kwa awamu kulingana na uwezo wa serikali kifedha.

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, tayari imeandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya viongozi hao". Mwisho wa kunukuu.

Kwa upande wa Makamu wa Pili wa Rais Ofisi imeshachukua hatua ya kulishughulikia suala hili, kwa kuandaa mradi wa ujenzi wa nyumba za makazi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Kisiwani Pemba na Dar es Salaam. Mradi huo utaombewa fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016, na utekelezaji utanza baada ya maombi hayo kukubaliwa na Tume ya Mipango.

Kwa upande wa usafiri tayari gari mbili kwa kuanzia kwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais zimeshapelekwa Pemba na kuanza kutumika.

### **Agizo la tatu**

Kwa upande wa Zanzibar Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ijenge jengo jengine la kisasa litakalokuwa na huduma zote na eneo lenye faragha sio pale lilipo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, agizo limepokelewa na linaendelea kufanyiwa kazi kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali zinazohusika.

### **Agizo la nne**

Serikali ihakikishe utekelezaji wa taarifa za Kamati za Kudumu na Teule, zinafanyiwa kazi ili kupunguza kero katika jamii na kupelekea wananchi kutokuwa na imani na serikali yao, kwani maelezo yanayotolewa Barazani mengi huwa yanatokana na wananchi wenyewe.

### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuliarifu Baraza kuwa mapendekezo ya Kamati za Kudumu na Kamati Teule za Baraza la Wawakilishi, yamekuwa yakifanyiwa kazi na serikali kwa ukamilifu na taarifa zake huwa zinawasilishwa katika Baraza la Wawakilishi.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa, inaendeshwa kwa uwazi na misingi ya sheria na haitamvumilia mtu yeyote atakayehusika na ubadhirifu wa mali ya umma. Zipo kesi zinazoendelea mahakamani kuhusiana na wanaotuhumiwa kufanya ubadhirifu na hatua za kiutawala zimechukuliwa na serikali kila pale unapopatikana ushahidi kwa mujibu wa taratibu ziliopo.

Hatua zilizochukuliwa hivi karibuni katika Baraza la Manispaa Zanzibar, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na ushahidi tosha wa kuwa serikali inayafanyia kazi mapendekezo ya Kamati za Baraza, tunaombwa sote tushirikiane na serikali pamoja na vyombo vyake vya ulinzi na usalama katika kukomesha vitendo vya ubadhirifu wa mali ya umma.

### **Agizo la tano**

Kamati imeona kuwa kuna malalamiko na migogoro mingi ya ardhi, hivyo kuna umuhimu mkubwa wa waratibu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kulifuatilia kwa karibu na kushauri na kumshauri ipasavyo Makamu wa Pili wa Rais na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa lengo la kuipatia ufumbuzi migogoro hii.

### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yeye mwenyewe huwa anafuatilia sana masuala ya ardhi na mara kwa mara huwa anakemea masuala ya migogoro ya ardhi, kwa kupitia hotuba zake za kuahirisha Baraza la Wawakilishi pamoja na mazungumzo yake na wawekezaji juu ya tofauti zao na wananchi. Ukweli ni kuwa anachukizwa sana na suala hili.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, huwa inaratibu na kufuatilia migogoro ya ardhi inayowasilishwa na wananchi na kutafutia ufumbuzi wake kwa kushirikiana na sekta husika. Serikali inawataka wananchi wote pamoja na wawekezaji kufuata sheria na taratibu zilizowekwa za umiliki na matumizi bora ya ardhi.

Viongozi wa Serikali za Mikoa, Wilaya na Shehia wawajibike ipasavyo katika kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya ardhi, inayojitokeza katika maeneo kama alivyoagiza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohammed Shein kwa viongozi hao.

Aidha, hivi sasa mkazo maalum umewekwa kwa mahakama za ardhi kusimamia migogoro ya ardhi kupitia sheria zilizowekwa. Hivyo, masuala yanayohusu migogoro ya ardhi yatasimamiwa moja kwa moja na mahakama hizo kwa mujibu wa taratibu ziliopo ili migogoro hiyo ipate ufumbuzi wa kisheria.

### **Agizo la sita**

Ili kutekeleza vyema suala zima la utawala bora na kuzifanya taasisi tatu za nchi kwa maana ya mahakama, chombo cha kutunga sheria na serikali, kutekeleza kazi zao bila kuingiliana na ni vyema mahakama ya ardhi ikawekwa chini ya Mahakama Kuu, badala ya utaratibu wa sasa ambapo mahakama hiyo huwa chini ya wizara inayoshughulikia utoaji wa uhaulishaji wa ardhi. Hii ni kutokana na malalamiko yaliopo ya ucheleweshaji wa kesi unaosababishwa na watendaji wa wizara husika.

### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, Mahakama ya Ardhi imeanzishwa kwa mujibu wa sheria namba 7 ya mwaka 1994, kama ilivyorekebisha na sheria namba 1 ya mwaka 2008, ikiwa na jukumu la kusikiliza migogoro inayohusiana na mambo ya ardhi. Uwezo na majukumu ya mahakama hiyo umeelezwa ndani ya sheria husika. Mahakama hiyo iko chini ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na ndio wenye dhamana ya kuiendesha. Hata hivyo, Mwenyekiti na Mahakimu wote wanaofanyakazi katika mahakama hiyo ni waajiriwa wa Mahakama Kuu.

Mwenyekiti wa Mahakama hiyo anateuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kushauriana na Mhe. Jaji Mkuu wa Zanzibar, kwa mujibu wa kifungu namba 4(4)(1) cha sheria iliyoanzisha mahakama hiyo. Mahakimu wengine wote wa Mahakama ya Ardhi Unguja na Pemba, huteuliwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama, kwa kuzingatia sifa zilizowekwa na sheria.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo serikali imelipokea agizo hili na itaifanyia kazi kutokana na mapendekezo yaliyotolewa.

### **Agizo la saba**

Serikali ipatie idara ya sherehe na maadhibisho ya kitaifa vitendea kazi vya kutosha, ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, serikali inanunua vifaa vya sherehe kila mwaka kulingana na mahitaji ya uwezo wa kibajeti. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, serikali ilinunua vifaa mbali mbali vya sherehe ikiwemo mashamiana, zulia, bendera na vitambaa. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 serikali imepanga kununua viti, zulia jekundu na kufanyia matengenezo mashamiana ya zamani.

### **Agizo la nane**

Kamati inaiomba serikali pale zinapotokea kazi na sherehe za kitaifa, kuhakikisha kuwa stahiki za watendaji wa idara hizi zinalipwa kwa wakati.

## **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, serikali huwa inalipa stahiki kwa watendaji wote wa sherehe na kwa wakati, pale wanapotekeleza majukumu ya ziada wakati wa sherehe za kitaifa. Aidha, ushauri tunaupokea na pale inapotokea kasoro za aina hiyo huwa tunachukua hatua za kuzirekebisha.

## **Agizo la tisa**

Serikali katika suala la uhifadhi wa kumbukumbu za viongozi wa kitaifa, ihakikishe kuwa kunakuwa na nyumba maalum ya makumbusho kwa ajili hiyo, ili uhifadhi uwe mzuri na endelevu kwa faida ya vizazi vijavyo na historia ya nchi hii.

## **Utekelezaji**

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imewasilisha serikalini wazo, yaani *concept note* la kujenga nyumba maalum ya kumbukumbu ya Rais wa kwanza wa Zanzibar na Mwenyekiti wa kwanza wa Baraza la Mapinduzi, Marehemu Sheikh Abeid Aman Karume. Hivyo, ujenzi huo utanza mara tu mradi huo utakapokubaliwa na Tume ya Mipango na kupatiwa fedha.

Sambamba na hilo serikali pia inakusudia kutenga eneo maalum katika mnara wa kumbukumbu ya miaka 50 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar hapo Michenzani, kwa ajili ya kumbukumbu za viongozi wa Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12/01/1964.

## **Agizo la 10**

Kamati inaishauri serikali kupitia idara ya maafa, kuipatia idara vifaa vya kutosha na vya kisasa ili iweze kukabiliana na maafa pindi yanapotokea. Kamati pia katika hili inashauri serikali kusaidia na kushirikiana na wawekezaji binafsi. Mfano, mwekezaji kwenye sekta ya ufundishaji wa kurusha ndege, kwani ana vifaa na ndege ambazo zinaweza kutua hata juu ya bahari. Hili kwa mazingira ya nchi linaweza kutusaidia na faida itapatikana kwa pande zote mbili.

## **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inaendelea kushirikiana na taasisi pamoja na wawekezaji mbali mbali, ili kuona kwamba suala la kujenga uwezo wa nchi juu ya kujikinga na kukabiliana na maafa linafanikiwa. Katika mwaka huu wa fedha, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inategemea kupata vifaa mbali mbali vya kukabiliana na maafa, kutoka *UNICEF* katika kuimarisha maghala ya kukabiliana na maafa. Kwa upande mwingine Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tayari imeandaa andiko la mradi wa kujenga uwezo wa kukabiliana na maafa baharini, angani na nchi kavu na kuwasilisha serikalini kwa utekelezaji.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeiandikia mamlaka ya viwanja vya ndege kutaka ushauri juu ya suala hilo.

## **Agizo la 11**

Kamati iliishauri serikali kuwa taarifa za ajali au maafa zitolewe kwa haraka kwa lengo la kuwasilisha uokozi na kupunguza athari za maafa.

## **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, serikali imechukua ushauri huu na kuufanyia kazi kwa kuweka maafisa viungo wa maafa katika taasisi mbali mbali za serikali, pamoja na wilaya zote za Unguja na Pemba. Leo la hatua hii ni pamoja na kurahisisha mawasiliano na upatikanaji wa haraka wa taarifa za maafa na kuharakisha masuala ya uokozi.

Aidha, hivi karibuni serikali imeanzisha sheria mpya ya kukabiliana na maafa na mambo mengine yanayohusiana na hayo, pamoja na mkakati wa mawasiliano wakati wa maafa ili kukabiliana na maafa.

## **Agizo la 12**

Kamati inaishauri serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kuharakisha kuwasilisha Barazani mswada wa marekebisha ya sheria ya maafa, ili kuleta ufanisi wa utekelezaji wa sheria hiyo, kwa lengo la kuondoa vikwazo vinavyokwamisha utekelezaji mzuri wa kazi za idara.

Mhe. Mwenyekiti, mswada wa sheria mpya wa kukabiliana na maafa umewasilishwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi, na sasa anasubiriwa Mhe. Rais kusaini na kufanya kazi kwa sheria mpya ya kukabiliana na maafa.

## **Agizo la 13**

Kamati vile vile ilishauri serikali kutekeleza sheria hiyo, kwa kuanzishwa kwa vitendo mfuko wa maafa ulioanzishwa katika sheria hiyo. Kuwepo kwa mfuko huo kutaiwezesha idara kuondokana na utaratibu wa sasa wa kutegemea fedha za matumizi ya kawaida, yaani *OC* peke yake ambazo kiukweli hazitoshelezi kwa asilimia kubwa katika utekelezaji wa mfuko huo.

## **Utekelezaji**

Katika sheria mpya ya maafa, mfuko wa kukabiliana na maafa umewekewa utaratibu mzuri wa utekelezaji wake, ambapo utaanza mara tu baada ya Mhe. Waziri kuitangaza sheria hiyo katika gazeti rasmi la serikali.

## **Agizo la 14**

Kamati pia iliishauri serikali kuijengea Idara ya Maafa jengo la kisasa na kuipatia vitendea kazi, ili kuharakisha utoaji wa huduma pale maafa yanapotokea.

## **Utekelezaji**

Katika hatua za kuhakikisha idara hii ina jengo lake la kudumu, serikali imeipatia Idara ya Maafa kiwanja huko katika eneo la Tunguu, ambapo kwa sasa ofisi inamalizia kazi za kuandaa michoro ya jengo hilo na hatua itakayofuata ni ofisi kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo.

## **Agizo la 15**

Kamati inashauri suala la elimu ya maafa lipewe kipaumbele kuanzia ngazi ya awali ya Shehia na hadi maofisini, ili wananchi waelewe jinsi ya kukabiliana na maafa pale yanapotokea.

## **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Kukabiliana na Maafa inafanya jitihada kubwa za kutoa elimu kwa kupitia njia mbali mbali, njia hizo ni pamoja na kupitia kipindi maalum kinachorushwa kupitia ZBC redio kila siku ya Jumatatu, kutoa elimu ya maafa kwa makundi mbali mbali ya watu wenye ulemavu, waandishi wa habari, wanafunzi wa skuli za msingi, sekondari na vyuo vikuu, watendaji wa sekta mbali mbali za serikali na binafsi na kadhalika.

Hata hivyo, idara itaendelea na jitihada zake za kutoa elimu, kwa kuyalenga makundi mbali mbali ambayo yamo katika hatari za kukumbwa na kuathiriwa na majanga, pamoja na mafunzo katika ngazi za shehia.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa kushirikiana na wahusika wengine wote wa maafa nchini, imeandaa mkakati wa mawasiliano kwa wakati wa maafa tangu mwaka 2012. Mkakati huo umewasilishwa kwa wadau, kwa wahusika wengine kwa ajili ya matumizi.

Aidha, jumla ya majaribio mawili ya mezani ya kukabiliana na maafa, yaani *table top simulation exercise*, yamefanyika katika kufanyia majaribio mkakati huo, ili uweze kutumika kwa mafanikio, pindipo maafa yakitokea na hivi karibuni kulikuwa na kongamano kubwa linalohusu kupima uwezo wetu wa kukabiliana na maafa na namna ya kujikinga, kukabili na kurudisha hali ya kawaida baada ya maafa kutokea.

## **Agizo la 16**

Kamati ilikumbushia kusaidiwa katika masomo na mafunzo kwa watoto ambao walioondokewa wazee wao katika ajali ya *MV. Spice Islander* lishughulikiwe ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, serikali iliwapatia fedha zilizotolewa kwa wahusika wote ambapo walielezwa kuwa fedha hizo zisaidie katika kuwasomesha watoto hao. Serikali pia inaendelea kuwapatia huduma baadhi ya watoto hao na wengine katika vituo vya kulelea watoto yatima kwa kushirikiana na wahusika wengine. Aidha, wahusika na jamaa wa wahusika wa maafa hayo wanahaki ya kuomba fidia kupitia taratibu za kisheria kama ilivyopendekeza ripoti ya Tume iliyoundwa na Mheshimiwa Rais kuchunguza ajali hiyo.

## **Agizo Nam. 17**

Kamati imeiagiza Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kukifanya Kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kuwa Wakala wa Serikali ili kiweze kujiendesha wenyewe.

### **Utekelezaji:**

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imelipokea agizo hili na tayari linafanyiwa kazi. Ofisi tayari imeandaa Waraka unaopendekeza Kiwanda cha Mpigachapa Mkuu wa Serikali kuwa Wakala wa Serikali ili kiweze kujiendesha wenyewe. Hatua nyengine zitafuatwa baada ya Waraka huo kuwasilishwa Serikalini na Serikali kutoa maamuzi na muongozo.

## **Agizo Nam. 18**

Kamati inaagiza juu ya umuhimu wa kuhifadhi na kuzitunza vizuri Nyaraka za Serikali kwa faida ya nchi. Kamati pia inatilia mkazo kuwa nyaraka zilizoachwa katika kiwanda cha zamani cha Saateni zihamishiwe Maruhubi kwa faida ya Serikali na jamii kwa ujumla. Sote tunaelewa umuhimu wa nyaraka si kwa sasa tu bali hata kwa siku za usoni. Utaratibu wa sasa kuziacha nyaraka Saateni na kuhamia Maruhubi si sahihi hata kidogo bali lazima nyaraka hizo zichukuliwe vizuri ama kama zitabakia Saateni basi pia zihifadhiwe vizuri na ulinzi pia wa nyaraka hizo uwepo tena wa kutosha.

### **Utekelezaji:**

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba wakati kiwanda cha Upigaji chapa kinahamishwa kutoka Saateni kwenda Maruhubi, baadhi ya nyaraka zilibakia Saateni hii ilitokana na kwa wakati ule ofisi iliweka kipaumbele uhamishaji wa Mashine na baadhi ya vifaa vyengine, hata hivyo utaratibu mzuri umeandaliwa wa kuzihamisha nyaraka zote zilizopo Saateni kuzipeleka Maruhubi na kazi hiyo tayari imeanza.

## **Agizo Nam. 19**

Kamati imeagiza kuwa suala la itikadi za kidini linalopelekea uvunjifu wa amani lisimamiwe ipasavyo na kuchukuliwa hatua za kisheria kwa yeyote atakaesababisha machafuko.

### **Utekelezaji:**

Mhe. Mwenyekiti, agizo limepokelewa na linafanyiwa kazi kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kwa mashirikiano makubwa na viongozi na taasisi za kidini.

## **Agizo Nam. 20**

Kamati imeagiza suala la tindi kali (*Acid*) lifanyiwe jitihada za makusudi kwa kudhibitiwa ipasavyo ili lisije likasababisha athari za mipasuko za kidini.

### **Utekelezaji**



Mhe. Mwenyekiti, kupitia vyombo vya ulinzi na usalama Serikali ilifanya operesheni maalum kwa waingizaji na wauzaji wa tindi kali ili kuwatambua na kutambua matumizi yake halisi. Tokea kufanyika kwa operesheni hiyo matumizi mabaya ya tindi kali yamepungua kwa kiasi kikubwa na kiasi fulani imewaondolewa wananchi wasiwasi na khofu. hata hivyo kuna mkakati maalumu wa vyombo vya ulinzi na usalama kukomesha vitendo hivyo.

#### **Agizo Nam. 21**

Kamati pia imeagiza kuangaliwa upya na kwa uzito unaostahiki suala la *Escort* la viongozi wakuu wa kitaifa kwa upande wa Zanzibar kwa vile ziko katika hali mbaya ili kuepusha athari na maafa yasiyotegemewa kwa viongozi wetu pamoja na nchi kwa ujumla.

#### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, Serikali tayari imelishughulikia suala hili na kwa sasa *Escort* mbili zimepatikana na zinatumika katika misafara ya viongozi wakuu wa kitaifa. Hata hivyo, juhudi zinaendelea ili kupata nyengine zaidi.

#### **Agizo Nam. 22**

Kwa upande wa bodaboda Kamati inashauri kutungwe sheria ambayo itaweza kudhibiti utumiaji wa vyombo hivyo pamoja na umiliki wake kwa ajili ya kupunguza ajali na uhalifu ambao unafanywa na watumiaji wa bodaboda.

#### **Utekelezaji:**

Mhe. Mwenyekiti, ushauri umepokelewa na unafanyiwa kazi kwa kushirikiana na taasisi husika ili masuala ya bodaboda yapate ufumbuzi muwafaka na kufuta utaratibu unaoeleweka.

#### **Agizo Nam. 23**

Kamati imeagiza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wataalamu wake kuwa tayari kwenda kujifunza nchi zenye uzoefu juu ya mambo mablimbali yanayohusu ufuatiliaji wa mafuta na gesi asilia.

#### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, agizo hili limeanza kutekelezwa na hadi hivi sasa ziara za mafunzo kwa wataalamu wa Serikali katika fani ya mafuta na gesi zimefanyika kwa nchi za Uholanzi, Ras el Kheimah na Norway nchi ambazo zina uzoefu mkubwa katika masuala ya mafuta na gesi. Katika ziara hizo watendaji wetu wamepata fursa ya kujifunza mambo mbalimbali kutokana na uzoefu wa nchi hizo.

Aidha, Serikali kupitia Wizara husika imechukuwa hatua za kusomesha vijana katika sekta hii na hadi kufikia 2014 takwimu zilizopo zinaonesha kuwa vijana 30 wamepatiwa mikopo na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu kwa masomo ya Fani ya Mafuta na Gesi Asilia.

#### **Agizo Nam. 24**

Kamati imeagiza kuendelea kwa ushirikiano uliopo kati ya JKU na JKT ili kusaidia maendeleo na kupiga hatua kwa JKU Zanzibar.

#### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, ushirikiano baina ya JKU na JKT ni mzuri na unazidi kuimarika siku hadi siku. Kwa kupitia JKT wapiganaji wa JKU wanapatiwa nafasi za mafunzo mbalimbali yakiwemo ya kilimo na ufugaji, malezi bora ya vijana na mafunzo ya amali. Aidha, Kamati maalum inayofanya kazi ya kuratibu mashirikiano baina ya taasisi hizi mbili imeundwa na inakutana kila baada ya muda. Pamoja na hayo wana JKU wanapatiwa mafunzo ya uongozi wa ngazi mbali mbali kupitia JKT.

#### **Agizo Nam. 25**

Kamati pia imeagiza kusaidiwa vijana wa JKU katika suala zima la elimu ya uzalishaji mali ili nao waweze kufikia lengo la kupunguza umasikini na kuongeza kipato.

### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, vijana wanaojiunga na JKU wanaendelea kupatiwa mafunzo ya uzalishaji mali katika sekta za Kilimo na Ufugaji, pamoja na mafunzo hayo vijana hao hupatiwa mafunzo ya Ufundi katika fani za Umeme, Uchongaji, Ufundi bomba, Ujenzi, Ushoni, Ufundi mafriji, Ufundi magari na uchongaji vyuma ili waweze kujajiri wenyewe na kujitegemea. Aidha, katika kuwaendeleza vijana JKU imeanzisha utoaji wa elimu ya sekondari ambapo uendelezaji huo unaenda sambamba na uimarishaji wa majengo ya Skuli ya Ufundi na Sekondari yaliyopo Mtoni.

### **Agizo Nam. 26**

Kamati imeagiza vikosi vya ulinzi wa vikosi vya SMZ kuanzisha kampuni za ulinzi ambazo zitakua zinatoa huduma za ulinzi binafsi kwa mashirika, kampuni na hata mahoteli ambapo Zanzibar utalii ndio pato la nchi.

### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, huduma hizo zinatolewa ingawa kwa sasa sio katika kiwango kikubwa. Hata hivyo katika kutilia mkazo suala la usalama katika mahoteli ya kitalii, hivi karibuni tulipitisha sheria katika baraza hili tukufu kuhusu kuanzisha wakala wa ulinzi chini ya Jeshi la Kujenga Uchumi JKU. Wakala huo utawezeshwa kivifaa na nyenzo za kisasa ili uweze kuimarisha ulinzi katika maeneo yote ya utalii Unguja na Pemba.

### **Agizo Nam. 27**

Kamati imeagiza jengo la Baraza la Wawakilishi Pemba lifanyiwe marekebisho makubwa ili vikao vya Baraza viweze kufanyika Pemba, kinyume na hivyo kwa hali ilivyo sasa vikao haviwezi kufanyika Pemba.

### **Utelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, Ukumbi wa Mikutano katika Ofisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba, unahitaji matengenezo makubwa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba jengo hilo ni la zamani na sio rahisi kukamilika matengenezo yake kwa muda mfupi kwa kutegemea fedha za matumizi mengineyo (OC) zinazopatikana kupitia bajeti ya Serikali. Hivyo, Ofisi imeona kuwa matengenezo hayo yafanywe kupitia Mradi wa Maendeleo, Ofisi imeanza maandalizi ya Mradi huo.

### **Agizo Nam. 28**

Kamati pia imeagiza suala la maji katika nyumba ya Mhe. Spika, litafutiwe ufumbuzi kwa haraka kwani bila ya maji nyumba haikaliki.

### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, Kwa vile tatizo kubwa ambalo limeikabili nyumba hiyo ni upatikanaji wa maji na hadi sasa juhudi za kuchimba kisima ili kupata maji hayo hazikufanikiwa. Ofisi imechukua hatua ya kuiomba Mamlaka ya Maji iweze kuipatia nyumba hio majikupitia Mradi wa Maji unaoendelea hapo Mnara wa Mbao, ombi ambalo limekubaliwa na hatua za awali za kazi hiyo zimeanza. Hata hivyo, wakati tunasubiri mradi huo, ofisi kwa kushauriana na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi imeandaa utaratibu wa kununua maji kwa muda hadi hapo mradi huo utakapo kamilika.

### **Agizo Nam. 29**

Kamati inaishauri Ofisi ya Baraza kuwa na maandalizi yakutosha kuhusu Bunge la Katiba kwa kuwapatia Wajumbe Rasimu ya pili pamoja na elimu juu ya Rasimu hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi ilichukua hatua zote muhimu zinazohusu ushiriki wa Wajumbe kwenye Bunge Maalumu la Katiba na waliweza kushiriki kwa ufanisi. Bunge Maalum limemalizika na kwa ujumla wake hakukuwa na tatizo lililojitokeza linalohusu maandalizi na kiutawala kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

### **Agizo Nam. 30**

Kamati iliagiza elimu juu ya uendeshaji wa miradi hasa ya *TASAF III* itolewe kwani ni nyenzo muhimu sana ili kufanya miradi hiyo kuwa yenye tija na endelevu na mwishowe kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kuondosha umasikini nchini.

#### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali imetoa elimu kwa makundi mbalimbali kuhusu Mradi wa *TASAF III* kabla ya kutekelezwa kwa mradi huo. Aidha, hatua ya kutoa elimu itaendelea kwa makundi mbalimbali ikiwemo jamii na viongozi na katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa mradi huo. Kwani utaratibu huo wa kutoa elimu hasa kwa jamii utawezesha kuyafikia malengo ya Mradi wa *TASAF* ya kusadia juhudi za Serikali katika kupunguza umasikini.

### **Agizo Nam. 31**

Kamati imeliagiza Jeshi la Polisi kutoa agizo kwamba vituo vya polisi isiwe sehemu ya Mahakama bali iwe ni njia ya kuelekea Mahakamani na hili ni zaidi katika kesi za udhalilishaji.

#### **Utekelezaji:**

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ilichukua hatua ya kuviarifu Vituo vya Polisi kuwa Sehemu ya Mahakama ni kinyume na Sheria na ili kuepukana na tabia hiyo mbaya mikakati kadhaa imeandaliwa ili kuona masuala ya udhalilishaji yanapelelezw haraka na kufikishwa Mahakamani. Miongoni mwa mikakati hiyo ni:

- Kuanzishwa na kuimarishwa kwa vituo vya mkono kwa mkono (*One Stop Centre*), mahospitalini na madawati ya jinsia na watoto katika vituo mbalimbali vya polisi.
- Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, watendaji wa madawati ya jinsia na watoto hupatiwa mafunzo maalumu ya jinsi ya kushughulikia mashauri yanayohusiana na udhalilishaji.
- Ushughulikiaji wa umakini wa mashauri yanayohusiana na udhalilishaji kuwa ni ajenda ya kudumu katika Mabaraza ya Askari katika ngazi ya kituo hadi Mkoa.
- Kwa kupitia programu za Polisi Jamii, kutoa elimu kwa wananchi juu ya athari za kushawishika kuyamaliza nje ya Mahakama mashauri yanayohusiana na udhalilishaji.
- Kuchukua hatua muafaka za kinidhamu kwa Askari wanaodhamiria kudhoofisha ukusanyaji wa ushahidi kwa malengo ya kutaka kuzimaliza vituoni kesi za udhalilishaji.

### **Agizo Nam. 32**

Kamati imeagiza suala la makaazi ya polisi liwekewe mpango maalum wa kukabiliana na tatizo hilo, lakini pia Kamati imeona kuwa wakati umefika sasa wa kujenga makao makuu mapya ya Jeshi la Polisi kwa Zanzibar yanayoendana na hadhi na wakati wa sasa.

#### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, kwa kufahamu umuhimu wa kuwa na makaazi bora kwa askari sambamba na kukabiliana na changamoto inayolikabili Jeshi la Polisi na idadi kubwa ya watendaji wake kuishi nje ya kambi, mikakati ya ujenzi

wa nyumba za ghorofa kupitia *programme* ya Maboresho ya Jeshi ya Polisi Tanzania imeandaliwa na inatekelezwa kwa awamu kama ifuatavyo:

- Kwa upande wa Zanzibar awamu ya kwanza imehusisha ujenzi wa nyumba za ghorofa mbili katika kambi za polisi Ziwani Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na Limbani Mkoa wa Kaskazini Pemba.
- Katika awamu ya pili, zinatarajiwa kujengwa nyumba za ghorofa tatu zenye *units* tatu katika kambi ya Polisi Ziwani Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkoa wa Kaskazini Unguja. Mazungumzo na wadhamini wa ujenzi huo yanaendelea kufanyika.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na jitihada hizo, nyumba za zamani zinaendelea kufanyiwa matengenezo katika kambi zote za Polisi Unguja na Pemba kulingana na upatikanaji wa mgao wa fedha kutoka Serikalini kila mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kujengwa kwa jengo jipya la Makao Makuu Zanzibar, Jeshi la Polisi limeona kuwepo kwa umuhimu huo kwani jengo la sasa limejengwa miaka mingi iliyopita kiasi kwamba halikidhi mahitaji ya sasa. Hivyo, ni azma ya Jeshi la Polisi kujenga jengo jipya la Makao Makuu Zanzibar. Hata hivyo, kukamilika kwa jengo hilo kutategemea sana na upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini.

### **Agizo Nam. 33**

Kamati imeagiza kuzingatiwa suala la ujenzi wa kituo cha Polisi katika uwanja wa ndege mpya kwani ni muhimu sana kwa usalama wa nchi na watu wake.

### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha kazi za ulinzi na usalama wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, imeonekana kuwepo haja ya kuongezwa kwa idadi ya Askari wa Jeshi la Polisi, jambo ambalo lithitaji uwepo wa kituo kikubwa ndani ya eneo hilo. Katika utekelezaji wa suala hili mazungumzo kupitia vikao vya pande mbili husika (Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Jeshi la Polisi) yamefanyika na hatua iliyofikiwa hivi sasa ni kuainisha mahala pakujengwa kituo hicho na mchango wa kila taasisi katika ujenzi huo. Ni imani yetu kwamba ndani ya muda mfupi ujao ujenzi wa kituo utaanza.

### **Agizo Nam. 34**

Kamati imeshauri Tume ya Uchaguzi kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria za nchi ili kuepusha vitendo vya uvunjifu wa amani hasa katika vipindi vya uandikishaji na uchaguzi wenyewe.

### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inaendelea kufanya kazi kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na sheria ya uchaguzi pamoja na sheria nyengine zinazohusiana na masuala ya uchaguzi. Hivi sasa Tume ipo katika utaratibu wa kupendekeza marekebisho ya sheria mbili kuu ambazo zinahusiana moja kwa moja na masuala ya uchaguzi, sheria hizo ni Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya 1984 na Sheria ya Tume ya Uchaguzi ya mwaka 1992, marekebisho hayo yataweka misingi bora katika kuhakikisha demokrasia na uchaguzi huru na wa haki unafanyika.

### **Agizo Nam. 35**

Kamati inapenda kuishauri Tume ya Uchaguzi kuanza kutoa elimu ya uraia kwa wananchi na kujua haki zao na mipaka yao kwa mujibu wa sheria. Elimu hii zaidi juu ya masuala yanayohusu mambo ya uchaguzi.

### **Utekelezaji**

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la kutoa elimu ya uraia haliko moja kwa moja kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Tume ya Uchaguzi kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi imepewa jukumu la kutoa na kuratibu elimu ya kupiga kura. Na hivi sasa Tume ya Uchaguzi imekamilisha maandalizi ya Uchaguzi Mkuu, ikiwemo suala la utoaji wa elimu ya wapiga kura ambalo ni sehemu ya maandalizi hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la elimu ya wapiga kura Tume ya Uchaguzi imeanza kutayarisha misingi ya utoaji wa elimu hiyo katika kutekeleza suala hilo imeanzisha Kamati Maalum ya kuishauri juu ya utoaji wa elimu ya wapiga kura, Kamati hiyo inaundwa na Asasi za Kiraia pamoja na Taasisi za Serikali ambazo zina nafasi ya kushiriki katika utoaji wa elimu ya wapiga kura.

Kamati hiyo ina majukumu ya kuandaa mtaala wa elimu ya wapiga kura kuandaa vielelezo vyote vya elimu ya wapiga kura. Kwa sasa Kamati imemaliza kuandaa mtaala na imeanza kutayarisha vielelezo mbali mbali vya kutoa elimu hiyo ya wapiga kura. Tume inatarajia kuanza kutoa elimu ya wapiga kura mapema iwezekanavyo, ili kuweka misingi bora ya uwezo na elimu itakayosaidia wapiga kura kuelewa umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi na kupiga kura.

Mhe. Mwenyekiti, Tume pia ya uchaguzi imejipanga kutoa elimu ya wapiga kura katika kipindi cha kura ya maoni na kipindi cha uchaguzi Mkuu. Elimu hii imepangwa kutolewa kwa upana wakati, ili kuhakikisha kuwa kila mpiga kura anapata elimu hiyo.

### **Agizo Nam. 36**

Kamati iliishauri Serikali kusisitiza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kulishughulikia Suala la *Echo* katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi pamoja na jengo zima la Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyoeleza katika Mkutano uliopita kwamba tumeendelea kulifatilia kutafuta wataalamu mbali mbali ili waweze kuondoa kabisa tatizo la *echo* kwenye ukumbi wa mkutano wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri tuliupata kutoka kwa wataalamu hao wa ndani na nje ya nchi ni kwamba ili tatizo hili liondoke linahitaji ukarabati mkubwa wa miundombinu ya ukumbi wenye gharama za kuondoa tatizo hilo zilizotolewa na Kampuni ya *CITCC* ni *US\$* laki mbili ishirini na tano elfu, mia tano na sabini na tano na senti hamsini na tano (*US\$ 225,575.55*) na Kampuni ya *Zanzibar Tread and Investment* ya Zanzibar na Tanzania shilingi milioni mia mbili sabini na nne, sitini na tisa elfu na mia mbili (Sh. 274,069,200).

Mhe. Mwenyekiti, katika kufanikisha jambo hilo baada ya Ofisi kupata ushauri pamoja na makisio ya awali na ili iweze kutangaza zabuni kwa ajili ya kazi hiyo, katika mwezi huo huo wa Novemba 2014, Ofisi iliwasilisha maombi ya mradi maalum kwa madhumuni hayo Serikalini, mradi ambao utagharimu jumla ya Tanzania shilingi mia nne, thalathini na tisa milioni, laki tano thamanini tisa, laki tisa arubaini na sita elfu kwa mchanganuo ufuatao.

Ununuzi wa vifaa ni jumla ya fedha za Tanzania milioni mia mbili, tisini na tano elfu, mia nne thamanini na tatu, laki tatu atubaini na saba elfu. Gharama nyenginezo *labour cost* ni Tanzania Shilingi milioni mia moja, arubaini na nne, laki moja, mia tatu tisini na nane elfu. Hizo ndio *costs* za kumaliza tatizo la *echo* katika mradi huo.

Hitimisho, Mhe. Mwenyekiti, napenda kuihakikishia Kamati ya Baraza lako kwa ujumla kwamba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wakati wowote ipo tayari kupokea ushauri, maagizo na maelekezo na kuyafanyia kazi ili kuleta ufanisi na utendaji wenye tija.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kukushukuru tena wewe binafsi na Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu na ni imani yangu kwamba Wajumbe wamefatilia kwa makini maelezo niliyoyatoa ambayo yamefafanua utekelezaji wa maagizo ya Kamati na Baraza kwa jumla yaliyotolewa katika ripoti ya Kamati ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante, kaimu waziri, sasa tunamkaribisha Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kuwa wazima na kutupa nguvu za kuweza kushiriki kikao hichi muhimu kwa manufaa ya Zanzibar na wananchi wake.

Naomba pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maelezo ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuhusu utekelezaji wa maagizo na ushauri tulioupokea kutoka kwa Kamati ya Kudumu ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukurani maalum na za kipekee kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mhe. Hamza Hassan Juma, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa michango, ushauri, maelekezo, miongozo na maagizo, waliyoitoa na wanayoitoa kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Hakika ushauri na miongozo yao imekuwa ni chachu ya mafanikio yaliyopatikana ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, pia, napenda kuwashukuru wajumbe wenzangu wote wa Baraza lako hili tukufu kwa ushirikiano wao wa dhati kwangu mimi binafsi pamoja na watendaji wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo kwa heshima, naomba nitoe maelezo ya utekelezaji wa maagizo na ushauri uliotolewa na Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa Fedha 2013/2014.

#### **Agizo la Kwanza**

Kamati inamtaka Waziri anayeshughulikia Masuala ya Ardhi kutoa maelezo ya kina na ufafanuzi ndani ya Baraza hili juu ya mmiliki halali wa eneo linatarajiwa kujengwa kituo cha kubadilisha tabia, yaani *rehabilitation centre* huko Tunguu.

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imewasiliana na Wizara inayohusika na masuala ya ardhi juu ya eneo lililokuwepo Tunguu. Serikali imeamua kuhamishia eneo la ujenzi wa kituo hicho kutoka Tunguu kwenda Kidimni kutokana na mazingira ya eneo ambalo ni kubwa zaidi kuweza kukidhi haja ya ujenzi unaokudiwa na kuwa mbali na mji.

Serikali kupitia Idara ya Mazingira kuhakikisha kuwa miradi yote ya Serikali na ya watu binafsi inafanyiwa tathmini ya kimazingira kabla ya kuanza kwake, ikiwemo miradi ya ujenzi wa barabara, hoteli na miradi mengine mikubwa.

#### **Utekelezaji**

Mahusiano na mashirikiano kati ya Idara ya Mazingira na Tume ya Mipango *ZIPA*, Kamisheni ya Utalii, Idara ya Misituta na Maliasili zisizorejeshika, Idara ya Barabara, Idara ya Mipango Miji na Vijiji na Idara ya Ardhi na Wilaya juu ya tathmini ya athari za kimazingira yameimarishwa.

Sharti la kufanya tathmini ya kimazingira kwa miradi inayohusika kuingizwa kwenye masharti yanayokuwemo kwenye vyeti vya muda wanavyopewa wawekezaji. Aidha, mafunzo ya tathmini ya athari za kimazingira kwa baadhi ya watendaji wa taasisi hizo na nyengine yamefanyika. Jumla ya miradi 17 kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 imefanyiwa tathmini ya athari za kimazingira idadi hiyo inategemea kuongezeka kwa kipindi cha mwaka 2014/2015.

Aidha, Sheria Mpya ya Mazingira ya mwaka 2015 imezingatia kazi muhimu zilizokuwemo kwenye sheria hiyo ikiwa ni pamoja na kasoro zinazoambatana na tathmini za athari za kimazingira.

#### **Agizo la Tatu**

Kamati inaitaka Idara ya Mazingira ishirikiane na Bodi ya Viwango Zanzibar ili bidhaa zinazoingizwa ziwe kwenye viwango vizuri vya matumizi na kiafya kwa wananchi.

Idara ya Mazingira imewasilisha shauri hili kwa Bodi ya Chakula na Dawa, Idara ya Biashara na Bodi ya Viwango Zanzibar ili kulisimamia suala hili kwa kuwa shauri hili linalihusu taasisi hizo. Bodi ya Chakula na Dawa ilikuwa ikifanya juhudi kubwa za ufatiliaji ili kuhakikisha kuwa bidhaa zilizopitwa na muda haziuzwi madukani. Katika ufatiliaji huo taasisi hiyo hivi karibuni imefanikiwa kukamata jumla ya tani thalathini ya nyama ya mbuzi, tani 70 za unga wa ngani na tani thalathini za tende. Bidhaa zote hizo zilikuwa hazifai kwa matumizi ya binaadamu na zimeangamizwa kwa mashirikiano na wadau mbali mbali ikiwemo pamoja na Idara ya mazingira.

### **Agizo la Nne**

Sheria ya Mazingira iharakishwe kuletwa Barazani ili mianya yote ya uharibifu wa mazingira iweze kuzibwa.

### **Utekelezaji**

Naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kupitisha Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2015. Sheria hiyo imepitishwa katika kikao kilichopita cha Baraza la Wawakilishi. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaamini kuwa mapungufu na mianya ya uharibifu wa mazingira yameweza kuzingatiwa vyema katika sheria hiyo.

### **Agizo la Tano**

Suala la usafiri wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba, Kamati inatoa agizo la kutatuliwa tatizo hili haraka iwezekanavyo.

### **Utekelezaji**

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Raisi bado inaendelea na ufatiliaji wa suala hili ili kulipatia ufumbuzi wake kwa kupatikana fedha za ununuzi wa gari hilo.

### **Agizo la Sita**

Kamati inaagiza kuwepo utaratibu maalum wa kushughulikia bidhaa chakavu zinazolingizwa nchini ikiwa ni pamoja na kuzingatia ubora wake na inapotokea kuziangamiza basi wataalamu husika washirikishwe ipasavyo.

### **Utekelezaji:**

Kamati maalum ya wadau ya kutayarisha muungozi wa kuingiza bidhaa chakavu imetayarishwa na Bodi ya Viwango Zanzibar. Kamati hiyo imekutana mara kadhaa na kutayarisha rasimu ya mwanzo ya muungozi huo. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, hivi sasa inakamilisha utafiti wa kujua kiwango na mfumo wa uingizwaji wa bidhaa chakavu za umeme na *electronic*. Taarifa za utafiti huo zinategemea kusaidia katika kukamisha muungozi wa bidhaa chakavu za umeme na *electronic*.

### **Agizo la Saba**

Kamati inatoa agizo kwa *ZIPA* kuacha tabia ya kuweka mbele maslahi yao binafsi bali waweke maslahi ya nchi kwanza na kuwajibika katika kutekeleza na kusimamia sheria ipasavyo. Hii inatokana na ukweli kwamba baadhi ya wawekezaji hupewa vibali hata kabla ya kufanya tathmini ya kimazingira, jambo ambalo ni kinyume na sheria.

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeliwasilisha agizo hilo kwa taasisi husika za *ZIPA* kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

### **Agizo la Nane**

Kamati inaagiza kufanywa kwa utafiti utakaowajumuisha wataakamu wa Serikali kukaa na kuangalia kitaalamu zaidi juu ya matumizi sahihi ya eneo la Kisauni ambalo lilikuwa likichimbwa kifusi kwa faida ya nchi na watu wake.

## **Ukelezaji**

Shimo hilo limo ndani ya miliki ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar. Mamlaka hiyo hivi sasa imo kwenye hatua za kuangalia matumizi sahihi ya eneo hilo. Wadau mbali mbali watashirikishwa katika kupitia mpango wa matumizi ya eneo hilo kabla ya kutekelezwa.

## **Agizo la Tisa**

Kamati inaiagiza Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kushirikiana kikamilifu na Idara ya Mazingira katika shughuli zao kwa maslahi ya umma.

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, imeliwasilisha agizo hilo kwa taasisi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa ajili ya utekelezaji wa pamoja na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka wa Fedha 2013/2014. Ni matarajio yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe, wamepitia bango kitita la utekelezaji huo na kwa heshima sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

## **HOJA ZA KAMATI**

### **Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Mwaka 2014/2015**

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Serikali):** Mhe. Mwenyekiti, muhtasari wa ripoti ya Kamati ya Kudumu ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa Fedha 2014/2015.

## **SEHEMU YA KWANZA**

### **Utangulizi**

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi imeundwa kwa mujibu wa Kifungu cha Kanuni 10(6) (h) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2012 kwa mujibu wake yametajwa katika kifungu cha 114 kama ifuatavyo:

Kufatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia, kufatilia utekezaji wa sera na mipango ya Wizara husika na kadiri Mhe. Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowakilishwa Barazani wakati wa usomaji wa bajeti au hotuba nyengine za waziri alizitoa Barazani:

- Kufatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kitaita na miradi ya wananchi ya wizara husika,
- Kuchunguza na kufatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha,
- Kuchambua mapengekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka,
- Kushughulikia Miswada na Sheria kutokabidhiwa kwa Spika,
- Kuchambua hali ahadi zote za Wizara zilizochini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufatilia utekelezaji wa ahadi hizo, na
- Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 ilianza shughuli zake za kufatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati, ahadi za Serikali kazi za kawaida na za maendeleo.

Ukusanyaji wa mapato na matumizi pamoja na kufanya ziara katika taasisi za Serikali za wizara zifuatazo:

Ofisi ya Nchi, Ikulu na Utawala Bora,



Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, na  
Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Aidha, Kamati Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki nne katika mizunguko miwili kama ifuatavyo:

Pemba wiki moja kuanzia tarehe 8 hadi tarehe 12 Disemba, 2014 na Unguja wiki moja kuanzia tarehe 15 hadi tarehe 19 Disemba, 2014. Pemba wili moja kuanzia tarehe 2 hadi 6 Februari, 2015 na Unguja wiki moja kuanzia tarehe 9 hadi tarehe 13, Februari, 2015.

Kikawaida Kamati za Baraza la Wawakilishi zinafanya kazi kwa mwaka kwa mizinguko minne ila kutokana na mchakato mzima wa Bunge la Katiba iliokuwa ukiendelea huko Dodoma ambapo Baraza nalo lililazimika kushiriki katika kazi hiyo kwa mujibu wa Sheria ya Marekebisha ya Katiba. Toleo la mwaka 2012 limepelekea Kamati za Baraza kukosa kufanya kazi kikawaida na kupelekea Kamati kufanya kazi kikawaida na kupelekea Kamati kufanya kazi katika mizunguko miwili kwa bajeti ya mwaka 2014/2015.

Napenda kuchukua nafasi hii adhimu kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa mashirikiano yao ambayo yameweza kufanya kazi zetu kwa ufanisi mkubwa wajumbe wenyewe ni kama wafuatao:

1. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti
2. Mhe. Saleh Nassor Juma - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Mzee Ali - Mjumbe
4. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Mjumbe
5. Mhe. Subeit Khamis Faki - Mjumbe
6. Mhe. Ashura Sharif Ali - Mjumbe
7. Mhe. Shadya Moh'd Suleiman - Mjumbe
8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni - Katibu
9. Ndg. Makame Salim Ali - Katibu

Kamati ilifanya kazi zake kwa kutumia Kanuni za Baraza la Wawakilishi, *Hansard* za Baraza, Hotuba za Bajeti za Taasisi za Wizara za Serikali za mwaka 2014/2015 pamoja na taarifa za taasisi husika za Serikali.

## SEHEMU YA PILI

### OFISI YA RAIS, IKULU NA UTAWALA BORA:

Ofisi hii imeundwa na Idara na Taasisi zifuatazo:-

1. Ofisi ya Faragha
2. Ofisi ya Baraza la Mapinduzi
3. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
4. Idara ya Mawasiliano - Ikulu
5. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
6. Ofisi ya Usalama wa Serikali (GSO)
7. Ofisi ya Ofisa Mdamini - Pemba
8. Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje
9. Idara ya Utawala Bora
10. Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi
11. Ofisi ya Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
12. Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Kisekta na Kupunguza Umasikini
13. Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi
14. Idara ya Ukuzaji Uchumi
15. Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

### OFISI YA OFISA MDHAMINI - PEMBA:

Kamati inaridhishwa na utendaji kazi unaofanywa na Ofisi hii kupitia idara zilizo chini yake.

Pamoja na ufanisi mzuri wa kazi Kamati pia imebaini changamoto kadhaa zinazoikabili Ofisi hii ikiwemo usafiri hasa katika Idara ya Utawala Bora na Ofisi ya Mdhubiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ambapo hupelekea kupunguza ufanisi katika utekelezaji wa kazi zake, ufinyu wa bajeti pamoja na uingizwaji mdogo wa OC ambapo hupelekea kukwamisha malengo ya Ofisi waliyojiwekea, ukosefu wa jengo la Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora Pemba. Hii ni changamoto iliyopo kwa muda mrefu sasa hali ambayo inapelekea kuwakata tamaa watendaji wa Ofisi ambapo wanafanya kazi katika mazingira magumu.

Aidha, pia kuna changamoto ya ukosefu wa Ofisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Pemba, kukosekana kwa taaluma juu ya mambo ya kisheria kwa wananchi hasa wa vijijini pamoja na uelewa mdogo wa jamii juu ya haki za binaadamu hasa kwa wanawake na watoto.

Mwisho, kwa upande wa changamoto ni kukosekana kwa mwanasheria katika Ofisi ya CAG Pemba hali ambayo ni changamoto kwao kwa vile hadi sasa wanategemea mwanasheria aliyeko ofisi ya CAG Unguja.

Kamati inashauri Serikali kuziangalia vizuri na kuzitafutia ufumbuzi changamoto zote zilizotajwa hapo juu na kutekeleza maoni na ushauri wa Kamati kama yalivyoelezwa kwa urefu kwenye ripoti ya Kamati.

#### **IDARA YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA URATIBU WA WAZANZIBARI WANAOSHISHI NCHI ZA NJE (DIASPORA):**

Idara imeendelea kuratibu ushiriki wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi katika Jumuiya za Kitaifa, Mashirika ya Kimataifa na nchi nyengine katika kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Mbali na kuratibu kazi zao idara inakabiliwa na changamoto kuu ya ufinyu wa bajeti katika kutekeleza majukumu yake.

Kamati inashauri kuwa idara ipatiwe fedha ili kuweza kuwafuata na kukutana na jumuiya za Wazanzibari wanaoishi nje kwa lengo la kuwatambua na kujua elimu zao, elimu na ujuzi wao ili kuweza kuwatumia pale wanapohitajika katika Serikali kwenye shughuli za maendeleo.

#### **IDARA YA UTAWALA BORA:**

Kamati katika utekelezaji wa kazi zake ilikutana na idara na kupatiwa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha 2014/2015, pamoja na taarifa iliyopatiwa Kamati iligundua kuwa bado Idara inakabiliwa na changamoto zinazofanana na taasisi nyingi za Serikali ikiwemo ufinyu wa bajeti na ukosefu wa usafiri.

Kamati inashauri ushauri yote yaliyotolewa kwenye ripoti hii kama ilivyo ifanyiwe kazi na Serikali ili kuleta ufanisi kwenye dhana nzima na Idara ya Utawala bora kiujumla.

#### **MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHJUMU UCHUMI:**

Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ni taasisi iliyoundwa kwa lengo la kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi. Kamati inaona bado kuna kazi kubwa ya kufanywa na Mamlaka kwani tatizo la rushwa ni kubwa kuliko mamlaka inavyochukua hatua. Hivyo bado jitihada ni ndogo na zinahitaji kuongezwa hasa kwenye suala la kufuatilia masuala ya uhujumu uchumi.

Aidha, Kamati inaitaka mamlaka kuzitumia ipasavyo ripoti za Kamati Teule za Baraza la Wawakilishi ili kuweza kuwachukulia hatua wale wote waliohusika.

#### **OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI:**

Ofisi inaendelea kutekeleza kazi zake kwa mujibu wa sheria katika ukaguzi wa hesabu katika Wizara na Mashirika. Kamati inaitaka Afisi ya CAG kupita Waziri husika kuleta ripoti husika ya mishahara hewa ambapo Baraza la Wawakilishi liliagiza uchunguzi ufanywe ili kuona upotevu wa fedha za Umma.

Aidha, Kamati inaiagiza Afisi ya CAG kutoa ripoti kuhusu fedha zilizokusanywa na Kampuni ya *Filtex* ya Dubai ambayo ilikuwa ni wakala wa shirika la meli.

## OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS:

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inatekeleza majukumu yake kupitia taasisi zifuatazo:-

- a) Ofisi ya Faragha
- b) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
- c) Idara ya Uendeshaji na Utumishi
- d) Idara ya Mazingira
- e) Idara ya Watu Wenye Ulemavu
- f) Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Pemba
- g) Tume ya Uratibu na Udhhibiti wa Dawa za Kulevya, na
- h) Tume ya Ukimwi

Kamati ilifuatilia Utekelezaji wa Bajeti, Miradi, Sera na Ukusanyaji wa Mapato katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Unguja na kubaini changamoto mbali mbali zikiwemo hizi zifuatazo:-

1. Wananchi bado wanavuna mali asili zisizorejesheka bila ya kufuata Sheria na Utaratibu wa Kimazingira.
2. Hakuna Utaratibu wa Ufuatiliaji wa athari za Kimazingira kabla ya kuanza Utekelezaji wa Miradi mbalimbali hasa mikubwa kwa hapa nchini. Hata ile miradi ambayo taratibu zilifuatwa basi kunakuwa na ukiukwaji wa makusudi wa maagizo na ushauri unaotolewa na Idara ya Mazingira kwa taasisi husika.  
  
Aidha, Kamati pia imebaini ukiukwaji wa Sheria ya Maadili kwa baadhi ya viongozi wa Serikali kuingilia utendaji wa baadhi ya taasisi hasa Idara ya Mazingira katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku hasa katika matumizi mabaya ya fukwe kwa ujenzi usiofuata masharti ya mazingira.
3. Uingizwaji, usafirishwaji na utumiaji wa dawa za kulevya bado upo na unaendelea kwa kasi nchini na kuendelea kuiathiri jamii.
4. Mabadiliko ya Tabia nchi yanaendelea kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii huku idadi kubwa ya jamii hawafahamu athari zake, ama hawana elimu ya kutosha juu ya athari za mabadiliko hayo kwa maendeleo yao binafsi na nchi kwa ujumla.
5. Udhalilishaji hasa kwa watu wenye ulemavu bado unaendelea katika jamii licha ya juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na watu binafsi pamoja na Serikali.
6. Kuhusu suala la ujenzi wa *Rehabilitation centre*, suala hili limekuwa ni la muda mrefu jambo ambalo linawakosesha vijana wanaoacha kutumia madawa ya kulevya kupata pahala pa kurejesha hali na afya zao. Ijapokuwa ucheleweshwaji huo unatokana na ufinyu wa bajeti, lakini Serikali lazima ioneshe nia ya dhati kabisa katika kufanikisha suala hili.

Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuanzisha ujenzi wa Kituo cha Kurekebisha Tabia (*Rehabilitation Centre*) huko Kidimni.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS:

1. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutenga fungu kubwa zaidi katika bajeti ya kila mwaka kwa kuweza kusaidia mapambano ya maambukizi mapya dhidi ya gonjwa hili hatari la Ukimwi na hili litafanikiwa tu pale itakapoweza kuendelea kutolewa elimu kwa wananchi kila itapobidi.
2. Kamati pia inaishauri Tume ya Ukimwi kutumia vyema fedha zote zinazotolewa ikiwa na Serikali ama zile za wafadhili kwa madhumuni ya kufikia lengo lililokusudiwa la kuwasaidia watu wanaoishi na virusi vya ukimwi pamoja na kutoa elimu kwa umma na si vyenginevyo.
3. Kamati inashauri kuangaliwa kwa kina suala la ajira kwa watu wenye ulemavu kwani wapo baadhi yao wana uwezo mzuri wa kufanya kazi.

4. Pamoja na yote hayo lakini Kamati pia inaishauri Serikali kuangalia kwa ukaribu zaidi shughuli za Idara ya Watu Wenye Ulemavu kwa kuwaongezea bajeti au angalau kile wanachokasimiwa waweze kukipata kwa asilimia mia (100%) ili waweze kutekeleza majukumu yao.
5. Baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, 2015, Kamati inashauri kuharakishwa mchakato wa kuundwa kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA) ili lile lengo la kupambana kwa dhati na suala la uharibifu wa mazingira liweze kushughulikiwa ipasavyo.
6. Kamati pia imebaini udhaifu mkubwa kwa upande wa ZIPA katika kutekeleza na kusimamia sheria ipasavyo, hii ni kutokana na ukweli kwamba baadhi ya wawekezaji hupewa vibali hata kabla ya kufanyiwa tathmini ya kimazingira jambo ambalo ni kinyume na sheria. Hivyo, Kamati inatoa wito tabia hii iachwe mara moja kwa maslahi ya nchi na kuwataka waweke mbele maslahi ya nchi kuliko maslahi yao binafsi, kwani janga lolote litakapotokea watakoathirika ni Wazanzibari na sio wawekezaji. Tunalizungumza hili zaidi kwenye miradi ya mahoteli na miradi mingine mikubwa ya uwekezaji.

Suala hili si mara ya kwanza Kamati yetu kulizungumza, lakini Kamati kila inapopata muda wa kupitia miradi hiyo ya maendeleo bado inakuta tatizo hili lipo, kwa hivyo, Kamati inamtaka Mwenyekiti wa Tume ya Maadili kuanza kushughulikia ukiukwaji huu wa madaraka kwani kama kusema tumeshasema sana.

7. Kamati aidha inaishauri Serikali kuhusu suala la uingiaji wa maji chumvi katika maeneo zaidi ya 150 kote nchini kufanyiwa utafiti wa kina, haraka na wa dharura ili kuweza kukabiliana na tatizo husika.

Kamati katika suala hili inasisitiza maeneo mahsusi ya kuangaliwa mwanzo kwani hali yake ni mbaya zaidi ikiwemo Bonde la Kitondooni Mkoani, eneo la Chuo cha Mafunzo Kengeja, Kisiwa Panza, Kangani na Mtambwe Mkuu.

8. Kutokana na ugumu na ukubwa wa kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya unaotokana zaidi na ukubwa wa mtandao wenyewe. Hivyo, Kamati yangu inashauri kuwe na ushirikiano wa pamoja na kuundwe kikosi maalum kuanzia ngazi ya shehia ili kuwabaini wale wote wanaojihusisha na biashara ama matumizi ya dawa hizi za kulevya.

#### **OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS:**

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inaundwa na Ofisi pamoja na Idara zifuatazo:-

1. Ofisi ya Faragha
2. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
3. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
4. Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali
5. Idara ya Maafa
6. Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa
7. Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali
8. Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar-es-salaam
9. Baraza la Wawakilishi
10. Tume ya Uchaguzi
11. Ofisi Kuu Pemba.

#### **OFISI YA FARAGHA**

Ofisi ya Faragha inaendelea na majukumu yake ya msingi ya kutoa huduma zinazostahiki kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

#### **MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuchukua hatua za kufunga *CCTV camera* katika Ofisi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa lengo la kuimarisha usalama.
2. Kamati yangu inaiomba Serikali Kuu kuliangalia suala la ujenzi wa nyumba za Viongozi wetu wakuu wa Kitaifa hasa kule Pemba, kwani Kamati hairidhishwi na jinsi wanavyoshughulikiwa wakiwepo Kisiwa cha Pemba, hasa Makamu wa Kwanza na Makamu wa Pili wa Rais. Aidha, hawana usafiri wa kutosha kwa Kisiwa cha Pemba jambo ambalo hulazimika ziara zao kusitisha shughuli nyingi za kikazi wakati wanapokuwepo Pemba kwani magari mengi ya mawizara huazimwa kwa ajili ya kuwahudumia viongozi hao pamoja na misafara yao.

Isitoshe, kwa vile sasa tunakaribia kumaliza muhula wa kwanza wa awamu ya saba, Kamati inaipa changamoto Serikali kujitathmini na kufanya hesabu ingekuwa imeweza kuokoa kiasi gani cha fedha kama angalau tungekuwa tumeweza kupata hata nyumba moja kwa mmoja kati ya Mhe. Makamu wa Kwanza au Makamu wa Pili wa Rais kwa kule Pemba.

Ni masikitiko ya Kamati inayosimamia Ofisi hizi kuona bado hadi leo tunakodi nyumba kwa ajili ya Viongozi wetu wanapokuwa Pemba.

Ni imani ya Kamati yangu kwamba Serikali Kuu italichukua suala hili na kulitafutia ufumbuzi utakaomridhisha kila mmoja wetu.

3. Vile vile, Kamati inaishauri Serikali kujenga jengo jengine Dodoma ambalo litaendana na hadhi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, lakini pia na Dar-es - Salaam kujengwa jengo la nyumba ya Mhe. Makamu wa Kwanza na wa Pili ili waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi zaidi.
4. Kamati yangu pia inashauri kwa upande wa Zanzibar kuhamisha ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kujengwa jengo jengine la kisasa litakalokuwa na huduma zote na eneo lenye faragha. Sio pale lilipo hivi sasa.
5. Kuhusiana na suala la Usafiri, Kamati bado hairidhishwi na hali za gari zinazotumiwa kwenye misafara ya Viongozi wetu, ukiacha gari anayopanda Mhe. Makamu wa Pili basi zilizobakia zote hali yake si nzuri na zinahitaji kubadilishwa ili kuwapa unafuu walenzi wetu kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

## **IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI**

### **MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

Kamati inaridhishwa kwa kiasi juu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali unavyofanywa hivi sasa, lakini inashauri mambo yafuatayo yazingatiwe ili kuimarisha uratibu huo na kufikia dhamira na malengo pamoja na mategemeo ya wananchi kwa nchi yao.

1. Serikali ihakikishe utekelezaji wa taarifa za Kamati za Kudumu na Kamati Teule za Baraza zinafanyiwa kazi ili kupunguza kero katika jamii na kupelekea wananchi kuwa na imani na Serikali yao kwani maelezo yanayotolewa Barazani mengi huwa yanatoka kwa wananchi na utekelezwaji wa maagizo hayo ndio kuwatumikia wao.

Vile vile, kuna ubadhirifu mwingi uliogundulika na Kamati zilizoundwa na Baraza la Wawakilishi lakini hakuna hatua za haraka kuchukuliwa, hii itapelekea wale wakosaji kujihisi wao wako sawa na wengine kuweza kufanya kama hivyo. Kwani watahisi kufanya ubadhirifu ni jambo la kawaida tu. Hivyo, hata malengo ya Serikali itakuwa ni ndoto tu ikiwa tutaendelea kuoneana muhali huku wachache wakiitafuna nchi. Kamati inaamini ikiwa Serikali itakuwa makini basi bado kuna uwezo mkubwa wa kujitegemea kwa bajeti ya matumizi ya kawaida kupitia mapato yetu ya ndani bila kutegemea wafadhili kutoka nje.

Aidha, kwa kuwa sasa tumeshatunga Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, wakati umefika sasa wa Tume baada ya kuanza kazi zake rasmi kuanza na Ripoti za Kamati Teule za Baraza ili kurejesha imani ya wananchi

kwa Serikali yao. Tukiangalia Sera ya Utawala Bora (2011) ambayo Serikali ndiyo inayoismamia inaeleza wazi kuwa;

"Utawala Bora ni utumiaji wa madaraka kwa ufanisi, uaminifu, usawa, uwazi na uwajibikaji katika ngazi tofauti za Serikali". Ukurasa wa 3.

Hivyo, Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ihakikishe kuwa inasimamia utekelezaji wa Sera hiyo kwani wao ni kiungo muhimu cha kufanikisha shughuli za Serikali na hivyo kutimizwa kwa matarajio ya wananchi kwa Serikali yao.

Kwa maelezo zaidi naomba Wajumbe waangalie ripoti ya Kamati.

## **IDARA YA MAAFA**

Kamati inaipongeza Idara hii ya Maafa kwa kujitahidi kutekeleza majukumu kwa kadiri ya hali inavyoruhusu.

Aidha, kutokana na kukamilika kwa Sheria ya Kukabaliana na Maafa Zanzibar, 2015 na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi, ni matumaini ya wananchi kwamba zile kasoro zote za kiutendaji na nyengine za kitaalamu zitakuwa zimepatiwa mwarobaini ili kuweza kukabiliana vyema na maafa pale yanapotokea.

Kwa maoni na ushauri wa Kamati kuhusiana na Idara ya Maafa naomba Wajumbe pia wafanye rejea kwenye ripoti ya Kamati.

## **IDARA YA SHEREHE NA MAADHIMISHO YA KITAIFA**

Kamati inatoa pongezi za dhiti kabisa kwa Mhe Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Makamu wa Pili wa Rais kwa kuadhimisha na kufanikisha Sherehe za Miaka 51 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, Kamati inatoa shukrani za dhiti kwa Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa chini ya Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Maandalizi na Uratibu wa Sherehe za Miaka 51 ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kazi nzuri aliyoifanya...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, kwa vile muda wetu umebakia mchache sana na ripoti yako imebakia kidogo kumalizika, tumuombe basi Mwanasheria Mkuu ili atuongeze muda kidogo umalizie.

## **UTARATIBU**

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, uko makini sana katika kusukuma mbele shughuli za Baraza, lakini naomba ukumbuke kwamba leo ni siku ya Ijumaa, ni siku ya ibada kiasi ambacho wengine misikiti yetu iko mbali sana. Kwa hivyo, kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu sana, nakuomba usimtaka Mwanasheria Mkuu kutengua Kanuni badala yake uliaharishe Baraza hili hadi saa 11.00 kamili za jioni leo, naamini Wajumbe wengi watafika kusudi Mhe. Shadya, ambaye yuko kwa niaba ya Mwenyekiti wangu hapo wa Kamati hii kusimamia viongozi wakuu aje amalizie hotuba yake.

Kwa heshima kubwa naomba tufanye hivyo ili tuwahi ibada kwa sababu wengine iko Unguja *dahil* katika sehemu za Fuoni huko na Mwera.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, nafikiri dakika zenyewe hazizidi tano nitakazozidisha. Naomba tukubaliane ili amalize tukija jioni kwa ajili ya kuchangia.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, naomba tutenge kando Kanuni ya 23 ya muda ili tuweze kumruhusu Mwenyekiti wa Kamati amalize hotuba yake ya uwasilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):**

Aidha, Kamati inapenda kuchukua nafasi hii adhimu kuishauri Serikali juu ya kumtangaza Marehemu Mzee Abeid Aman Karume; Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Jemedari wa Mapinduzi tunayokula matunda yake kuwa Baba wa Taifa la Zanzibar.

Ni kawaida na utamaduni wa kila mtu kuthamini chake na mwenyewe Mzee Karume aliwahi kusema; "Tukuza chako mpaka usahau cha mwenzako". Ni imani na matumaini ya Kamati yetu kwamba itaona busara na umuhimu wa kulifanya hili kulinda heshima na historia ya muasisi huyu wa Mapinduzi ya nchi yetu.

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

Baraza la Wawakilishi ndiyo ngome ya wananchi kama Mhe. Aboud Jumbe, alivyowahi kusema. Kamati inaridhishwa na utendaji wa kazi za Ofisi wa majukumu yake ya kila siku.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati pia inaendelea kushauri na kusisitiza kuwa taratibu zote za lazima zifanywe ili Mhe. Spika aweze kuhamia katika nyumba iliyojengwa maalum kwa ajili yake. Kamati inaona kuendelea kukaa tu kwa nyumba ile bila ya kutumiwa ni kupoteza gharama kubwa zilizokwisha tumika ambapo Baraza letu ndilo linalotakiwa liwe mfano wa kutumia vizuri kodi za wananchi. Kuendelea kukaa tu kwa nyumba ile bila ya kutumika ni jambo ambalo haliridhishi wala halipendezi mbele ya macho ya wananchi.
2. Kuhusu Ofisi za Baraza Pemba Kamati inaomba kufanyiwa ukarabati zaidi pamoja na kuwepo huduma zote ili iweze kutumika. Aidha, Kamati inatoa pongezi kwa matengenezo makubwa yaliyofanywa hadi sasa, lakini pia kuna kazi kubwa ya kufanywa mpaka Ukumbi wa Baraza uweze kufanya kazi zake zilizokusudiwa.

Hali ya ukumbi wa mikutano ya Baraza bado ni ile ile isiyoridhisha, vikalio ni vile vile vya mabenchi ambayo kiumri yamechoka na kukosa hadhi ya kukaliwa na Wajumbe kwa shughuli za vikao vya Baraza.

Halikadhalika ukumbi wenyewe unahitaji matengenezo makubwa ili uoane na hadhi ya kumbi za mikutano ya mabunge. Kiujumla ukumbi unahitaji matengenezo makubwa ili uweze kutumika tena kwa shughuli za Baraza.

Dawa ya kutibu ugonjwa huu wa saratani ya ubovu wa majengo ni kuingiziwa fedha ipasavyo ili yaweze kushughulikiwa iwapokuwa kwa awamu.

Kuhusu nyumba ya Mhe. Spika, iliyopo Uzunguni, Wete hali yake siyo mbaya ila tatizo kubwa liliopo hivi sasa katika nyumba hiyo ni ukosefu wa maji safi ya matumizi, kwani hulazimika kununua maji kila wanapopata wageni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa maelezo zaidi naomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie ripoti ya Kamati.

**TUME YA UCHAGUZI**

Tume ya Uchaguzi Zanzibar inaendelea kutekeleza majukumu yake kama ilivyopangiwa ikiwemo kufanya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015 kwa kuendelea na zoezi la ugawaji wa Shahada za wapiga kura Unguja na Pemba.

Aidha, Tume pia inaendelea kumalizia hatua za mwisho za zoezi la uchaguzi wa idadi, majina na mipaka ya majimbo zoezi ambalo linategemewa kumalizika kabla ya mwezi wa April, 2015.

Mbali na utekelezaji wa majukumu yake Kamati ilibaini changamoto zifuatazo katika Tume ya Uchaguzi:-

1. Kamati ilibaini Tume ya Uchaguzi Pemba haina majengo yake yenyewe ya kufanyia kazi. Ofisi imo katika jengo kongwe ambalo wamelirithi kutoka Wizara ya Biashara, licha ya matengenezo jengo hili haliendani na mazingira ya kiuchaguzi kwani lipo barabara kuu, limezungukwa na maduka na halina mlango wa kutokea wakati wa dharura.

2. Aidha, Kamati pia kwa Pemba Ofisi za Tume za Wilaya zote zimo katika majengo ya Ofisi za Wakuu wa Wilaya hali ambayo inapunguza muono wa uhuru katika masuala ya kiuchaguzi.

3. Ufinyu wa Bajeti.

4. Ukosefu wa elimu ya uraia miongoni mwa wananchi.

5. Kutochukuliwa kwa vitambulisho vikongwe vya wapiga kura kwa upande wa Pemba. Ni vitambulisho 234 tu ambavyo vimechukuliwa kati ya vitambulisho 333, licha ya njia mbalimbali za kupasha habari kutolewa.

### **MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Tume ya Uchaguzi Zanzibar kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria za nchi ili kuepusha vitendo vya uvunjifu wa amani hasa katika vipindi vya Uandikishaji na Uchaguzi wenyewe.
2. Aidha, Kamati inapenda kuishauri Tume kuendelea kutoa elimu ya uraia kwa wananchi na kujua haki zao na mipaka yao kwa mujibu wa sheria. Elimu hii zaidi juu ya masuala yanayohusu mambo ya Uchaguzi na wajibu na haki za raia pamoja na masuala yanayohusu haki za binaadamu.

### **SEHEMU YA TATU**

#### **HITIMISHO**

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumalizia napenda kuchukua nafasi hii kutanabahisha kwamba muhtasari huu pamoja na ripoti yake kwa ukamilifu wake ichukuliwe kuwa ni sehemu ya ripoti ya Kamati na vyote naomba viingie kwenye *Hansard*. Kwa ujumla Kamati imeweza kufanikisha majukumu yake kwa kufuatilia utekelezaji wa kazi katika taasisi zilizoainishwa katika ripoti hii kwa ufanisi mkubwa.

Kamati pia inashukuru jitihada zinazochukuliwa na taasisi hizo katika utekelezaji wa kazi zao ambapo Kamati imeweza kutoa maelekezo, ushauri na maagizo ambayo inaamini yataweza kusaidia kutekeleza majukumu ya Serikali kwa ufanisi kupitia Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Pia, Kamati inatoa shukrani kwa wale wote waliofanikisha kazi za Kamati kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na pia kuwezesha taarifa ya Kamati kutayarishwa na kuwasilishwa kunakohusika.

Aidha, Kamati inamshukuru kwa dhati Mhe. Spika, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, watendaji wote wa Serikali, Watendaji wa Baraza la Wawakilishi na wote waliofanikisha kazi za Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, baada ya uwasilishaji huo, sasa tutasitisha shughuli za Baraza letu hili hadi saa 11.00 barabara jioni kwa ajili ya maendeleo.

*(Saa 06.03 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*



**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, wakati wa asubuhi tulimalizia kwa ripoti ya Mhe. Mwenyekiti na ripoti ile ikapokelewa sasa ni zamu ya wachangiaji tunaanza na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, baadae Mhe. Ismail Jussa Ladhu na kama kuna wengine ambao wanataka kuchangia ripoti hii tunaomba waleta maombi yao huko. Ahsante.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru sana kwa leo hii kuweza kupata nafasi ya mwanzo kama kawaida yangu, lakini japo watu wengine inawauma potelea mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu hasa nikazanie katika yale matamshi ambayo tuliyokuwa tukitamka wana Kamati kwa kuielekeza Serikali na huo ndio wajibu wetu wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi sana wajumbe tunapotoa agizo kwa kuipeleka Serikali Kuu, mara nyingi sana tunapenda kupata mafanikio ambayo yaliyokuwa yenye asilimia ya kuridhisha katika wizara. Lakini mara nyingi sana tunapata hoja ya kuambiwa bajeti finyu, bajeti finyu, bajeti finyu, hiyo ndio lugha ambayo tunaipata. Kwa kuwa sisi Wajumbe wa Kamati hatutochoka kwa mujibu wa Kanuni zetu kutoa agizo kwa Serikali Kuu, kwani tunajua iko siku itatokea rehema wanaweza wakafanikisha.

Mhe. Mwenyekiti, tulisema sana suala la kisakina, kwenye ripoti leo hii ya Kamati iligusia sana na mara nyingi sana mimi nilikuwa nikisema hapa sijui watu wanakuwa wananifahamu lugha yangu au inakuwa na utata lugha ya maongezi. Kwa sababu kile tunachokizungumza unajua mara nyingi sana Mhe. Mwenyekiti, huwa napata *reference*. Safari moja tulikwenda kwenye mkutano ulikuwa Nungwi na Mhe. wangu Makamu wa Pili, alikuwepo kule siku hiyo niliona *fence* na siku hiyo sijui ilikuwaje simu yangu ilikuwa haina *camera*, maana yake ilikuwa vichekesho.

Kisakina kimepata pancha tayari Mhe. Makamu anataka kuondoka ama kweli siku hiyo ilikuwa *fence* kubwa sana maana yake nilicheka mpaka udenda ulinitoka. Sasa wale badala ya kutumia jeki ilibidi watumie wao wenyewe polisi kwa kukibeba kisakina kwa kuweka mpira mwengine (*step ring*). Kwa kweli ni jambo ambalo haliridhishi.

Mhe. Mwenyekiti, tungeomba sana siku moja Mhe. Waziri alitwambia tayari *ame-connect* na watu wa Maskati na tukaambiwa wakati wowote vinaweza vikafika. Sasa nikubaliane na waziri kwamba bado viko njiani meli inakuja, hilo nalikubali sana wala sina pingamizi, naomba aharakishe tu viingie kwa wakati, kwa sababu bado visakina ni viwili. Kwa taarifa tuliyoipata leo visakina vipya viwili na viongozi wako wengi wanataka kutumia visakina.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, niombe sana Serikali *vi-escort*, sakina ni *escort* ndugu yangu, ukisema sakina watu wanafahamu Zanzibar nzima vile vinaitwa visakina, *escort* ni jina ambalo jengine la Kiingereza. Sasa nikisema *escort* nitawapa tabu wale Waswahili wenzangu kule mitaani bora niseme kisakina ndio wanavyofahamu sana hivyo, naomba ndugu mjumbe nikubalie hapo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hili suala ambalo tunaomba sana kwa kuwa sasa hivi tunakwenda na wakatim magari mazuri kitu ambacho kinachonishangaza mimi utanunua buti na soksi iwe mbovu, haiwezekani. Magari ya wakubwa mazuri sana *BMW* na *Mercedes Benz* sasa leo unakwenda kuchukua kisakina kidogo kibovu hairidhishi, ki-voxy wagon kibovu unakwenda kumuwekea pale Makamu wa kwanza, Makamu wa Pili au Rais mwenyewe. Kwa kweli hairidhishi tulateeni vipya na sisi tunajiandaa kuwa Marais angalau tutumie vile vipya, ndio maana yake msione tabu, mkiona muda labda unapita wengine watakuwa hawavipati. Kwa hivyo, mimi naomba sana hili suala liweze kufikishwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili katika kumpongeza kwangu, unajua kuna watu wengine hawafahamu nini kazi ya Makamu wa Pili, yaani hawafahamu sana. Sasa leo naomba kidogo niwape taaluma ya kuwaelimisha.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar huyo ni muhimili mkubwa katika shughuli hasa za Serikali, lakini watu wanapokwenda na matatizo yao wanakuwa na elimu au wanajua wana uhakika *hundred percent* labda wanaweza wakafanikisha katika matatizo yao wanayoendea pale.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mgogoro wa ardhi, kwa kweli hili suala Mheshimiwa, huwa tunampa mzigo mkubwa sana, lakini ninachotaka kumuomba kwanza hapa angeweke kitengo maalum ili kuweza kufanikisha na kuondoa matatizo ya mgogoro ya ardhi na kufuatilia kwa kina kwa mujibu wa sheria.

Kwa sababu wengine wanapokwenda kwa Mhe. Makamu wa Pili, wanakwenda kama wao wanakuwa hawana *document* na wanakwenda kama wao tu na akifika pale mtu anajieleza vya kujieleza. Sasa mara nyengine sana Mheshimiwa huridhika na upande ule wa kwanza, haangalii na upande wa pili. Kwa hiyo, tungekuwa na Kamati ambayo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, angeiachia na akairidhia, kwa sababu ile Kamati ingeweza kutafuta *sides* zote mbili; sehemu ya kwanza na ya pili.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba sana hili suala Mhe. Makamu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ajaribu kuunda tume hiyo, kwa sababu juzi moja mimi nilipokuwa nikizungumza kwenye *ZBC* kuna mmoja alizungumza suala, ooh! Mheshimiwa, huoni kuwa hii Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, anapoingilia katika masuala haya ya ardhi nakutoa uamuzi na kila kitu, ni kukiuka sheria.

Nikawaambia hapana, mimi nikamjibu nikawaambia ni utendaji, ameshapata lile jambo ambalo lililompa uhakika wa umiliki wa mtu nani au nani similiki na ndio maana akafika pahala kutoa uamuzi huo. Sasa inafaa vizuri kwa sababu kuna barua ambayo anaweza akatoa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa kumpelekea waziri afatilie kwa mujibu wa sheria. Lakini inatoka barua inawezekana ikatoka kwa mwanasheria wake akatoa amri kinyume na ile barua ilivyokwenda. Sasa hapa kunakuwa na *something wrong*, sio.

Mhe. Mwenyekiti, hapa inakuwa haieleweki, kuna mambo ambayo yanakuwa yanachanganyika huku na huku. Kwa hiyo, mimi naomba sana hili suala kuwekwe na *team work* isiridhike na upande mmoja watake ushahidi na upande wa pili kwa sababu kuna watu wanafanya *forgeries* za mikataba, unajua watu wajanja sasa hivi nchi hii. Halafu wakiona kuna watu wengine wameshituka, sasa wao wanawatafutia mazingira mabaya na kuwasema vibaya wanavyotaka wao wenyewe, lakini hawafahamu kama lile kosa la jinai walilolifanya, hawaliona hilo.

Ni kosa kubwa sana la jinai kwenda kumuibia mkataba mtu au kufanya *forgery* ya mkataba, hilo mtu halioni au *forgery* ya *sign* ya mtu mwingine hilo hawalioni. Na tunavyojaribu kupeleka barua ikiwa kwa Marais, ikiwa kwa Makatibu kwa Mawaziri hebu tupeleke vielelezo vinavyohusika vya kufanya wewe kweli una haki ili Rais aweze kutoa haki. Lakini wewe unapokwenda pale unakwenda kutoa barua tu kwamba mimi nimeonewa na Mshimba akiwemo na nani akiwemo, sasa hutoi uthibitisho huyu mtu unayemsema baadae na yeye anaweza akaingia kwenye vyombo vya sheria kwa sababu umemdhaliisha, toa hili jambo anahusika na nini.

Sasa nimeona nalo hili nilizungumzie kwamba ni lazima kuwepo na *special committee* ili kuweza kusahihisha hili suala na kuweza kufuatilia hili jambo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimekuja na mikataba hiyo na ningependa sana watu wake kama wapo Makamu wa Pili wangeona haja ipo au kama watu wa rushwa, kitengo cha rushwa naomba kama ipo haja waje niwaoneshe mikataba na niwape, halafu wao watatafuta njia ya kisheria. Sasa hizo wakija kuziona wao na yale maelekezo waliupeleka kule kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ataweza kujiridhisha, ataona kumbe kweli kama sio tabia nzuri au sio vizuri kusikiliza mtu kesi upande wa kwanza. Kwa hiyo, nimeona mimi niitolee ufasaha ili kuweza kufikisha ujumbe wangu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, niingie katika suala ambalo agizo letu la Kamati tulilitoa hasa katika mambo ya Jeshi la Polisi.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana hata ukiona Kamati inatoa agizo, basi kuna mambo ambayo yametendeka kinyume na sheria au bila ya askari kutokamilisha ushahidi kamili.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kesi hizi za unyanyasaji, mimi nakubaliana mkono kwa mkono, sio tatizo lakini isiwe Mahakama kama ambavyo unaweza kusema, ah, madhali huyu aliyemuingilia ni mtoto wa kaka basi nyie kubalianeni familia ili yaishe, "muonja asali ataonja mara ya pili", ataonja na mtoto wa jirani. Katoka ndani anakwenda nje, hili jambo kwa kweli si la kulifumbia macho.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilisema hapa nikalia, lakini leo sitolia nitajikaza kwa sababu Kizimkazi kumetokea tatizo moja kubwa sana mstaafu wa KMKM amemuingilia mtoto mdogo kinyume na utaratibu na mpaka leo jamaa

anadunda. Hajakamatwa ukiliuliza hilo *file*, kwanza nakushukuruni sana wajumbe leo mmekuwa *silence* mmenisikiliza vizuri *very good*.

Nakushukuruni sana wajumbe mmekaa kimya kwamba hili jambo kumbe kweli linawa-*touch* kweli. Huyu mtwana mkubwa na kitoto chenyewe kidogo, amemuharibu vibaya sana, wanazungushwa maana yake mpala leo hii anadunda yuko Kizimkazi hajatiwa ndani, tuna polisi, tuna nani, tuna watu mpaka leo hii, sasa sisi tunataka ushahidi wa aina gani, niseme ushahidi wa kinyumbani au tunataka ushahidi vipi?

Haidhuru ndio *DNA machine* hatuna basi mtoto hajui kusema na mtoto anasema mimi akinipa peremende huyu babu, sasa sijui mnataka tuseme vipi. Kwa kweli hili suala Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, umeona tabu ya kupata ushahidi kwa mbali niite mimi nitakupa *reference* ya ushahidi tosha, kwa nini uone tabu kwa sababu sisi wote jamii tunafanya kazi. Mimi nafanya kazi chini ya Makamu wa Pili wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais, anafanya kazi chini ya Rais mwenyewe na mimi ni kiongozi na mimi nina haki ya kufanya kazi kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa kweli hili suala linasikitisha hawa wazee walienda kwa Kamishna wa Polisi walipofika kule kuna mama mmoja akaitwa, kwa kweli wale wazee waliangua machozi baada ya kutoka pale. Baada ya yule mama kuonesha msaada aliwaambia kumbe mtoto wenyewe kazoea, kama hakuzoeshwa atazoea vipi? Hebu niambieni polisi hiyo na huyo ni mama, hao wazee hawasemi uongo walikuja kwangu na kilio ambaye mmoja ni mwananchi wangu wa Jimbo la Kitope, anakaa Kazole ambaye ni ndugu yake mama mmoja. Anasema huyo mtoto amezoea, Kamanda wa Polisi mkubwa huyo anawaambia wale kina mama, yule mama masikini ya Mungu alivumilia pale alipotoka kwenye ngazi alilia machozi, alitegemea atapata msaada mkubwa kwa chombo cha polisi, lakini lugha haikuwa nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, hili suala linasikitisha sana na mara nyingi sana tunawasema baadhi sisemi polisi wote, *of course*, baadhi ya polisi wengine sijui kuna tatizo gani, sijui inakuwaje hata ukilifikisha pahala wewe ukakamilisha jambo hili, linasikitisha sana. Naomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, mambo haya kukomesha kwetu tuangalie kubadilisha tabia asikudanganye mtu, tabia haibadilishiki kama hakukuwa na sheria kali.

Mhe. Mwenyekiti, pakiwa na sheria kali mimi naamini tabia inaweza ikabadilika, lakini mtu anajua aah, mimi nikifanya kitendo hiki polisi wapo nitawalishia tu, nitawazungusha hivi, nitadanganya hivi na nitampa kitu kidogo polisi, mambo yatakuwa pabaya.

Mimi naomba sana Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Kamishna bado arudi kwa polisi wake awaeleze, awape *training* awaambie nini msingi kama huu hatari yake. Kwa sababu huu haitegemei mimi na yeye au na mtu mwengine yeyote asijione mtu aah, mimi halinifiki lahasha, tuombe rabi rabi Mwenyezi Mungu atujaalie hadi ufe lisikufike jambo kama hili, ndio hili jambo ambalo tunaweza tukaliomba kwa Mwenyezi Mungu.

Kwa hiyo, mimi naomba sana kwa kuwa nimeliona hapa na kwa kuwa agizo tumelitoa sisi Kamati, mimi wajibu wangu ni kulinda agizo langu la Kamati, sitokuwa na jibu jengine, sitokuwa na uwezo wa kujibu hoja dhidi ya hivi ninavyotaka mimi. Kwa hiyo, mimi hapa ninaweka msisitizo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, hapa mimi ninaweka msisitizo kabisa, tuwe *serious* na jambo hili la watoto kunyanyaswa, watoto kudhalilishwa, watoto wanakosa haki zao wanavyoharibiwa za kimsingi kabisa. Linasikitisha sana na kwa nini utaniambia naling'ang'ania kwa sababu nina ushahidi.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja nilienda hospitali yule anayetoa *PF3* pale zamani tumezoea mzee Makwega aliniita Mheshimiwa, njoo nikupe siri nikuoneshe jambo utalia machozi lakini jikaze. Mimi nikenda nikaona vitoto viwili vya kiume vishaharibiwa vidogo kabisa, haya vipi akasema ndio hali hiyo Mheshimiwa, nikwambieni nini hali ndio hii mnaiona nyinyi wenyewe, vitoto Taifa la kesho vijanadume viwili jamaa aliyeko sasa hivi kanionesha. Nilitoka machozi lakini nilijitahidi sana siku hiyo, maana yake nusura yajae kwenye mfuko kutokana na hali halisi yalivyokuwa yakinitoka.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana Serikali tuache yote...

**Mhe. Mwenyekiti:** Una dakika tano Mhe. Mjumbe.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Eeh!

**Mhe. Mwenyekiti:** Umebakiwa na dakika tano.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Wachangiaji wenyewe tumebaki wawili tu Mhe. Mwenyekiti, nipe raha, hakuna wengine, nawavuta vuta angalau watu wanachangia changia wakati wanapata *speed* sasa hivi. Sawa Mheshimiwa, nimekusikia kwa heshima yako, naheshimu kiti chako, lakini ndio ninawapa *speed up* hawa wachangiaji wengine.

Mhe. Mwenyekiti, niondokane na suala hilo, niende kwa waziri wangu dokta hapo. Mheshimiwa, hiki kitengo cha rushwa kwa kweli kimekuja kwa wakati mzuri sana. Mara nyingi sana huwa nasema jamani tunapounda sheria, tutapotafuta vitengo vya kuweza kutusaidia tuanze kuji-*prepare* na yale mambo yalikuwa muhimu. Nakushukuru sana gari wameendelea kupata, ulinzi wamepata hilo nitoe hongera kubwa sana kwa sababu ni sehemu moja ya kitengo ambacho kilichokuwa ni cha hatari sana hiki na kina fitina ndani yake.

Sasa leo mtu akawa hana gari akifadhiliwa gari na mtu mwingine hakuna kazi, hakuna kazi. Mheshimiwa, itakuwa. Sasa hili nilipongeze sana, lakini mambo ya ndani ya mishahara mtaweka wenyewe vizuri kwa sababu lazima tuangalie mazingira na hali halisi ya kitengo hiki ni sawa sawa na Mahakama. Kwa hiyo, mimi naomba sana Mheshimiwa dokta, kwa kuwa mimi ni Kamati yangu kama nilivyokwambia nitadokoa dokoa tu, lakini sheria tumepitisha juzi ya *PP*.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii naomba sana tuna tabia Serikali ku-*delay* kupitisha miradi haraka, sababu mimi nashindwa kuzielewa, miradi inakuwa mizuri, lakini mpaka wawekezaji wananuna, hili mliangalie Serikali, tatizo liko wapi. Nasikia sasa hivi sheria tayari kuna miradi inaambiwa ije katika Mambo ya Tume ya Mipango, naomba wawe *faster* basi, ikija miradi kama ile i-*forward* kule kunakohusika. Naomba sana masuala haya yawe *faster*, lakini tuna tabia ya ku-*delay*, kwa kweli mpaka yule mtu anachoka anakwenda akirudi tu, wengine wanakuwa Marekani.

Kwa hivyo, mimi naomba kwa heshima na taadhima hii *PPP* itengeneze mazingira mazuri yaoneshe kazi halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwa Makamu wa Kwanza wa Rais, nawashukuru sana Mhe. Waziri na watendaji wake wakuu wote, nawashukuru sana na leo walionesha mfano, walikuwa wengi sana, lakini najua sasa hivi sijui kuna mvua huko nje. Leo walikuwa wengi, walikuja na sasa hivi wako njiani wanakujam maana sisi tunachelewa Waheshimiwa Wawakilishi siwalaumu, lakini leo walionesha mfumo mzuri. Mhe. Makamu wa Pili *well and good*. Leo wamekuja watu sana, wamekuwekea heshima kubwa watu wako na naambiwa wapo huko nimeshamsikia katibu wangu anasema nipo. Mimi nakubaliana na wewe katibu endelea.

Mhe. Mwenyekiti, tuna Sheria ya Mazingira tulipitisha, sheria hii tumesisitiza utendaji wake wa kazi hasa *ZIPA* asiamuru mradi kama watu hawajapita katika masuala ya mazingira kuangalia au kutoa kibali ambacho kinakubalika kwa mujibu wa sheria. Kufanya hiyo *environment associate*, ndio hiyo hiyo, unajua wakati mwingine mdomo unakuwa mzito kutokana na mate, hatuna pahala pa kutemea, sasa inakuwa ndio hivyo.

Kwa hiyo, hizi sheria tulizozitunga hebu tuwe *serious* katika utendaji wake wa kazi, kwa sababu hawa wenzetu wataalamu wanapokaa wakajifungia na wakatafuta wadau, wakatutafuta na sisi Kamati na hata kuingia ndani kuweza kuchangiwa si jambo la masihara, hapo *cost* nyingi imeshapotea hasa pesa za wavuja jasho.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana sheria lazima ifuate mkondo wake, tuwape nafasi tuwasikilize wanachosema, mtu akisema hiki kitu *failure*, tunaomba sisi tusiweke mkono kutokana na *failure* ilivyo. Kwa sababu wao ndio wanaojua kuwa hili jambo halikukubalika hapa hoteli utajengaje pahala pana mmong'onyoko.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa, muda wako umemalizika.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, nataka nipongeze sasa, kwa heshima yako na taadhima naiunga mkono kwa asilimia mia moja wizara zote zilizopo hapa.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) ambaye kupitia neema zake na rehema zake ndio tukawa na nguvu ya kusimama humu tukiwa hai na wazima kutekeleza yale ambayo yanatupasa kama Wawakilishi wa wananchi wa Zanzibar katika chombo hiki ambacho muasisi wake Rais wa Pili wa Zanzibar Sheikh Aboud Jumbe Mwinyi Mwenyezi Mungu ampe umri na afya alikiita ni ngome ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia mjadala huu wa Taarifa ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Vile vile, taarifa za mawaziri husika wa ofisi hizo tatu za utekelezaji wa maagizo ya mwaka jana.

Mhe. Mwenyekiti, nataasaf kusema kwamba nimeamua kuchangia eneo moja tu katika ripoti hii ya Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na sababu yangu nitaijeleza. Katika ripoti hii ukurasa wa 9 hadi wa 10 kuna maelezo yanayohusu Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa umuhimu wake naomba niisome kwa kuinukuu. Inasema kama ifuatavyo:

"Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali maoni na ushauri wa Kamati. Kamati inaridhishwa kwa kiasi juu ya uratibu wa shughuli za Serikali unavyofanywa hivi sasa, lakini inashauri mambo yafuatayo yazingatiwe ili kuimarisha uratibu huo na kufikia dhamira na malengo pamoja na mategemeo ya wananchi kwa nchi yao.

Moja, Serikali ihakikishe utekelezaji wa taarifa za Kamati za Kudumu na Kamati Teule za Baraza zinafanyiwa kazi ili kupunguza kero katika jamii na kupelekea wananchi kuwa na imani na Serikali yao, kwani maelezo yanayotolewa Barazani mengi huwa yanatoka kwa wananchi na utekelezaji wa maagizo hayo ndio kuwatumikia wao.

Vile vile, kuna ubadhirifu mwingi uliogundulika na Kamati zilizoundwa na Baraza la Wawakilishi, lakini hatuoni hatua za haraka kuchukuliwa, hii itapelekea wale wakosaji kujihisi wako sawa na wengine kuweza kufanya kama hivyo, kwani watahisi kufanya ubadhirifu ni jambo la kawaida tu. Hivyo, hata malengo ya Serikali itakuwa ni ndoto tu ikiwa tutaendelea kuoneana muhali huku wachache wakiitafuna nchi. Kamati inaamini ikiwa Serikali itakuwa makini basi bado kuna uwezo mkubwa wa kujitegemea kwa bajeti ya matumizi ya kawaida kupitia mapato yetu ya ndani bila ya kutegemea wafadhili kutoka nje.

"Aidha, kwa kuwa sasa tumeshatunga Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, wakati umefika sasa wa tume baada ya kuanza kazi zake rasmi kuanza na Ripoti za Kamati Teule za Baraza ili kurejesha imani ya wananchi kwa Serikali yao. Tukiangalia Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011 ambayo ndiyo inayoisimamia inaeleza wazi kuwa: "Utawala bora ni utumiaji wa madaraka kwa ufanisi, uaminifu, usawa, uwazi na uajibikaji katika ngazi tofauti za Serikali."

Mwisho wa kunukuu wamenukuu ukurasa wa tatu wa hiyo Seya ya Utawala Bora.

"Hivyo, Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ihakikishe kuwa inasimamia utekelezaji wa sera hiyo, kwani wao ni kiungo muhimu cha kufanikisha shughuli za Serikali na hivyo kutimizwa kwa matarajio ya wananchi kwa Serikali yao".

Mhe. Mwenyekiti, maelezo haya ukiondoa hii *paragraph* inayozungumzia Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, kama yalivyo na neno kwa neno unayasoma katika Ripoti ya Kamati hii hii ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka jana ambayo ninayo mkononi hapa. Vile vile, iko katika ukurasa wa 9 hadi wa 10, anayependa kufanya utafiti zaidi anaweza kwenda kuitafuta ripoti hii atayakuta maneno niliyoyanukuu yameandikwa neno kwa neno, ingekuwa lugha ya watu wa mwambao kule Mombasa wanasema "chapa kwa ya pili".

Mhe. Mwenyekiti, sasa nimesema najikita katika eneo hili moja, tangu tumeanza kupokea Ripoti za Kamati hii ikiwa ni Kamati ya tatu nimekuwa nikisema na kurejea tena na tena kwamba Serikali hii si makini na imeshindwa

kazi. Wengine mkawa wakali sana, nasema mkawa wakali Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu pamoja na wewe ulipokuwa umekaa huku nilikokaa mimi. Lakini nasema haya niliyoyasoma na kwamba yamekaririwa tena vile vile kwa mwaka jana ndio ushahidi kwamba Serikali hii imeshindwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, tangu tumeanza mara hii tumeshuhudia vituko vya ajabu katika Baraza hili. Kwa mfano juzi tulitanabahisha hapa kuna wizara moja imeandika ripoti ya maagizo yaliyotolewa mwaka huu, ikabidi kufanyiwa marekebisha asubuhi siku ya pili. Lakini kwa jumla kila Kamati ukiisoma kwa ujumla wake katika maudhui ukiondoa hili ambalo limeandikwa neno kwa neno kwa jumla maagizo yake yamekuwa yanajirejea kila mwaka.

Nilichangia hili kwa uchungu mkubwa sana katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, nikachangia Kamati ya Maendeleo ya Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto nikakaa kitako baada ya kuona wahusika ambao napaswa kuzungumza nao hawapo Barazani. Lakini leo sikuchukua zote nimekuja nazo tatu hapa;

Hii ni ripoti ya mwaka 2012/2013, hii ni 2013/2014 na hii tulionayo sasa ni 2014/15. Ukisoma katika maeneo mengi ni yale kwa yale, "chapa kwa ya pili", au kwa maneno yetu "yayo kwa yayo, maji ya futi na nyayo".

Mhe. Mwenyekiti, moja wapo na chombo hiki hiki cha kujipima hapa ama Kamati hatufanyi kazi na uzuri wake wananchi ndio watakaotupima maana sote tunarudi kwa wananchi, kwamba tunanukuu yale yale kumbe hatufanyi kazi, tunakwenda kuzidurusu ripoti zile zile au ni kwamba haturidhiki kuwa mambo yako vile vile tunaendelea kurejea maagizo yale kwa yale. *(Makofi)*

Mimi mtazamo wangu na nauamini kwa dhati ya nafsi yangu ni kwamba la pili ndio sahihi tunarejea kwa sababu hayatekelezwi. Shahidi wa haya ni yale ambayo tumeyanukuu hayakuwa yamenukuliwa neno kwa neno, lakini maudhui yalikuwa yale yale katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambayo aliisoma ndugu yangu Mhe. Wanu Hafidh Ameir. Zaidi shahidi wa haya ni wananchi wanapooona matatizo yao yako vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, mpaka leo tujipime kwamba kwa nini Baraza hili kuanzia mwaka 2011/2012 mpaka 2013 lilikuwa na mvuto mkubwa sana kwa wananchi kupitia mijadala yake na kwa nini sasa wananchi wale wale wamepoteza mvuto na mijadala ya Baraza hili. Zanzibar hii ndogo wanatwambia tunakuoneni mnapoteza wakati wenu na kupoteza wakati wetu mnarejea yale kwa yale, hakuna moja liwalo.

Sasa nimependa kuinukuu sehemu ile kwa sababu kwangu mimi wa kubeba dhamana katika hili ni Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Kwa sababu ofisi ambayo imepewa dhamana ya kuratibu shughuli za Serikali katika serikali nzima ni Ofisi ya Makamu wa Pili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba ninukuu Katiba yetu ya Zanzibar isije ikaonekana labda haya ni maneno ya Ismail Jussa tu leo kashiba mseto vizuri, kwa hivyo, labda yanamtoka tu hapa.

Katika Katiba yetu, kifungu cha 39(7) kinasema;

"Makamu wa Pili wa Rais atakuwa ndiye Mshauri Mkuu wa Rais katika kutekeleza kazi zake na pia atakuwa ndiye Kiongozi wa shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi".

Mhe. Mwenyekiti, lakini isitoshe, ibara ya 43(5) inasema;

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndiyo itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya Sera za Serikali kwa ujumla na Mawaziri chini ya uongozi wa Makamu wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar".

Mhe. Mwenyekiti, ninaposhuhudia maagizo ya chombo hiki muhimu ambacho muasisi wake kakiita ngome ya wananchi hayatekelezwi kiasi ambacho Kamati inarejea yale kwa yale kila mwaka, mimi nachukulia kwamba hii ni *failure* ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika kuratibu shughuli za Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi mara nyingi najiuliza hii Idara ya Uratibu shughuli yake kubwa ni nini, ikawa inagharamiwa? Mimi nilitegemea hii katika vikao vya Baraza sio katika Ofisi ya Makamu wa Pili tu, kila siku ya

Mungu iweko hapa kwa sababu shughuli yake ni uratibu haina shughuli nyengine, ichukue kila maagizo yakishamalizwa hapa yanayotolewa na yakafanyiwe kazi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme inawezekana kuna dhana mbovu inajengeka kwamba haya ni maagizo ya Kamati ni maagizo ya Kamati kabla ya kufika Barazani, yakishafika hapa, yakasomwa na yakajadiliwa, pale mwisho unapotuhaji walioafiki ripoti hii ya Kamati tukanyanyua mikono, maana yake yameondoka kuwa ya Kamati na yamekuwa ya Baraza na yamekuwa ya wananchi kupitia umilikishwaji uliofanywa na Wawakilishi wao ambao ndio sisi humu ndani, isingewezekana watu 1,300,000 tukakusanyika pamoja tukaja tukaamua ndio maana dunia tulikotoka huko tangu zama za Wagiriki kukawekwa utaratibu wa kuwa na Wawakilishi wanaochaguliwa na wananchi wakapewa ridhaa kuja kuwakilisha katika vyombo kama hivi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niseme nimesikitika sana na ushahidi wa hayo, tazama leo angalia haya maeneo ambayo tunapewa ripoti zake, nataka kutoa mfano huu wa leo kwa sababu leo hasa nimekusudia kuzungumzia Ofisi ya Mratibu. Kwa sababu nimechoka mimi na wenzangu kila wakati kuzungumza yayo kwa yayo humu ndani ya Baraza la Wawakilishi, msifikiri tunapenda sisi kutumia nguvu kubwa kuyazungumza haya yanatuchosha kwamba unalosema halichukuliwi hatua, inachosha kwamba unalolisema lile kwa lile halichukuliwi hatua.

Mhe. Mwenyekiti, kuonesha kwamba hakuna umakini katika kuratibu shughuli angalia ripoti hizi, unaichukua Ofisi ya Rais, Ofisi Kuu ya Kiongozi wa nchi ingepaswa iwe mfano kukosa umakini. Nimeiangalia taarifa hii ya mwaka jana kilichotolewa ripoti humu ndani kimechukuliwa yale maagizo ya jumla ya mwisho ambayo yako katika ukurasa wa saba mpaka wa nane wa ripoti ya mwaka jana, lakini humu ndani kuna maagizo kwa kila idara.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia humu Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba imepewa maagizo sita mwaka jana yako ukurasa wa tatu, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na *DIASPORA* imepewa maagizo mawili yako ukurasa wa nne, Idara ya Utawala Bora imepewa maagizo manne yako ukurasa wa nne hadi wa tano, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kuhujumu Uchumi imepewa maagizo tisa yako ukurasa wa tano hadi wa sita, Ofisi ya *CAG* ina maagizo manane yako ukurasa wa sita hadi wa saba, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu ina maagizo mawili yako ukurasa wa saba na halafu ndio hayo maagizo ya juma kumi yaliyoko ukurasa wa saba na nane. Leo ripoti iliyokuja kusomwa hapa ina maagizo yale ya jumla tu.

Hivyo hivyo kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza. Ofisi hii Tume ya *UKIMWI* kuna maagizo mawili yako ukurasa wa 19, Idara ya Watu wenye Ulemavu kuna maagizo mawili yako ukurasa wa 19, Idara ya Mazingira ina maagizo manne yako ukurasa wa 20, Tume ya Uratibu na Udhhibiti wa Dawa za Kulevya ina maagizo mawili yako ukurasa wa 20 hadi 21, Ofisi Kuu Pemba ilikuwa na maagizo saba yako ukurasa wa 21 hadi 22 halafu ndio yako ya jumla ambayo yako ukurasa wa nane hadi wa tisa.

Sasa unapokuja kuzitizama hizi ripoti unajiuliza maneno tele, Serikali hii kweli iko makini na *serious*? Kwa sababu hakuna binadamu anayependa kudharauliwa, mbaya zaidi hunidharau mimi kama Ismail Jussa, humdharau Mhe. Hija Hassan, humdharau Mhe. Hassan Hamad, humdharau Mhe. Mohamedraza, kwa hapa tukikaa kwa pamoja unakidharau chombo cha uwakilishi wa wananchi, yaani ngome ya wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema hayo kwa sababu hapa tunaonana na tunajuana, juzi kuna waziri mmoja humu ndani, mfano mwengine wa kuonesha kwamba tunafeli katika uratibu. Kuna waziri mmoja mpaka unawasilisha mezani kwamba anakuja kusoma maagizo hana hapa, katufungia ngulai katoka hapa kwenda kuandika, anaaga anakwenda kuandika anakuja kutusomea maagizo ya mwaka jana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini ukosefu mwengine wa umakini umeonekana jana hapa, kwamba Wizara ya Afya hoja yake iko mezani Kamati yake inajadili, si Waziri au Naibu Waziri analoona umuhimu wa kuweco hapa, tena wengine wanaleta *message* kwa njia za simu waambie hao tunawasikia huku. Sasa kama mmekaa huko majumbani mnatusikia na sisi tungeweza kuuliza kwa simu na mkatujibu kwa siku na tusingekuja hapa tukapoteza pesa za wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, hakuna umakini.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nimesema inasikitisha sana na nimalizie kwa kusema, mimi nimefurahi sana kwamba Kamati hii ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi wa Kitaifa katika ukurasa wake wa 11 imekuja na pendekezo zuri sana

katika suala la Sheria za Kitaifa. Kwamba tumtangaze Rais wa kwanza wa Jamhuri wa watu wa Zanzibar Marehemu Shekh Abeid Aman Karume kuwa ni baba wa Taifa la Zanzibar. Mimi naiunga mkono sana, lakini itakuwa haina maana na tutafanya unafiki wa hali ya juu kumtumia Mzee Karume kisiasa lakini yale anayoyataka hatuyasimamii.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mzee Karume ya mwanzo niliwa siku moja kuisoma hii ilikuwa na jumla la waziri 10 tu; Mawaziri na Manaibu Waziri, ilikuwa na Rais mwenyewe -

Rais Shekh Abeid Aman Karume	-	Abeid Aman Karume
Makamu wa Rais Shekh	-	Abdallah Kassim Hanga
Waziri wa Fedha na Maendeleo	-	Hasnuu Makame Mwita
Waziri wa Elimu na Utamaduni	-	Othman Sharifu
Waziri wa Kazi, Njia za Umeme Shekh	-	Idrisa Abdul Wakili, Mungu amrehemu
Waziri wa Afya na Majumba Shekh	-	Aboud Jumbe Mwingi
Waziri wa Mambo ya Nje na Biashara Shekh		Abdrahman Mohamed Babu

Walikuwepo na wasaidizi Mawaziri wawili; mmoja katika Afisi wa Rais ambaye alikuwa ni Abdul-Azizi Twala na mmoja Waziri wa Nchi Afisi Wizara ya Kazi, Nguvu za Umeme Shekh Hassan Nassoro Moyo.

Kazi iliyofanywa na hawa tumeishuhudia mpaka leo tunajivunia, tunadhimisha kila mwaka Mapinduzi tunaendelea kukumbusha yale yale ya miaka 8 ya mwanzo, makubwa mengine hayapo baada hapo.

Sasa leo tungetegemea tuone uwajibukaji huo katika Serikali hii. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nasikitika sana kwamba Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika hili imetungusha na imeshindwa kazi na Mhe. Mwenyekiti, niseme Afisi kabla ilipokuwa Afisi ya Waziri Kiongozi ilikuwa wa Kwanza ni Mhe. Ramadhan Haji Faki na wa Pili ni Mhe. Seif Sharif Hamad, ikaja wa Tatu Dr. Omar Ali Juma, akaja wa Nne Dr. Moh'd Gharib Bilali na akaja wa Tano Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, lakini sijawahi kuona ukosefu wa umakini kama ninavyoushuhudia kama hivi sasa na mimi nadhani nimuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika hili awajibike, ajizulu na ampishe Rais tafute mwengine anayeweza kumsadia kazi hii. (*Makofi*)

Hatuwezi kufuja fedha za wananchi kuja kukaa hapa kutoa maagizo kila mwaka tukarejea yale yale, hakuna yanayotelezwa na viongozi bukheri wa hamsa ishirini.

Mhe. Mwenyekiti, nasema tena katika hili tumuombe sana Makamu wa Pili wa Rais akubali kabisa kuwajibika akae upande ampishe Rais atafute masaidizi anayeweza kufanya kazi ya utaratibu ili shughuli za Serikali ziende chombo hiki kifanye kazi yake.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**Mhe. Salim Abdallah Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kupata nafasi hii ya kutoa maoni yangu machache kuhusu Afisi za Viongozi Wakuu ambazo zinafanyiwa kazi na Kamati husika.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuanza kwanza nitoe shukurani za dhati kwa Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwa maelekezo yake na nia yake ni moja tu tuwe na *accountability* katika shughuli zetu. Na hili litaendelea mpaka hapo mambo tutakapoyaona yameelekea.



Mhe. Mwenyekiti, nianze na Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Katika ukurasa wa 4 wa ripoti yake kuna agizo la kwanza la Kamati hii ya Kudumu ya Baraza inayoshughulikia Afisi ya Viongozi Wakuu ambayo Kamati hii iliekeza kumalizwa kwa haraka kwa utata juu ya swala la juu ya swala la Ikulu ya Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti, na hili katika majibu yaliyotolewa na wizara ni kuwa Afisi hii ikishirikiana na Afisi ya Tawala za Mikao na Idara Maalum za SMZ, Wizara ya Fedha pamoja wamekaa na mkandarasi kwa lengo la kutatua utata uliipo. Kimsingi utata huo kwa sasa umeisha.

Mhe. Mwenyekiti, ninavyoelewa katika Ikulu hii iliyoko Micheweni kulikuwa na matatizo makubwa baina ya Serikali na mkandarasi na huyu mkandarasi alikuwa akidai pesa zake nyingi tena kwa muda mrefu. Naomba kujua utata huu kama umemalizika na hauko tena ni kwa sababu huyu ameshalipwa haki zake au umu humu kimaandishi tu?

Jambo jengine kwa mujibu wa ripoti hii inavyoendelea ni kuwa kwa sasa ramani ya majengo na mambo mengine yanayohusiana na hayo, zimo zimeshachora upya na zinafanyiwa utaratibu wa kufanyiwa thamani kabla ya kuitisha zabuni ya kumtafuta mkandarasi atakaemaliza ujenzi wa jengo hilo. Jengo hili ambalo lilikuwa halijamaliza na limekuwa na utata wa kudaiana na sasa utata umemalizika, ningepomba kujua mkandarasi huyu wa zamani likianza kujengwa jengo hili atakuwemo katika hawa watakaotafutwa au yeye baada ya kumaliza utata ndio ametolewa nje na kwa sababu gani?

Mhe. Mwenyekiti, nikiendela na ofisi hii hii naomba kuzungumzia kuhusu mmongonyoko wa ardhi ulivyoenezwa na hii unaipata katika ukurasa wa 5 wa ripoti, ukisoma ripoti hii, mwisho imeeleza kuwa ofisi iliandaa andiko la mradi wa kushughulikia mmongonyoko katika nyumba ya Kibweni, Mkaoni, Bwefumu, Mkokotoni na gharama za mradi huo zinakisiwa hazipungui bilioni moja, milioni nane na laki tatu za sabini na kuwa fedha hiyo inatarajiwa kuombwa katika bajeti inayofatia.

Mhe. Mwenyekiti, huu mmongonyoko wa ardhi kama ilivyosema Kamati unahatarisa majengo haya na kila siku zikenda mbele mmongonyoko unaendelea na maji yanaongezeka na sisi tunajua tunapopitisha bajeti zetu wizara itaomba fedha fulani wengine hupewa mpaka 13%, kwa sababu wizara imetegemea bajeti ijayo kwa kukamilisha haya na hali yetu ya kiuchumi tunajua, je, kama haikuwezekana kupatikana hizi bilioni moja na laki nane, ndio basi tungejee bajeti ijayo au si vyema kama wizara ingelijiandaa kutafuta njia nyengine japo wa kuomba au kukopa na kadhalika lakini hili tatizo liweze kuondoka.

Mhe. Mwenyekiti, tukiendelea na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais sasa kuna agizo namba 5 ambalo liko ukurasa wa 14 na 15.

Mhe. Mwenyekiti, agizo hili ambalo linatoka kwenye Kamati linaeleza kuwa Kamati imeona kuwa kuna malalamiko na migororo mingi ya ardhi na kwa hivyo, Kamati kwa ufupi imeitaka wizara kujitahidi kuondoa matatizo hayo. Sasa kutokana na maelezo pamoja na juhudi nyingi zilizochukuliwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, lakini hatimae malekezo ni kuwa masuala yanayohusu migogoro ya ardhi yatasimamiwa na moja kwa moja na Mahakama hizi, yaani Mahakama za Ardhi kwa mujibu wa taratibu zuliopo ili migogoro hiyo ipate ufumbuzi wa kisheria.

Hapa Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeliomba nipaje majibu tokeoa Mahakama ya Ardhi kukabidhiwa migogoro hii ambayo ni mikuwa hata Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kashiriki katika kuitatua hadi hii leo ni migogoro mingapi Mahakama hii ya Ardhi imekabidhiwa na mingapi imetatuka, mingapi bado na mingapi baada ya kutatuliwa wahusika hawakukubali wakenda katika Mahakama ya Rufaa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, katika ofisi hii hii ya Makamu wa Pili wa Rais kuna agizo la Kamati na hili ni agizo nambari 19 na liko ukurasa wa 23. Kamati imeagiza kuwa swala la itikadi za kidini linapelekea uvunjifu wa amani isimamiwe ipasavyo na kuchukuliwa hatua za kisheria kwa yeyote atakaesababisha machafuko.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hili mimi binafsi ningeliomba kupata ufafanuzi kwa sababu ninavyoelewa nchi hii kila mtu ana uhuru kwa mujibu wa Katiba yetu kifungu 19 naomba kunukuu;

"Kila mtu anastahili kuwa na uhuru wa mawazo, wa imani na uchaguzi katika mambo ya dini pamoja na uhuru wa kubadilisha dini au imani yake".

Vile vile, katika kifungu kidogo cha pili cha Katiba kinaeleza;

"Bila ya kuathiri sheria zinazohusika kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa huru na jambo la hiyari ya mtu na uedeshaji wa jumuiya ya dini zitakuwa nje ya shughuli za mamlaka za nchi".

Kwa hivyo, watu wa dini wana uhuru wa kuabudu dini wanayotaka katika nchi hii, tuna Waislamu na wasiokuwa Waislamu, kila mtu ana miongozo yake ya kidini, hakuna kwa Waislamu na kwa wasiokuwa Waislamu kifungu chochote cha dini kilichokuwa kinaanisha kuhatarisha amani na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Isipokuwa dini inahimiza umoja, inahimiza udugu na inahimiza mashirikiano na kwa sababu Serikali kabisa kwa mujibu wa kifungu nilichokusoma haitakiwi kujishuhulikia na shuhuli za dini hapa nina masuala mawili.

(1)Hii Kamati imefanya utafiti gani wa kutosha mpaka ikaiomba Serikali ichukuwe hatua hii kwa mambo haya yanayohusiana na dini, wakati Serikali haihusiki kuingilia dini ya mtu yeyote.

(2)Kwa nini kwa sababu ni uhuru wa mtu kuabudu dini anayotaka na miongozo ya dini iko sivyo anavyotaka kwa kufuata miongozo ya dini ilivyo na moja ni kujenga amani. Ni kwa nini leo Serikali ikakubalia kupokea agizo hili na ikasema kuwa italifanyia kazi kwa kushirikiana kwa kushirikia na Vyombo vya Ulinzi na Usalama na kwa mashirikiano makubwa na viongozi wa taasisi za kidini.

Naomba Serikali injibu kwa upande wake na naomba naomba Kamati inambie imefanya utafiti gani mpaka ikaona kuwa kuna matatizo ya kidini yanayohatarisha amani mpaka ikaleta suala hili kwenye Serikali na likapokelewa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea, naomba sana niende katika ofisi hiyo hiyo ya Makamu wa Pili wa Rais na sasa hivi nitazungumza namba 20 la Kamati na hili liko katika ukurasa wa 23 wa taarifa hii na linahusu mambo ya tindikali.

Kamati imeiagiza suala la tindikali yaani *acid* lifanyiwe jitihada za makusudi kwa kudhibitiwa ipasavyo ili lisije likasababisha athari za mipasuko ya kidini. Nauliza tena.Hii Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi inayoshughulikia Ofisi ya Viongozi Wakuu ni Kamati ambayo ina wataalamu wa kutosha tunawaelewa, ni wazuri tu, lakini *acid* kuitia katika dini! Waheshimiwa mimi naomba tena utafiti walioufanya mpaka wakaileta hii.

Kwa sababu kama *acid* itatumika vibaya na kwa sababu takribani asilimia kubwa za watu wana dini zao; ikiingia huku inaweza ikaingia huku. Lakini kuna wazungu hapa hatujui kuwa wana dini au mapagani, wamepata matatizo haya. Kwa hivyo, kwa nini watu huleta vifungu kama hivyo ambavyo vinaashiria amani za kidini kutokana na vitendo vinavyofanywa. Kwa hivyo, ningeliomba sasa mambo kama haya yaliokuwa hayahusiani na kidini yasiingizwe katika dini ni kuelekea katika uchochezi na mimi hili siliungi mkono.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naendelea tena Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na sasa naenda katika agizo namba 23 na agizo hili iko katika ukurasa wa 24. Mhe. Mwenyekiti...

**Mhe. Mwenyekiti:** Una dakika tano za ziada.

**Mhe. Salim Abdallah Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, hapa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeagizwa kupitia wataalamu wake kuwa tayari kwenda kujifunza nchi za nje udhoefu kuhusu mambo mbali yanayohusiana mambo ya mafuta na gesi. Kwa sababu wakati nitasema tu.

- (a) Mhe. Mwenyekiti, ninavyojua kuwa Serikali tayari imeshapeleka vijana hawapungui 30 na tena wanapewa mikopo ili wakosome mambo haya ya kitaalamu. Hivi ilikuwaje Serikali kupoteza mapesa mengi kwa kupeleka wataalamu tu kwenda kule kuangalia na kurudi wala hakuna *feedback* tuliyoipa, kwa nini Serikali haitupi utaratibu endelevu kwa vile suala la mafuta ni suala nyeti, ikawa hawa wanafunzi wakapata taaluma katika fani mbali mbali zinazohusiana na mafuta na ikawa wanatosha kuja kuishauri Serikali tufanye nini ili shughuli hii iende ipasavyo.
- (b) Nataka nijue ni wataalamu wangapi waliokwenda kutoka Serikalini na ni fedha iliyotumika katika shughuli hizo na mrejesho gani umepatikana mpaka hivi sasa kwa sababu tunasikia kimnywa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile sina muda naomba pia niende kidogo katika hii Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na nasikitika kuwa muda hautoshi. Lakini Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais mimi jambo ambalo naomba kulieleza ni kuwa kuna mambo mawili kwa pamoja.

- (a) Kwanza kuna agizo namba tano kwa sababu ya wakati na agizo hili linahusiana na usafiri wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iliyoko Pemba kwa jibu lililotolewa na wizara haliridhishi. Kwa hivyo, naomba nipate maelezo zaidi.
- (b) Vile vile, agizo namba tatu hili linahusu Bodi ya Viwango, tumeona unga uliokamatwa ambao haufai kutumika na tendele. Hivi ndio vifaa tu vilivyoonekana vibovu?
- (c) Kwa sababu ninavyojua vifaa vibovu vimeenea hapa kila aina tunavyotumia kwa chakuka hata mchele, mchele tulionao hivi sasa kuna utaratibu watu wanachukuwa kilo moja huku na wanachukuwa na mchele wa mbeya angalau uweze kulika, mchele usiolika una uzima gani.
- (d) Nataka nijue kuwa hichi chakula kibovu au hivi vifaa vibovu ambavyo havifai kutumika ni kwa hapa Unguja tu au na Pemba pia ilifanywa hii kazi. Nataka nijue Pemba ni kiasi gani kilichopatikana aina gani na Unguja ni kiasi gani.

La mwisho kwa sababu ya wakati Mhe. Mwenyekiti, katika Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kuna suala linalohusiana na miundombinu. Kamati imeandikia lakini Wizara imejibu kuwa taarifa hii imepelekwa kwa taasisi inayohusika. Ninataka nijue ni taasisi gani ya wizara yake inayohusika na mambo ya mazingira au ni Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu inayohusika na mambo ya ujenzi wa barabara na kadhalika, kwa sababu ujenzi huu wa barabara unaharibu mazingira kiasi kikubwa kiasi ambacho hata kueleza hatuwezi.

Mfano hivi sasa Vitongoji ni mahandaki matupu kwa sababu ya shughuli hizi, Micheweni ni hivyo hivyo wala hakuna ujazaji na hata Mtambwe suala linatokea na shughuli za ujenzi bado zinaendelea. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atupe ufafanuzi ni taasisi gani hizo na zitafanya vipi kuona kuwa haya mambo yamerekebishwa ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya muda ni mdogo, sitongojea ukasema kaa kitako. Ninakushukuru. (*Makofi*).

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante. Anayefuata sasa ni Mhe. Salma Mohammed Ali baadae Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali.

**Mhe. Salma Mohammed Ali:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu kwa kunipa uzima na kuweza kusimama hapa.

Pili ninakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia taarifa hii ya Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa pamoja na utekelezaji waliotoa Mawaziri wa wizara tatu zinazosimamiwa na kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwenye agizo namba tano linalohusu usafiri wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii imetoa agizo la kutatua tatizo hili. Katika agizo hili Mhe. Waziri amejibu ofisi yake bado inaendelea na ufuatiliaji wake ili kupatiwa ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hakika jawabu hii hairidhishi. Iweje Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ishindwe kuwa na usafiri kwa mujibu wa maelezo ya Waziri, lakini Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti ya utekelezaji ya Mhe. Waziri wa Makamu wa Pili wa Rais kwenye ukurasa wa kumi na tano, Waziri wa Ofisi hii anajibu kwenye agizo namba mbili Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu, "Kwa upande wa usafiri tayari gari mbili kwa kuanzia kwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais zimeshapelekwa Pemba na kuanza kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuelezwa Mawaziri hawa wawili wa Serikali moja, wanaofanya kazi chini ya Kamati moja ya Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kutofautiana; mmoja akawa na kauli ya kusema kama Wizara yake inafuatilia kuondoa tatizo hilo na nyengine ikasema kama tayari gari mbili zimeshapelekwa. Naomba Mhe. Waziri Mhe. Mwenyekiti, tufahamishwe katika Mawaziri hawa wawili ni Waziri gani aliyelidanganya Baraza? (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani Mawaziri hawa wawili wakose uratibu kwa kiwango kikubwa au tuseme gari imepelekwa Pemba lakini ni gari hewa. Naomba Mhe. Mwenyekiti, nipate jawabu kuhusu hili. Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nikienda na agizo namba saba na tisa inayohusu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kusimamia tathmini ya kimazingira katika miradi mbali mbali. Hapa Mhe. Mwenyekiti, pia mimi sijafahamu jibu la Mhe. Waziri wa Makamu wa Kwanza wa Rais kwamba imewasilisha agizo hilo kwa taasisi zinazohusika.

Mhe. Mwenyekiti, maoni yangu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais chini ya Idara ya Mazingira ndiyo msimamizi wa tathmini ya mazingira. Haiwezekani agizo hili lililotolewa na Kamati kwa Idara ya Mazingira itoe agizo kwa taasisi nyengine. Kinachopaswa Mhe. Mwenyekiti, kufanywa kwa Idara ya Mazingira ni kuhakikisha hakuna mradi wowote unaofanywa bila ya tathmini ya mazingira, kufanywa kwa kusimamiwa na Idara ya Mazingira na mradi usiofuata masharti hayo lazima Idara ya Mazingira iwe na uwezo na meno ya kuzuia.

Mhe. Mwenyekiti, agizo hili lilikuwa halipaswi kupelekwa kwa taasisi husika, linapaswa kusimamiwa na Idara ya Mazingira yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa niende katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kuna agizo namba kumi na sita kuhusiana na matunzo na masomo kwa watoto ambao waliondokewa na wazazi wao katika ajali ya *MV. Spice Islander*.

Mhe. Mwenyekiti, katika jibu la Mhe. Waziri kuna mambo mawili ambayo naomba nipate ufafanuzi zaidi. Mhe. Mwenyekiti, amejibu Serikali inaendelea kuwapatia huduma baadhi ya watoto hao. Swali langu Waziri angelikuwa wazi zaidi akatupa ufafanuzi ili tukajua Serikali imetekeleza vipi. Watoto waliofiliwa na wazazi wao ni wangapi na katika hao, baadhi ya hao aliosema wanaopata huduma ni wangapi na wanaokosa huduma ni wangapi. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, je, Serikali chini ya Ofisi hii imeridhika kuona baadhi ya watoto waliofiliwa na wazazi wao wanapata huduma na baadhi ya mayatima wamechiwa tu. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hilo siyo haki. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini jambo jengine ambalo linanishtua ni jibu la Mhe. Waziri katika ukurasa wa 21 mistari mitatu ya mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani majibu haya ya Serikali yanaweza kuwa ni dhahaka kwa wahanga wa ajali ile. Nilidhani Serikali kupitia Ofisi hii ingelichukua jukumu lake kwa kutafuta maslahi ya wananchi wake. Kwa kweli jibu hili la Mhe. Waziri linahuzunisha sana, linakumbusha kilio upya. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, watoto wameondokewa na wazazi wao. Leo Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inawaambia wakadai fidia kupitia taratibu za kisheria. Mhe. Mwenyekiti, watoto hawa mayatima wanajua nini, wana uwezo gani. Hivyo Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeshindwa kuwatetea mayatima hawa? Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha na inanimaliza nguvu, ninashindwa hata kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikae. (*Makofi*).

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mjumbe ambaye umemaliza sasa hivi. Sasa tunamkaribisha Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali na mtu wa mwisho niliyenaye ni Mhe. Ali Salum Haji.

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kutupa afya na kutupa pumzi hizi ambazo tulizosimama nazo na yeye ndiye ametupa nguvu hizo ambazo ametuwezesha kufika muda huu.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa dhiti kabisa kwa kunipa nafasi kwa kuweza kuchangia viongozi wetu, wpendwa wetu katika Kamati nzima pamoja kuanzia Waziri mpaka Kamati; kuanzia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, binadamu sote hatujakamilika na binadamu sote, kila mmoja binadamu ana kasoro zake. Mhe. Mwenyekiti, mimi niendeleo kuwapongeza viongozi wote watatu; Mhe. Rais wa Zanzibar, Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais kwa hekma zao, busara zao, usikivu wao kwa kuweza kutuunganisha na sisi sote humu ndani tukawa na kitu cha kupendana na tukafika pahala tukaweza kuiendesha Serikali yetu hii ya Mapinduzi chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kutoa ushauri kwa watendaji pamoja na Mawaziri. Mhe. Mwenyekiti, imani yangu utekelezaji wetu wote huu unaotekelezwa katika Baraza lako hili Tukufu la Wawakilishi, mambo yote haya yanakuwa yameshapita kwenye Baraza la Mapinduzi. Maana ukisema Baraza la Mapinduzi ni Mwenyekiti mwenyewe Rais wa Zanzibar, Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais na Mawaziri wote wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Hivyo Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba tatizo, tunasema kwamba *we have a problem and we have the solution*, baada ya *solution* tunasema *what's next*. Mhe. Mwenyekiti, mimi nashauri, hawa viongozi wetu wa kitaifa na viongozi hawa pamoja na sisi kazi yetu kubwa ni kutekeleza vilio vya wananchi na kwa jamii kwa ujumla.

Kitu ambacho kinachonisononesha Mhe. Mwenyekiti, viongozi wetu hawa wanapofanya ziara kwa maslahi ya wananchi ambayo ndiyo yaliyotufanya sisi tuwe humu Wawakilishi kwa niaba ya wananchi na Serikali ya pamoja, kwamba tatizo Mhe. Mwenyekiti, ninaloliona mimi na hasa katika Baraza zima la Wawakilishi na Wawakilishi wenzangu kwamba ahadi za viongozi wakuu wa kitaifa; kuanzia Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais, sijui kunakuwa na kigugumizi au kunakuwa na tatizo gani Mhe. Mwenyekiti, hayatekelezwi. Kama hayatekelezwi Wizara zinazohusika, Mawaziri wanaohusika, Makatibu Wakuu wanaohusika. Maana yake Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano kwa bahati nzuri tunaye Makamu wa Pili wa Rais ambaye ndiye Mwenyekiti wetu wa Baraza kwa upande wa Serikali ya Zanzibar Alhaji Balozzi Seif Iddi. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, tumeshuhudia kwenye bajeti sisi sote Wawakilishi kwa kupiga buti mpaka kuzuia zile bajeti kwa uchungu wa wananchi wetu, lakini anapokuja kuingilia kiongozi wa Serikali kwa kusema kwamba hili litatekelezwa.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, tunarejea tena humu na Mawaziri na Makatibu Wakuu wamesikia agizo hilo la Serikali, halafu hakuna utekelezaji. Sasa ina maana Mhe. Mwenyekiti, hizi ni njama makusudi zinafanywa na baadhi ya watendaji kuonekana viongozi wetu wa kitaifa hawana kauli au wanachokisema sicho. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi niseme kwamba wakati viongozi wanapotoa kauli zao na hasa kwenye Baraza hili ambalo umma mzima unasikia kuwepo na utaratibu maalum wa Mawaziri na Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na watendaji, waelewe kwamba hili Baraza limekuja hapa kwa niaba ya wananchi kushughulikia matatizo. (*Makofi*).

Sasa kama Makamu wa Rais ameshatoa ahadi, halafu kila mmoja anaona aah! acha tunyamaze. Tunakuja kwenye bajeti tena tunakumbusha vile vidonda.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na mazingira, kutokana na utamaduni wetu sisi wa Wazanzibari. Mimi Mhe. Mwenyekiti, inanipa tabu sana kwa watendaji hawa wahusika, kwa sababu kuna vitu vyengine vinakwenda kwenye Baraza la Mapinduzi. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa mfano jana Mwakilishi wa Matemwe alikuwa anachangia Wizara ya Elimu, alikuwa akisema hapa miaka miwili iliyopita Mhe. Rais wa Zanzibar alikwenda Jimbo la Matemwe pale Pwanimchangani.

Ninamnukuu Mwakilishi alisema hivi ambaye ninashukuru Mwenyezi Mungu kampa afya yupo mbele yangu hapa, alisema, "Rais aliahidi kwamba ikifika wakati wa 'kuzekwa' (kuezekwa); Mheshimiwa anajua Kiswahili changu cha Kihindi naomba unisamehe, kuzekwa". Kwa bahati Mwakilishi wa Jimbo la Matemwe anasema miaka miwili leo. Yule ni Rais. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa hawa watendaji ina maana kuna njama kumfanya kama Rais anapokwenda asionekane ile kauli yake, lakini siyo hayo, kuna mengi yanafanywa. Mimi nasema yanafanywa kwa makusudi. Sasa hatuwezi kuja tukawasimamia viongozi wetu wa kitaifa, tukawaacha watendaji na wahusika wenyewe na hili siyo moja yapo mambo mengi. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi niseme kwamba tufanyeni tathmini Wawakilishi kabla ya bajeti, kabla ya utekelezaji, tukae na viongozi tuseme bwana! Kulikuwa na moja, mbili, tatu vimefikiaje, lakini Rais ni Rais, ameshasema pale kama utekelezaji, basi wale wahusika wapo tena hili siyo eneo moja, kuna maeneo mengi kwa viongozi wetu wa kitaifa wamesema utekelezaji hakuna, tena wakati mwengine wanafanya kwa makusudi.

Sasa tusitake kulaumiana kwa sababu hii ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Mawaziri wote ni wetu, sisi tunawaheshimu na tunaendelea kuwa nao na ndiyo wanaoshiriki kwenye Baraza la Mapinduzi. Maana Baraza la Mapinduzi anashiriki Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais na Mawaziri wote wa Serikali wote wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Sasa unapofika wakati kuleta vitu ambavyo hivyo, ndivyo Mhe. Mwenyekiti, tunapofika hapa tunakuwa na uchungu na nchi. Mimi nimekuja hapa kuwatetea wananchi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hili tunakwenda kwenye bajeti asilimia 80 ya ahadi waliotoa viongozi wa kitaifa hazijatekelezwa, na unapeleka barua hakuna mmoja anayejali. Siku nyengine ni njama. (*Makofi*).

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachoomba kutumia hekma na busara, tuwe wasikivu, tukaeni tuone jinsi gani, kama hii hali hairuhusu tusemeni jamani sisi hohe hahe, Serikali ndiyo hiyo ilikuwepo. Tupate pesa tutengenze lakini kwa kukaa kimya unaandikiwa barua hakuna mmoja anayejali, kila mtu anasema yeye mbabe kateuliwa tu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ninachoomba wengi tupo wasikivu Wawakilishi, tuitane tukaeni, lakini mtu akishatoa barua, kuna ubadhirifu mkubwa kwenye Wizara mbali mbali kwa ushahidi. Ninaamini kama ingelikuwa kuna mambo leo Serikali yetu isingelikuwa kuyaondosha matatizo ya afya, elimu, barabara za ndani, lakini Mhe. Mwenyekiti, vitu vinakwenda vinaamuliwa; yaani huko mbele kuna mambo mengi yanafanyika.

Hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri viongozi wetu wawe makini katika hali hii. Maana yake hii ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kilichokuwemo humu inatekelezwa ilani ya Chama cha Mapinduzi. Sasa lazima tusimame tuone utaratibu mzima, lakini tunaingia kwenye bajeti kesho kutwa na ninakuhakikishia Mhe. Mwenyekiti, hapa patakuwa hapatoshi kwa sababu sote humu tumechaguliwa.

Kwa hivyo hiyo ningeliomba watendaji na Mawaziri husika kwa kila mmoja aliyechukua jukumu la viongozi wa kitaifa waliotoa ahadi twambieni, jamani hee! sisi hohe hahe Waziri wa Fedha hakuwa na fedha za kutosha. Maana yake Waziri wa Fedha atapokuja utamuonea tu lakini anakusanya zile alizokuwa nazo, lakini ukimpa Mwakilishi, ukiita jamani hili tunalifanya hili, hili tunakaa tunafanya hivi, lakini hakuna kabisa kitu kama hichi. (*Makofi*).

Mimi Mhe. Mwenyekiti, nilimwendea Waziri mmoja, *wallahi* nilizungumzia naye kuhusu suala la ahadi *wallahi billahi tallahi* na mimi ni muislamu, nilimwambia basi nitakuletea barua, akaniambia sikujibu wala sina habari na wewe, *Wallahi laadhimu* na ahadi imetolewa na viongozi humu ndani. (*Makofi*).

Sasa Mhe. Mwenyekiti, *what's next*. Mimi nimekuja hapa kwa niaba ya wananchi, *we are all in transit*, tuningana na pumzi za Mwenyezi Mungu. Hapa tunazungumza siku nyengine Mohammedraza mimi nikitoka nje tu nitatangulia mbele ya haki, *we are all in transit*, huo ndiyo ukweli. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini tusikilimbie kwenda kusali tu, tusikilimbie kwenda kufunga, tusikimbilie kwenda kutoa zakka. Tukimbilie kwa Mwenyezi Mungu tukawahudumie wananchi, ndiyo kazi ya Serikali kutatua matatizo ya wananchi, wananchi wana shida, lakini itakuwa umimi, mimi mbabe mpaka mtu ule mwendo anabadilisha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana kwamba sote ni ndugu, sote tunaheshimiwa, na sote ni watu wamoja, ndio maana leo *Alhamdulillah* tumekaa tunapanga. Mhe. Mwenyekiti, hili nilikuwa niombe ushauri.

Mhe. Mwenyekiti, nimeshazoea viriri ndio maana sauti yangu iko hivi, sizungumzi kwa jazba lakini ndio nilivyo mimi Raza.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la vitega uchumi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Una dakika tano Mhe. Raza za ziada.

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Ahsante. Wizara ya vitega uchumi ni lazima tuwe makini, kwa sababu tumeshuhudia tuliipa vitega uchumi Kampuni ya nje ya Italia pale *Venta Club*, kwa bahati mbaya au nzuri yule mwekezaji kafanya biashara kapata pesa na kachukua kila kitu, matokeo yake alipoona keshakusanya pesa kaacha deni kwa wakulima wetu wauza mboga mboga, walikuwa wanadai shilingi milioni 400.

Mhe. Mwenyekiti, pesa za serikali karibu bilioni 2 hakulipa, na huo uko ushahidi milioni 400 za wananchi hajatumia, matokeo yake serikali inabeba mzigo. Sasa mimi nawaomba wahusika tuwe makini sana katika kuwatizama watega uchumi na hao wanaotaka kuja kuleta vitega uchumi, tuwe makini kuona *CV's* zao na uwezo wao.

Mhe. Mwenyekiti, la tatu ni suala la Shirika la Meli. Wakala wa Shirika la Meli Kampuni ya Filtext ya Dubai. Mhe. Mwenyekiti, nataka kuliambia Baraza la Wawakilishi kwamba pesa zilizokuwa zimetafunwa ni nyingi sana, ni mabilioni. Ndio maana ripoti iliposomwa hapa na dada yangu Mhe. Shadya ilishindwa kutoa taarifa.

Kwa kweli lilitengenezwa buku la pili *duplicate* na mapesa haya mabilioni, tumekuja kugutuka mwisho kabisa kwamba pesa zile hazikuingia kulikuwa na risiti ya pesa. Kwa sababu hili suala nalielewa, ndio maana Mhe. Shadya aliposoma ripoti yake kamati ilikuwa inapata kigugumizi kwamba haitoi ile *fact* yenyewe.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi ningepomba kwamba jamani hii Zanzibar ni yetu na sote ni watu ambao tumekuja kuwatumikia wananchi, na serikali yetu ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ni serikali ambayo haina ubaguzi. Ninalotaka kuliambia Baraza hili ni kwamba tuje hapa tufanye mazuri ili Mwenyezi Mungu akitujaalia, hivi sasa hivi tunateremka kilima, hatupandi kilima, basi tukumbukwe tuliokuwa tumefanya kazi ili na wenzetu tuwakumbushe siku vitu ambavyo binadamu vinawapitikia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono kwa asilimia zaidi ya mia moja kwa viongozi hawa, Mwenyezi Mungu awape afya njema pamoja na sisi Wawakilishi na wananchi kwa kuwatumikia wananchi wa Unguja na Pemba, bila kujali rangi, kabila wala dini. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa dhati kwa kunipa fursa hii, kuweza kuchangia maelezo ya utekelezaji wa maagizo na ushauri wa kamati kwa wizara tatu hizi. Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

**Mhe. Mwenyekiti:** Una Mhe. Mjumbe hiyo spika iweke vizuri ili maelekezo yako yaingie kwenye *Hansard*.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante Mwenyekiti. Nasema nikushukuru kwa dhati kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia. Nimuombe Mwenyezi Mungu anipe nguvu niweze kuchangia kwa hekima na busara na niondokane na jazba katika uchangiaji wangu, kwa dhamira moja tu ya kuweza kusaidia taarifa za kamati hizi katika utekelezaji wa majukumu yao katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, michango yangu ni mifupi sana na nitajitahidi ku-*save* muda ili na wenzangu waweze kupata nafasi. Katika Ofisi ya Rais Mhe. Mwenyekiti, karatasi namba 5, kuna suala la mimomonyoko ya ardhi katika majengo ya Ikulu Mkoani na maeneo ya Bwefumu ambayo yanatokana na maji ya chumvi.

Ushauri wa Kamati uliotolewa na wizara wameeleza namna walivyoiona ile hali na namna ambavyo wamejiandaa. Sasa wamesema kwamba jambo hili wanategemea kulipeleka katika bajeti inayokuja na wamekisia kwamba ujenzi wote utagharimu karibu bilioni 1,008,370,000. Sasa pamoja na kwamba ushauri huu umepokelewa, mimi ningewaomba kwa dhati kabisa pamoja na kwamba tunasubiri bajeti itakayokuja, lakini tunafahamu kwamba bajeti yetu sisi inakuwa ni changa na mambo mengi, tunaweza tukaja kufika mwaka uwezo ukawa haujapatikana taarifa hii ikaja tena ndio tukaambiwa yale yale, mwaka jana imekuja na mwaka huu inakuja. Lakini uwezo kumbe mdogo.

Kwa hivyo, watafute njia mbadala kwa sababu unapoacha suala hili athari zake zitakuwa ni kubwa. Bajeti ambayo tumeletewa leo, basi baada ya muda mchache itakuwa inaongezeka maradufu kutokana na athari, kwa sababu bahari haiondoki na mawimbi yanaendelea kuwepo. Sasa ningeeomba kwa busara kabisa kutafuta njia mbadala ili kuweza kuziokoa nyumba hizi, ili zikija kufika pahala zikashindikana katika masuala ya majenzi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuna jambo nimeliona katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, liko katika ukurasa wa 10 kwenye utangulizi, kwenye suala zima la maji safi na salama. Mhe. Mwenyekiti, tumeambiwa hapa kwamba serikali ina dhamira kwa upande wa mjini, kuweza kulifanya suala la maji safi na salama kuwafikia wananchi kutoka asilimia 75 mpaka 95. Jambo hili Mhe. Mwenyekiti, mimi huwa nalipigia kelele sana, kwamba inawezekana tunayoambiwa na yanayotendeka ni tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, asilimia 75 kwa upatikanaji wa maji safi na salama kwa mjini ni asilimia kubwa, lakini kinadharia ukiangalia maeneo mengi sana suala la maji limekuwa ni tatizo. Kila ukiuliza sababu zinakuwa ni za kila namna. Kwa hivyo, ningeeomba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ikajaribu kuiangalia Mamlaka ya Maji, mimi nina mashaka na Mamlaka ya Maji namna watendaji wanavyoratibu shughuli zao.

Kwa nini nasema hivyo Mhe. Mwenyekiti. Sina kumbukumbu ya tarehe, lakini karibu tu hapa niliuliza swali la ukosefu wa maji katika Shehia ya Kwaalimsha, na Mhe. Waziri katika majibu yake akaniambia basi suala amelipokea na atalifuatilia, lakini Mhe. Mwenyekiti cha kushangaza na cha kusikitisha na ndio vitu vinavyotupa mashaka tukaonekana labda serikali hii haifanyi kazi zake, lakini kumbe kuna watu wanatutafuna kama mchwa ndani ya nyumba yetu. Sasa unaishi unajiona uko salama, mtu anakula matokeo yake jengo mpaka linafika kuanguka hujui nini kinachoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuuliza swali lile saa 4:25, saa 6:40 maji katika Shehia niliyoitaja hapa yameanza kutoka kwa wingi na watu wameshangaa vya kutosha. Sizungumzi hili Mhe. Mwenyekiti kama nazungumza kisiasa. Mimi ni Muislamu nazungumza ya udhati na ninayozungumza basi Mwenyezi Mungu atakwenda kunihukumu mbele ya haki, lakini huo ndio ukweli uliotokea.

Mhe. Mwenyekiti, nikaja nikamuuliza Mhe. Waziri. kuna nini? Nilikuuliza swali ukanijibu kwamba mimi na wewe tutalifuatilia kwa pamoja ili kulipatia ufumbuzi, hata saa 6:40 maji yakaanza kutoka. Mhe. Mwenyekiti, hii ndio athari ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nazungumza hili makusudi wala sina dhamira mbaya, lakini mara nyingi mnapoungana katika serikali, mmoja anataka afanikiwe lakini mmoja anatafuta njia za kuharibu kwa makusudi, ili serikali ionekane haifanyi kazi halafu baadaye tuje hapa tupewe lawama.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo na serikali hii ambayo inaongozwa na Chama cha Mapinduzi yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa. Kwa kweli nawashukuru mawaziri wote wanajitahidi kadiri ya uwezo wao kwa upande wa CCM na upande wa CUF, lakini nasema kuna mambo watendaji wanayafanya katika hali isiyostahiki na kuharibu mustakabali mzima wa serikali hii, lakini Mwenyezi Mungu *Inshaallah* atasimama na serikali ya CCM na kuweza kupata ushindi mwaka 2015. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mengi nimeangalia na nimeridhika kabisa na jitihada za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, jitihada za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na jitihada za Ofisi ya Rais, nawaomba wajitahidi kadiri ya uwezo wao katika kutekeleza majukumu yao, Mwenyezi Mungu atawalipa kutokana na matendo yao, hawalipi kwa dhana au na dhamira nyengine.



Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie kabisa, kwa sababu nasema nimeridhika na taarifa na namna majibu ya wizara yalivyokuja, lakini nataka nimalizie kabisa Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko sana.

Mhe. Mwenyekiti, sipendi na mara nyingi huwa simtaji mtu, lakini kauli aliyoizungumza Mjumbe mwenzangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu, mimi huwa namuomba sana unapotengeneza maelezo basi usitizame upande mmoja, kama tumekosea useme upande huu umekosea na upande huu umekosea. Kama sote jahazi hili moja tulilolingia la Serikali ya Umoja wa Kitaifa tunakwenda sawa, basi tuseme sote tunakwenda sawa, lakini jahazi hili sio vyema kusema kwamba sijui muongoza usukani anakwenda sawa na aliyekamata tanga anakwenda sivyo, sio vyema kabisa Mhe. Mwenyekiti. Kwa nini nikasema hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilifikiri alipokuwa akimtaja Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mtendaji mkuu wa serikali, nilifikiria Mhe. Ismail Jussa pia angemzungumza Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, nilikuwa na imani hiyo kabisa. Kwa nini niseme hivyo Mhe. Mwenyekiti, nasema kwa ushahidi na Mhe. Waziri akija atakuja kusema hapa kuwa ninayozungumza yana ukweli au hayana ukweli. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, hebu tujiulize huko nyuma, UKIMWI ulikuwa asilimia ngapi na sasa hivi UKIMWI uko asilimia ngapi na unasimamiwa na wizara gani. Pili, tuangalie athari za kimazingira huko nyuma tunakotoka na athari za kimazingira sasa hivi, lakini pia tuangalie suala la ongezeko la madawa ya kulevywa huko nyuma na sasa hivi. Sasa nilifikiria angesema na huyu pia ameshindwa kusimamia masuala haya na anapaswa ajiuzulu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ndio binadamu unaweza kuzaa watoto wawili, mmoja ukampenda sana na mmoja ukampenda kidogo.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hotuba yote. (*Makofi*)

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo kuchangia taarifa hii au ripoti hii ya kamati ya Viongozi Wakuu, inayoongozwa na Mheshimiwa Alhaji mtarajiwa Mhe. Hamza Hassan Juma. Vile vile kuchangia taarifa za utekelezaji za mawaziri husika wa kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli nokoa ni mkali kuliko mwenye mali na sababu ya kuwa nokoa ni mkali kuliko mwenye mali ni kwamba analinda ugali wake asiye akafukuzwa, kwa sababu nazi au ndizi au shamba limeibiwa, kwa sababu mwenye mali akijua kwamba nokoa yupo halafu nazi zimeibiwa atafukuzwa kazi tu nokoa. Kwa hivyo, ni haki ya nokoa kuwa mkali kuliko mwenye mali. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, tuko hapa kuchangia taarifa hizi tatu, lakini jambo ambalo linanisikitisha sana tena sana ni kuona hakuna *seriousness* ya serikali katika utekelezaji wa karibu shughuli zote. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kamati hii inaongozwa na Mhe. Hamza Hassan Juma ina wajumbe saba, katika wajumbe hao saba wanne wanatoka CCM na watatu wanatoka *CUF*. Nafikiri ndio maana hata katika uchaguzi Mhe. Hamza Hassan Juma akaibuka kuwa Mwenyekiti. Sasa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ismail Jussa Ladhu kasema mengi hapa, mimi katika kuungana naye, hapa hatuchangii masuala haya kisiasa. Kwa sababu Mhe. Hamza Hassan Juma ni *system man*, taarifa hizi zote tatu mwaka 2012/2013, 2013/2014, na 2014/2015 ni hayo kwa hayo.

Sasa Mhe. Hamza Hassan Juma kama Mwenyekiti na kamati yake anaporudia mambo ya mwaka jana na mwaka huu, ni kwamba hakuridhika. Hizi ni ripoti zenyewe na kama aliridhika na kamati yake asingeyarudia yale kwa yale. Kwa hivyo, hili mimi nataka niliweke *very clear*, ripoti hizi tatu za kamati ya Mhe. Hamza Hassan Juma ni hayo kwa hayo maji ya futi na nyayo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais ina idara na taasisi 15, sitaki kuzitaja. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ina idara na taasisi 8, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ina idara na taasisi 11. Kila taasisi ilete mtu mmoja tu wa ofisi hizi tatu, basi tungekuwa na maofisa 34. Hebu angalia kule juu wako wangapi, Msikitini? Kusali nini Isha. Angalau hamna hamna basi kungekuwa na watu 34 kule, tangu asubuhi ripoti hii ilipokuwa inawasilishwa. Hivi kweli haya yanayozungumzwa hapa yote ndio anayaandika Makamu wa Pili wa Rais, sio kweli.

Mhe. Haji Omar Kheri wale walioko hata ukiwapungia hawaongezeki. Mimi nimeshawahesabu wale, naendelea.

Jengine kama hili maofisa wamekimbia hakuna taarifa, basi hata mawaziri. Leo asubuhi hapa waziri mmoja huyo kasoma taarifa za mawaziri wawili na zote hizo sio wizara zake. Hivyo, kuna *seriousness* hapa? Tunakuja hapa Barazani na ndio hivyo kama unavyoona, lakini kuliko yote hayo suala zima la uratibu wa shughuli za serikali Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe, hebu angalieni vizuri, haliko kwa Rais wala Makamu wa Kwanza wa Rais, liko kwa Makamu wa Pili wa Rais, uratibu wa shughuli zote za serikali.

Kwa hivyo, anapozungumza UKIMWI umeongezeka, mazingira sijui yameharibika, sijui madawa ya kulevya yamefanyaje. Mratibu mkuu wa shughuli za serikali nakwambieni tena ni Makamu wa Pili wa Rais, hili halimvuki, hawezi kulivua. Na sisi hatuwezi kumvua kwa sababu ni kwa mujibu wa Katiba. Kwa hivyo, ni vizuri sana tunaposema hapa tuwe makini katika kusema.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika Ofisi ya Rais yako maagizo 41, hii hapa *paper* ya Mhe. Mwinyihaji, amejibu ya jumla 10, hii hapa. Tena yeye kaweka rangi hasa ile nembo yetu ya SMZ hakutoa kopi kumi tu. *Serial number 1 to 10* agizo namba 1 mpaka 10 utekelezaji wake hayo ni ya jumla, lakini maagizo ya kamati hii ya Mheshimiwa Hamza Hassan Juma ni 41, *ten over forty* ni *percentage* gani huo ndio utekelezaji wake *twenty five percent* (F) kama unafanya kwa mwalimu wa skuli 10 juu ya 40 ni 25, ni (f) bwana.

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, maagizo yake kumi na saba amejibu tisa kwa ujumla ni kwamba zipo hizi taarifa sio kwamba anasoma zangu mimi aa, tisa juu ya kumi na saba ni ngapi asilimia hamsini na tano asilimia, sijui ni (B) au ni ngapi, ni (C) inategemea Chuo lakini mwengine hata *sixty* ni (C) mwengine *sixty* ni (B) na hapa ndio panapotuathiri kisiasa.

Mhe. Mohammed Aboud kabrasha hilo lina *page* 34, yeye amejibu katika 43 nasema amejibu 36 na taarifa hii Mheshimiwa ukiisoma kwa sababu kuna suala la ukubwa wa kabrasha na kilichomo ndani, ukifungua *page* tisa zinasoma hivi nakuonesheni tu ile test iliyomo ndani ya kabrasha hili, mkisoma lote ndio mtajua yaliyomo.

Kwa upande wa Skuli za Sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita nazo zimeongezeka kutoka 194 mwaka 2010 hadi skuli 210 mwaka 2014, kwa wanaojua Kiswahili vizuri mimi Kiswahili nilipata (A) Hivyo kweli tuna skuli 194 mpaka *Form six* nakuulizeni nyinyi.

Mhe. Zahra Ali Hamad tunazo kidato cha kwanza mpaka cha sita skuli 194?. Sasa kama huu si uongo ni nini, lazima tuwe makini, hizi taarifa hatukuja hapa kupotoshana skuli ambazo zina mpaka *Form Six* hazifiki hata 40 na za *private* zake. Leo unasema una skuli mia mbili na *Form one to Form Six* maana yake nini, na nyote hapa mmeshalewa na pengine mtu angeulizwa angesema hivyo. Mhe. Jaku ee tuna skuli 210 hivi hivi, si kweli, hakuna *Form six* 210 si *printing error*, hii imefanyiwa *proof reading*.

Na hapa huwezi kabisa ukatwambia kitu hichi, na kama kuna makosa tuambiwe mapema kwamba kuna makosa, tuambiwe mapema kwamba kurasa fulani imekosewa ndiyo utaratibu wetu. Miswada inachapishwa Kamati zinakaa zinasema, kwa hivyo nasema taarifa hii ni ya Makamu wa Pili wa Rais ina maofisa Idara tu 11, na Waziri huwa haandiki hizi, Waziri anaandikiwa anakuja kusoma anaweka nyama tu kidogo kwenye taarifa yake, kama hamna siasa akaingiza siasa kwa sababu watendaji siasa hawaingizi ndiyo uzoefu ulivyo.

Kwa hivyo Mheshimiwa mimi bado nasema kwamba Baraza hili taarifa hizi ambazo tunazileta hapa ni za Serikali nzima, na tuisahau waheshimiwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa suala la *opposition* halipo, ni *front benchers* ambao ni Mawaziri, na *backbenchers*, na sisi kazi yetu ni kuwasimamia hawa. Sasa nyinyi mnataka iwe kama kundi la ng'ombe aliyekuwepo mbele ndio anasimama kula majani lakini anapigwa aliyekuwepo nyuma, hapigwi aliye mbele ndiye aliyesababisha wengine huku nyuma wasimame.

Kwa hivyo sisi wajibu wetu kama *backbenchers* Waheshimiwa ni kuhakikisha kwamba tunaisimamia Serikali, tena tunaisimamia kweli kweli na ndio maana tunakaa hapa tunasema haya, kama hakuna suala kwamba ni Serikali ya umoja wa kitaifa kama ina maana kama haina maana, Serikali ipo, ipo kikatiba na itaendelea kuwepo mpaka siku ya hukumu *inshaallah*. Maamuzi haya ni Katiba na wamefanya haya Wazanzibari, kama kuna makosa ndio haya tunayasema yarekebishwe, na makosa yapo si ndio hayo tunayozungumza sote ni wanagenzi hapa katika Serikali ya Umoja wa kitaifa, tumezoea Serikali ya Chama kimoja miaka 49, hii 2010 mpaka 2014/15 leo ni miaka mitano tumeingia na hata Serikali ya Chama kimoja mwanzo mwanzo ilikuwa inasuasua.

Kwa hivyo Serikali ya Umoja wa Kitaifa Mheshimiwa ipo kikatiba na itaendelea kuwepo na naamini *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu Oktoba mwaka huu, baada ya uchaguzi mkuu CUF itashinda Urais, Rais atakuwa kutoka CUF, hapo mtajua tofauti ya Serikali hii ambayo Rais ni wa CCM na Serikali ambayo Rais wa Umoja wa Kitaifa atakuwa CUF *inshaallah*.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

**Mhe. Abdalla Mohammed Ali:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru magharibi haya kupata fursa ya kusema machache katika maoni haya ya Wajumbe wenzangu na majibu ya Serikali. Mimi nataka kidogo niwakumbushe tu wenzangu kwamba katika Marais ulimwenguni walioongoza na kupata umaarufu na heshima kwa nchi yao ni Winston Churchill ambaye ameiongoza Uingereza wakati wa vita kuu ya dunia mwaka 1940 hadi 1945. Na akaiongoza tena Uingereza mwaka 1951 mpaka 1955.

Nawaomba watambue tu katika viongozi waliopata umaarufu ni Winston Churchill na kiongozi huyu alitunukiwa uraia wa nchi moja kubwa ulimwenguni ya Marekani, kwa hivyo yeye alikuwa ni raia wa kuzaliwa wa Uingereza na Raia wa kutunukiwa wa Marekani kutokana na ile juhudi yake aliyioifanya na kuiongoza nchi ile, yeye hakutawala yeye aliongoza.

Na Rais huyu kama alivyokuwa mwanzisishi wa Taifa hili alivyotuwekea maneno ya hekima na yeye pia aliweka maneno ya hekima katika nchi yake, naomba ninukuu kwa sababu alijifunza historia ya nchi yake yeye alisema kwamba "*criticism may not be agreeable but it's necessary*". Kwamba kukosoa inawezekana pengine isikubalike lakini ni jambo la lazima, sasa na sisi kama ni Wajumbe ni lazima tutakapona kwamba pana kasoro tunatakiwa tuseme, watakaokubali sawa wasiokubali sawa, lakini ni lazima tuseme.

Mhe. Mwenyekiti, kama walivyosema wenzangu kwamba ripoti hizi ni mwendelezo tu na maneno tu ubadilishaji wa miaka iliyopita, na utekelezaji wake ni ule ule bado tuko njiani na mengineo. Mimi nataka nigusie maeneo mawili tu leo Mhe. Mwenyekiti, na eneo la kwanza ninalotaka kuligusia ni kuhusu idara ya ushirikiano wa kimataifa na uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nchi za nje kwa jina jengine tunawaita (*DIASPORA*).

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeona na imeshauri kwamba hili lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa, kwa kauli hii lililokusudiwa mimi natafsiri kwamba Idara hii haijafanya shughuli yoyote kwa sababu lengo lililokusudiwa halijafikiwa, kwa maana hiyo hivyo kuna haja sasa ya Idara hii kuwepo.

Tokea mwaka 2011/12/13 maneno ni haya haya Idara inaendelea, idara inataka fedha ni hawa Wazanzibari wangapi mpaka sasa wameshajitokeza kusema kwamba sisi tunataka kuja Zanzibar turudi, au tunataka kuja kuwekeza katika mradi fulani hata sisi tuendele tena Idara hii kuwa tuiipatie fedha iende nchi za nje ikawashawishi Wazanzibari waje hapa, miaka minne mfululizo hatujaona matunda yoyote.

Ni wangapi ambao labda wameshafikia lengo hatuoni kwamba kuingiza fedha itakuwa ni ubadhirifu wa kuingiza fedha katika idara ambayo labda uratibu wake sisi tuna mabalozi nchi nyingi, kwa nini kazi hii isifanywe na wao iwe leo hapa tena tuingize fedha tununue magari wakati watu wapate kutembelea na kwenda na shughuli zao wakati shughuli inataka kufanyika Muscat, shughuli yenyewe ya kuratibu inataka kufanyika Uingereza ndiko waliko Wazanzibari sasa kule kuna mabalozi wetu, sasa kuna haja kweli ya kuendelea idara hii kusema kwamba tuiipatie fedha, wakati miaka mitano yote iliyopita sijaona faida yoyote iliyofanywa na Idara hii. Nafikiri Mhe. Mwenyekiti, ipo haja sasa ya Serikali kuona kwamba hizi shughuli nyengine zilizowekwa kama hazitekelezeki basi ziondoshwe.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kidogo kwenye Ofisi ya Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Serikali, kamati hapa imesema kwamba inataka Afisi ya CAG kuileta ripoti kuhusu mishahara hewa ambapo Baraza la Wawakilishi liliagiza uchunguzi wake ufanyike ili kuona upotevu wa fedha za umma, sasa hapa wajumbe wengine ndio walipojenga hoja hii Serikali inafanya shughuli gani kazi yake ni nini. Kwamba leo tumeunda ofisi inayoshughulikia masuala haya tupeleke kamati ikaiombe, hebu Mdhhibiti na Mkaguzi tulettee ripoti pana Serikali, hapo kweli pana utendaji hapo kweli, na sio hilo tu tena inasema Kamati afisi ya CAG pia itoe ripoti kuhusu fedha zilizokusanywa na kampuni ya Filtex ya Dubai ambayo ilikuwa ni Wakala wa Shirika la Meli.

Mhe. Spika, hii ni kazi ya *CAG* aliyopewa kisheria, lakini leo mpaka kamati iende ikamwambie tulettee ripoti hii pana utendaji hapo kweli, Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba yale maneno yaliyotangulia kusema kwamba Serikali iwajibike katika masuala haya basi iwajibike, kama kunahitajika ripoti ije hapa Serikalini kwa nini haiji.

Sasa anatokea mjumbe anasema anavyotaka yeye haiwezekani, sisi tunakosoa kwa sababu ya kujenga, tunaeleza ili tusikilizwe na tufahamiane, hatusemi hapa kwa sababu ya kwamba mimi nataka niseme tunataka tujenge tuone Taifa linakwenda mbele. Leo *CAG* anashindwa kuleta ripoti na yeye ndio anayeshughulikia ripoti zote za matumizi ya fedha za nchi hii, sasa nani mwengine alete hapa. Tukiwaambia kwamba Serikali imeshindwa mnatafuta mawaziri wengine nje kujibu masuala Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na kwa kweli nitatoa mchango mdogo sana kwa sababu sioni cha kukisema kwa sababu ni yayo kwa yayo.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilishiriki kwenye semina ya kimataifa Dar es Salaam kuhusu wahasibu wakuu wa nchi za Afrika. Mwalimu mmoja wa semina ile alisema kwamba matatizo ya nchi za Afrika ya wizi wa mali za umma, utendaji mbovu wa Serikali mashaka yote haya ni matatizo ya Wabunge. Kwamba unapokuwa na Bunge dhaifu lazima utakuwa na Serikali dhaifu na huu ndio ushahidi kwamba unamwambia Waziri awajibike kwa mujibu wa Katiba matokezo Mwakilishi mwenye watu elfu 20 wewe ndio anakujibu, ni udhaifu.

Jeuri ya Serikali yoyote duniani Mheshimiwa Mwenyekiti, huondoka ikiwa bunge la nchi hiyo ni bunge makini, leo humu kila mtu anataka uwaziri. Rais ametuua Mawaziri 16 na kuna wengine 20 wa ziada.

Mhe. Mwenyekiti, sisi Wawakilishi na tume yako ni wajibu wetu kuisema Serikali waacheni Mawaziri wajibu hoja za Wawakilishi kwenda kwa wananchi, sasa kama wewe umekuwa Waziri usiye mshahara si mashaka hayo?

Mhe. Mwenyekiti bunge dhaifu huzaa Serikali dhaifu, kwa hivyo tuwalaumu Mawaziri lakini sababu kubwa ya msingi ni Wawakilishi wenyewe ni tatizo, tukichambuana hapa humu ndani wawakilishi wana dili, yeye ndio dalali wa kiwanja, yeye ndio dalali wa nyumba yeye ndio dalali wa kila kitu. Msifanye tukasema mambo ambayo tunayajua.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niombe kiti chako sasa kielekeze Wawakilishi kwamba Mawaziri watujibu hoja zetu, na kama mtu anaona kwamba Waziri fulani hafai basi amwambie Rais nipe mimi nafasi, ikiwa kuna mtu anaona Waziri fulani hawezi kujibu hoja basi na aombe yeye aende kule mbele akajibu hoja. Haipendezi, wananchi wanashangaa nani Waziri, nani *backbencher* nani Mwakilishi, mashaka tu.

Niseme kwamba mimi ripoti hizi na tumekuwa tukihoji hii Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais si kwa sababu ya kumchukia. Wawakilishi wote wanaamini mimi nakaa shamba naamini, Mhe. Jussa anakaa mjini anaamini kwamba haya hayafanyi yeye *totally*, lakini ndio kiongozi wa Serikali.

Sisi kazi yetu ni kumuelekeza na kumkumbusha kwamba watendaji wako wanafanya hivi si kwamba na yeye ndio anafanya haya, yeye siye anayefagia Manispaa, yeye siye anayelinda kule Uwanja wa ndege, lakini yeye ndiye muwajibikaji wa Serikali ndani ya Baraza hili, wengine hatuwaelewi.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ripoti hizi kwa kweli zinatia aibu na mimi nataka niseme maneno mafupi sana hata wenyewe wamekiri ukurasa wa tatu Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwamba miongoni mwa changamoto za Serikali hii ya utendaji wa Serikali ni uwajibikaji, utii na nidhamu, kwamba hapana, sikuandika mimi, mimi nakaa Pemba kule Mwambe wameandika wenyewe kwamba miongoni mwa changamoto za Serikali hii ni uwajibikaji, utii na nidhamu ndogo. Sasa mwengine anajibu kwamba hapana. Ikiwa yeye mwenyewe anasema kwamba mambo haya ni changamoto, anatokezea Mwakilishi anasema hapana. Mimi naitwa Hija, aah wewe si Hija, si ugonjwa huo.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya pili ambayo nataka nichangie ni suala la ukurasa wa tano, kwamba sasa serikali imetangaza kwamba wametiliana mkataba na kampuni ya *CHEC* juu ya ujenzi wa bandari ya Maruhubi. Basi watwambie serikali bandari hii itaanza lini. Mimi nina wasiwasi ni yale yale ya tamaa ya fisi, fisi anatembea mkono katika, watu wanafata nyuma tu. Kwa hiyo basi Mratibu wa serikali, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, mtwambie basi angalau serikali itajenga lini. Wasiwasi wangu ni kwamba haya ni yale yale ya tamaa kwamba watu waonekane kwamba mambo yanakwenda na Oktoba uchaguzi.

Nasoma ripoti ya Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa sikuandika mimi haya.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri, tunaomba uzungumze na kiti huku. Mhe. Mjumbe aendelee na taratibu zake kuchangia ripoti inayohusiana na Viongozi Wakuu wa Serikali.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, naomba niinukuu hii ripoti ukurasa wa 5.

"Mhe. Spika, ni katika kuimarisha miundombinu muhimu ya usafiri na usafirishaji, serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo imeimarisha miundombinu ya barabara mjini na vijijini. Upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari mpya ya Mpiga duri umekamilika na serikali imetia saini ya makubaliano ya ujenzi wa bandari hiyo na Kampuni ya China yaani *China Harbour Engineering Company (CHEC)*"

Mheshimiwa sikuandika mimi haya. Hoja yangu ni kwamba tungewaambia kwamba basi ujenzi baada ya kutia saini utaanza lini? Hiyo hoja yangu ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya tatu, na hii bahati nzuri ni ripoti ya Waziri ndio naambiwa Mheshimiwa kanikumbusha. Maana kamati ndio wale watu saba, Kwamtipura, Makunduchi, Kiwani, lakini hii ya Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 8, kuna suala zima la kukabiliana na matatizo ya elimu. Kwamba serikali imejitahidi kuongeza walimu, maabara na vitabu vya kusomea, lakini Mhe. Mwenyekiti, serikali wanashindwa kutwambia kwamba hadi hii leo madarasa ambayo yameanzishwa kwa mujibu wa Sera ya Elimu hayana walimu wala vitabu.

Leo kuna darasa la tano ambao wanasomeshwa Kiingereza hakuna mwalimu wala kitabu. Serikali haiyazungumzi hayo, wanaandika kwamba tayari wamefikia hatua nzuri ya kuongeza vitabu, maabara na walimu, lakini hawatwambii hadi leo madarasa kwamba hakuna mwalimu wala kitabu halafu tunategemea kwamba mwanafunzi apasi kwa kiwango ambacho ni cha kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 11 wa ripoti ya Waziri ni suala zima la Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Mhe. Waziri amesema hapa kwamba Utumishi wa Umma umekuwa sana baada ya kurudishwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Mimi kwa maoni yangu Utumishi wa Umma chini ya Kamisheni hii umeporomoka sana. Ushahidi wa hayo Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kabla ya Kamisheni hii watumishi wangapi wataalamu wamekimbia nchi, na baada ya Kamisheni hii watumishi wangapi wataalamu wamekimbia nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kila Idara serikalini imekuwa ina migogoro ya maslahi ya watumishi, chini ya Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Hayo Kamati zinashuhudia, sio Baraza la Wawakilishi, sio Mahakamani sio Serikalini. Kwamba Utumishi wa Umma sasa Maafisa na Makamishna ndio wamekuwa Mungu mtu, wanaamua vile ambavyo wanaona ni sawa kuamua.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani hili suala serikali chini ya Makamu wa Pili wa Rais waliangalie kwa ufanisi mkubwa ili kuleta maslahi ya wafanyakazi wetu ndani ya serikali ili usawa wa wafanyakazi waweze kuzingatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 14 kuhusu uwajibikaji wa serikali juu ya Kamati Teule na Kamati za Baraza la Wawakilishi. Mimi hapa majibu ya serikali hapa nayakataa sio sahihi, kwamba eti kwamba kila penye serikali, Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi, serikali imechukua hatua kwa ukamilifu wake.

Mhe. Mwenyekiti, wale wote waliochukuliwa hatua au wengi ni watu ambao ni wadogo sana ambao kwa kweli wengine ni kwa njia ya kuzuga tu Wawakilishi. Lakini wapo watumishi ambao walichukuliwa hatua kwa mkono wa kushoto, mkono wa kulia wakarejeshwa, ndio ile *mumechukua, mumeweka, waa*. Wapo watumishi ambao wamechukuliwa hatua lakini hatimaye serikali hii hii ikaamua kuwarejesha kwa mkono wa kushoto. Yale maeneo ambayo Kamati Teule zimeelekeza maelezo mazito kwa maslahi ya nchi hakuna hatua zilizo chukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kama hayo sio kweli na watwambie basi waliofanya uharibifu ujenzi wa jengo la Wizara ya Fedha ya Pemba waliochukuliwa hatua ni wangapi. Majibu ya serikali ni yale yale ya kuridhisha watu ambao hawataki ukweli, lakini kwa kweli ni suala ambalo linakatisha tamaa sana katika Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, migogoro ya Ardhi ripoti ya Waziri inasema maneno mazuri sana na naomba ninukuu sehemu hii.

"Mhe. Spika, Mhe. Makamu Wa Pili wa Rais yeye mwenyewe huwa anafuatilia sana masuala ya ardhi na mara kwa mara huwa anakemea masuala ya migogoro ya ardhi kupitia hotuba zake za kuahirisha Baraza la Wawakilishi pamoja na mazungumzo yake na wawekezaji tofauti na wananchi. Ukweli ni kuwa anachukizwa sana na suala hili."

Mhe. Mwenyekiti, hayo ndio majibu kwamba migogoro ya ardhi hatua iliyochukuliwa na serikali hii ni kutokana na makameo ya Makamu wa Pili wa Rais kwenye Baraza wakati akifunga Baraza na anapooonea na wawekezaji na wananchi na kwamba Makamu wa Pili wa Rais anachukia sana suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa maagizo ya Mtume (*S.A.W*) jambo likiwa baya, Mtume ametuagiza kwamba uliondoe kwa mkono wako, na kama huliwezi basi ulikemee na kama hayo huyawezi basi uchukie. Kwa hiyo Makamu wa Pili wa Rais yeye anachukia, lakini Mtume (*S.A.W*) kasema hiyo ni imani dhaifu, kwa hivyo badala ya kuondosha kwa mkono au ukasema sasa unachukia.

Mhe. Mwenyekiti, tuambiane ukweli, migogoro ya ardhi haijatatuliwa na ni kwa sababu kwamba waliohusika ni sisi wenyewe viongozi miongoni mwetu. Kwa hiyo nadhani kazi hii kwa kweli ni kubwa. Kila kukicha migogoro inaongezeka. Kama Wawakilishi wataambiwa walete ushahidi kama ushahidi utachukuliwa basi serikali itaona jinsi ambavyo migogoro ya ardhi inaongezeka kwa *speed* kubwa, tena katika maeneo ambayo ni maeneo nyeti ya serikali na ni maeneo muhimu kwa maslahi ya viongozi na wananchi wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi niseme tu kwamba mimi sioni kitu cha kukisema, kwa kweli wenzangu wamezungumza maneno mazito kwamba hatuoni hatua za serikali. Lakini mimi binafsi naamini kwamba udhaifu huu wa serikali ni udhaifu wa Wawakilishi wenyewe. Ingekuwa Wawakilishi wanajua wajibu wao, serikali ingefanya wajibu wao kwa mujibu wa sheria, lakini madamu Wawakilishi wenyewe ni dhaifu, acha na serikali iwe ni dhaifu.

Mhe. Mwenyekiti, nina hakika hapo ulipo ingelikuwa upo hapa nyuma basi leo ungenijibu. Maana yake humu kila mtu Waziri, kila mtu Naibu Waziri, *baah!* tabu tu kusema kweli. Mimi naona kwamba Wawakilishi ni dhaifu na ndio maana serikali ikawa dhaifu mara zote. Nakushukuru sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante, ilikuwa ni nafasi ya Mhe. Saleh Nassor Juma, lakini kwa vile yeye anaendelea kufanya kazi ya kukusanya maoni, nafasi hii sasa inaondoka kwake na inakwenda kwa Mhe. Marina Joel Thomas na baada Mhe. Mohammed Haji Khalid ajiweke tayari.

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi kuchangia ripoti hizi za wizara tatu. Pia nawapongeza Mawaziri kwa kazi waliyoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, nitachangia katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, nitaanza katika Agizo la pili. Ripoti hii kuna maagizo ambayo yametokelezwa, kuna maagizo ambayo yamo mbioni yanaendelea kutekelezwa, hizi zote ni hatua. Ukizisoma zinaeleza hizi ripoti na kila hatua imeelezwa na penye mapungufu pia imeeleza.

Mhe. Mwenyekiti, Agizo namba mbili suala la ujenzi wa nyumba za viongozi. Nyumba za viongozi ni muhimu sana kujengewa, wakijengewa nyumba ina maana inapunguza hata zile gharama za kodi za nyumba ambazo zinatimia pesa nyingi katika bajeti zetu. Hapa nitilie msisitizo katika Wizara husika hii utiliwe mkazo ili hizi nyumba za viongozi zijengwe na hatimaye tupunguze zile gharama ambazo wanakodiwa viongozi wetu kwani pesa nyingi zinakuwa zinatimika, pesa ambazo zingekwenda kwenye maendeleo ya wananchi katika huduma za afya, huduma za elimu, miundombinu na kadhalika. Hapa nasisitiza tu kwamba ujenzi wa nyumba za viongozi ni muhimu serikali ilichukue suala hili kwa bidii kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika Agizo namba kumi na sita katika ripoti hii hii ya Makamu wa Pili wa Rais, ipo katika *page* 21. Hii naisema kwa sababu mchangiaji mmoja hapa alisema kwamba watoto wamepewa ili waombe, naomba ninukuu kwanza, Agizo namba kumi na sita.

"Kamati inakumbushia kusaidiwa masomo na matunzo kwa watoto ambao waliondokewa na wazee wao katika ajali ya *MV. Spice Islander* ishughulikiwe ipasavyo".

Mhe. Spika, alisema, serikali iliwapatia fedha zilizotolewa kwa wahusika wote ambapo walielezwa kuwa fedha hizo zisaidie katika kuwasomesha watoto hao. Serikali pia itaendelea kuwapatia huduma baadhi ya watoto hao wengine"

Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna Mjumbe aliyepita alisema kwamba watoto wametakiwa wadai haki zao za madai hizi. Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii hapa naomba muisome na baada ya kusema hivyo imeeleza.

"Aidha wahusika na jamaa wa wahusika wa maafa hayo wana haki ya kuomba fidia kupitia taratibu za kisheria kama ilivyopendekezwa na ripoti ya Tume iliyoundwa na Mhe. Rais, kuchunguza ajali hiyo."

Hapa Mhe. Mwenyekiti, ripoti haijataka watoto kudai fidia, haijasema katika ripoti kitu chochote. Imesema jamaa wa wahusika wa watoto hawa ambao wamepata maafa haya wadai fidia kisheria lakini sio watoto, haijasema ripoti hii watoto waombe fidia hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wakichangia wasikate maneno wachangie waseme maneno ambayo yanaleta hasa maana, ukisema nusu ina maana unapotosha watu. Humu haijaandikwa mtoto aombe fidia, imesemwa tu jamaa, wahusika, wazee waombe fidia kwa watoto wao.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika Agizo namba kumi katika Afisi hiyo ya Makamu wa Pili wa Rais, ambayo inasema kuhusu suala zima la vifaa mbali mbali vinavyokabiliana na maafa. Mimi nasisitiza tu kuwepo kwa vifaa vya maafa ni muhimu kwa sababu hatujui muda gani maafa yanaweza yakatokea. Hatuombei hayo, lakini tunatakiwa tujiweke tayari ili tusirudie makosa. Tukijiweka tayari vifaa vipo likitokea suala lolote tunaweza kulihami kwa njia yoyote ile. Hapa naomba nisisitize tu serikali ilianganalie kwa kina suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nitakwenda katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kuna agizo hili la namba moja, *page* namba 2. Mhe. Mwenyekiti, suala la UKIMWI, madawa ya kulevya, mazingira yote yanamuhusu, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Nitakwenda katika suala zima la ujenzi wa kituo kile cha kurekebisha tabia ambacho kilikuwa kianzishwe Tunguu na kimehamishiwa Kidimni.

Mhe. Mwenyekiti, hapa naunga mkono kwa sababu tutawalea vijana wetu ambao wameathirika. Lakini kwa nini tusilenge katika kuzuia huu uingizaji wa madawa ya kulevya. Tutajenga vituo, tutawaweka hawa vijana wetu, vijana hawa watahitaji huduma, vijana hawa itabidi watafutuiwe shughuli mbali mbali ambazo watafanya ili wasirudie tena madawa hayo. Naomba Wizara au serikali ijikite katika kuzuia uingizaji wa madawa ya kulevya, kuliko tukaamua kujenga vituo. Vituo hapa tutaiibebesha mzigo serikali, mzigo ambao kwa kweli utashindwa baadae kutekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, vijana watazidi kuendelea kuathirika kula madawa, tutajenga vituo na waingizaji watafurahi kwa sababu wanajua tukishaleta wakishatumia watajengewa majumba ya kurekebisha tabia. Kwa nini tusijikite katika kuzuia haya madawa. Naomba serikali au wizara husika ijikite katika kuzuia sio kulenga kujenga vituo mbali mbali vya kurekebisha tabia.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika Agizo namba saba, kuhusu miradi ya wawekezaji. Nakumbuka zamani miradi hiyo ya wawekezaji kabla haijatekelezwa kunakuwa na taratibu zinafuatwa. Miradi hii kabla haijatekelezwa kunapelekwa barua katika Wizara ya Ardhi, Tawala za Mikoa, ambao kupitia Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa, wanapelekewa ule mradi, wanatakiwa watoe maoni yao. Kwa hiyo kama Wilaya ina maana kwenye ule mradi husika, kwa mfano mradi unafanywa Nungwi ina maana Wilaya ya Kaskazini (A) inakwenda kuangalia lile eneo husika la mradi, inajaribu kuwauliza wananchi na inatoa maoni yake kuhusu mradi ule. Wanasema tunapendekeza mradi huu uwe kwa sababu utasaidia kadha, kadha kwa wananchi mambo kama ya ajira, au tunaomba usiwe kwa sababu una madhara haya na haya.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi inatoa maoni yake, Tawala za Mikoa kupitia Mikoa na Wilaya, inatoa maoni yao na wadau mbali mbali na wao wanatoa maoni yao. Mradi hata ukikubaliwa katika *ZIPA* unakuwa umeshakusanya maoni ya taasisi mbali mbali. Kuliko sasa hivi inavyofanyika *ZIPA* tu ndio inayoamua kuupokea mradi wakati haijatao taarifa hizo katika taasisi hizo. Nimejaribu kuulizia utaratibu huo, nimeambiwa haupo sasa

hivi. Sisi katika Kamati yetu ya Mazingira tuliuliza suala hili, wanasema Wizara ya Ardhi hawapelekewi hiyo taarifa ya mradi kutoa maoni yao, utaathiri vipi kimazingira, utaathiri vipi nini. Lakini utaratibu huo umekufa,

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Waziri kwamba taratibu hizi zirudi. Ndio maana saa nyengine miradi inafanyika matatizo yanajitokeza kati ya wananchi na wawekezaji, lakini ingepitia katika zile taratibu za zamani ingesaidia kupunguza hizi changamoto ambazo zinajitokeza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia Mhe. Mwenzangu hapa aliiomba dua ikifika Oktoba suala la uchaguzi CUF ishinde na mimi naiomba CCM iendelee kushika madaraka. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata nafasi ya kutoa machache kuhusu maoni ya Kamati inayoshughulikia Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha jioni hii kukutana hapa kuendelea na kazi zetu za kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, pia nikupongeze wewe kwa kunipa nafasi wakati huu baada ya sala ya Magharibi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze na hili Baraza wenyewe la Wawakilishi, tokea lilipoanza Baraza hili miaka minne nyuma huu wa tano ilikuwa tunaingia kwa mlango mkubwa na hatimaye tunatoka kwa milango mengine iliyobakia kwa jinsi mtu anavyopenda mwenyewe kutoka, lakini kuanzia kipindi hiki hili Baraza limekuwa ni *one way traffic* kuingia hapo hapo utokee hapo hapo.

Sababu za kufanyiwa hivyo sizijui, lakini huu mjengo tujaalie sasa hivi liripuke hili hapa tunatokea wapi, sote tumefikichana hapa tu lakini baadae wengine wangeelekea huko, sasa sote tunafikichana pale tunakufa wengi. Ni sababu zipi za msingi ambazo zimefanya milango mengine ifungwe na zamani ilikuwa wazi kutumia yote. Ni sababu zipi hasa za msingi ambazo tutaridhika nazo kuwa ni kweli kuna haja ya kufungwa na kuacha usalama wetu kwa sababu panapo usalama unaofikiriwa ni usalama wa sisi humu ndani, pindi huu mjengo ukiripuka tutokee wapi, mnaona upande mmoja tu au tupondane pondane. Mhe. Mwenyekiti hili ningomba nipate majibu mazuri ya Serikali.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, mimi miaka miwili na nusu ya mwanzo nilikuwemo katika Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na pale Migombani kuna nyumba nzuri imejengwa ni nyumba ya Baraza nasikia ni nyumba ya Mhe. Spika. Wakati nilipokuwa katika kamati na nyumba ile ilikuwa haijakamilika tumepewa maelezo kuwa kwa wakati huo ilikuwa tayari ishatumia milioni mia tisa na ilikuwa haijakamilika. Leo nadhani imekamilika sijui imetumia kiasi gani. Je, Mhe. Mwenyekiti, nyumba ile tayari inakaliwa, na kama haijakaliwa kwa nini au bado haijakamilika kujengwa kama haitumiki ina maana Baraza linatumia pesa kiholela au kuna sababu yoyote ya kukaa vile ilivyokaa.

Sisi kule kwetu nyumba ukijenga ikimalizika asikae mtu tunasema anahamia shetani, na mashetani wako wa aina nyingi hata watu ni mashetani. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ningetaka kujua vile vile kwa nini kama imekamilika na kama haijakaliwa kwa nini haikaliwi. Kama haina haja basi iuzwe, lakini Serikali au Baraza kutumia pesa chungu nzima zilizotumiwa kwa jengo ambalo halina haja ni upotevu wa pesa bure.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokwenda kwa mpangilio kama walivyokwenda watu hapa na pale nitasema itakayonijia mwanzo halafu nitakwenda vyengine, kwa sababu wote watatu hawa ni wakubwa. Nirudi kwenye Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora kwenye haya matengenezo ya Ikulu ya Mkoani.

Mimi nimeandika matengenezo wao wenyewe wameandika ukarabati. Matengenezo haya kwa nyinyi watu wa sasa ukarabati huu ulianza zamani na nadhani umekamilika, sasa kamati inashauri kujengwa uzio na kupanda bustani kwa ajili ya kuzuia mmong'onyoko.

Mhe. Mwenyekiti, nikwambie pale iko miti mikubwa mbali ya bustani na inaporomoka kulingana na mmong'onyoko wa ile ardhi. Kwa hivyo pale hapataki bustani, ule mlima unataka kujengwa kuzuia usimong'onyoke, vyenginevyo iko siku ile nyumba ya Ikulu itaning'inia kwa kupanda bustani tu itamong'onyoka kwa mvua na mabadiliko haya yaliyoko. Kwa hivyo kupanda bustani haitosaidia kitu.



Halafu Mhe. Mwenyekiti, kumezungumziwa kupatikana hati miliki kwa majengo ya Ikulu kwa upande wa Pemba. Serikali imejibu kuwa tayari imepatikana kwa Ikulu ya Chake Chake na ya Mkoani, lakini je, niulize Serikali ina hakika kuwa ina hati miliki kwa hizi Ikulu za Unguja? Ya Chake Chake na Mkoani tayari imepatiwa, je, hizi nyengine hati miliki zipo? Kwa hivyo kama hazipo zitafutwe na zipatikane.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Ofisi hii takriban ina Idara za Majanga matupu Idara na Tume. Kwa hivyo ina matatizo makubwa kwa sababu inakabiliana na kupambana na madawa ya kulevya, UKIMWI, mazingira na mengineyo yote haya ni mambo makubwa mno. Sasa Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii au Ofisi hii inahitaji kufanya kazi kubwa sana.

Nije kwenye madawa ya kulevya. Haya yanaingia Zanzibar mengine yanabakia Zanzibar kulingana na taarifa za kidunia na mara nyengine Zanzibar ni kama njia ya kupitia hizo dawa kuelekea sehemu nyengine duniani.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali hili ni tatizo la kitaifa lazima kutafutwe mbinu madhubuti na kabambe za kupambana na madawa ya kulevya tusiwashikilie wenye kesi mbili tatu lakini tuwatafute ma-agent na matajiri wanaoingiza kama kweli Serikali iko *serious* juu ya suala hili, basi mkamate yule kijana anasema aa ndege ile ni ya kwangu, wamtafute ni nani aliyemsababishia kijana yule aone ndege inayopita kuwa ni ya kwake, yaani muingizaji tajiri yule kauziwa tu kidogo, lakini yuko mtu anauza kilo sita, saba, nane ni kweli hatuwaoni au hatuwajui au tunafumba macho.

Tulipokuwa watoto sisi tunacheza tunasema shetani anapita fumba macho usimuone, je, na sisi hawa wakiingia tunafumba macho tusiwaone. Serikali sidhani kuwa haiwajui, kwa sababu sisi bado tuko wachache tunajuana nyendo na tabia za kila mmoja wetu.

Sasa kwa suala kama hili si vyema tukalindana na hatimaye tukamchukulia hatua yule mdogo na tukasema unaenda Chuo cha Mafunzo kwa miaka kadhaa iwe ni funzo kwake na wengine wenye tabia kama hizo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, Serikali ishirikiane katika kusimamia uingizwaji wa madawa ya kulevya, vyenginevyo *Sober Houses* na mengineyo yatakuwa ni kama vituo vya kucheza tu. Uhifadhi ni kuzuia, kujaribu kwa nguvu zote kujaribu kuzuia uingiaji wa hayo madawa yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine katika Ofisi hii ni la mazingira. Kitengo hiki kina kazi kubwa na kama wataalamu wake ingelikuwa wanasikilizwa, wanafuatwa ushauri wao katika masuala ya kimazingira katika mambo tunayotekeleza basi matatizo mengi ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira ungelipungua, ungelibakia ule wa kimaumbile ambao uko nje ya uwezo wa mwanaadamu. Lakini kila mmoja anafanya anavyotaka, anafanya anavyopenda na baadhi ya wakati Idara hii inakosa meno kushughulikia masuala yanayowahusu.

Miradi mara nyengine mpaka inakamilika ndio wanatakiwa ushauri wa Mazingira wafanye nini na hili ndio tatizo letu mara nyingi hapa kwetu, utahisi pahala hapa hata nyumba ya kawaida si pa kujenga lakini ataachiwa mtu atajenga mpaka ataezeka ndio anakuja mkubwa hapa hapafai kujenga. Ikiwa ubavu wake mdogo jengo lake litaondolewa, ikiwa ana ubavu jengo lake litaendelea. Tushaona miradi kadhaa iliyochukuliwa hatua kuwa isimame kuwa yamejengwa mahala simo maeneo ya wazi, Serikali ikachukua hatua hatimaye jengo hilo lililochukuliwa hatua likaendelea kujengwa. Hapa kuonesha Serikali bado haijakuwa imara ya kusimamia yale ambayo wanataka yawe na kuyakataza yale ambayo wanataka yasifanyike.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwenye Idara ya Maafa. Idara hii isikae kutokee maafa ikawa kama ni kitega uchumi, iwe ni Idara ambayo itashughulika kukabiliana na maafa, na maafa yanaweza yakatokea nchi kavu, ardhini na angani. Je, Serikali inavyo vyombo madhubuti vya kukabiliana na matukio mbali mbali ambayo yanaweza yakatokea. Je, Serikali imejiandaa vipi na masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia niende kama *msumeno mbele na nyuma kukereza*, nimalizie kwa ile niliyoanzia kwenye Utawala Bora Ikulu ya Mkoani ukarabati wake. Mhe. Mwenyekiti, ningependa nijue kuwa ni kiasi gani ya fedha zilitumika katika kuikarabati, nitumie neno kama mnavyotumia nyinyi wenyewe ile Ikulu ya Mkoani. Ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe huku nina orodha ya watu watano ambao wamebakia hawa tutaendelea nao siku ya Jumatatu *inshaallah* tukijaaliwa, itakapofika wakati wa kuchangia tutaanza na Mhe. Mussa Ali Hassan, akisaidiwa na Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Farida na wengine watafuatia.

Lakini tukiacha hayo kuna matangazo mawili hapa. Tangazo la kwanza linahusu semina ambayo itafanyika kesho kwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria lakini na Wenyeviti pamoja na Makamu Wenyeviti, katika ukumbi wetu wa Baraza la Wawakilishi hapa hapa.

Halafu siku ya Jumapili kuna tangazo jengine la Semina ya *Angoza* ambayo hii inawahusu Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi na munaombwa sana muhudhurie katika semina hii. Itafanyika katika ukumbi wetu wa Baraza la Wawakilishi na tunaombwa semina hii ianze saa 4.00 za asubuhi *inshaallah* na mambo yale mazuri yatakuwepo pia munaombwa muelewe hivyo.

Baada ya maelezo hayo sasa Waheshimiwa Wajumbe muda wetu tulionao hautoshi kwa jambo lolote la ziada, kwa hivyo tunachukua fursa hii kuwashukuru sana kwa namna ambavyo tulishirikiana kwa pamoja hadi kufikia hapa kwa siku ya leo. Sasa nachukua fursa hii kuahirisha Baraza hili hadi siku ya Jumatatu tarehe 23/03/2015 saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 1:35 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 23/03/2015 saa 3:00 za asubuhi)*

